# Nipashe

Alhamisi Februari 27, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580165

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



ama
AFYA NA MAZINGIRA
Maboresho Hospitali Temeke yatokomeza vifo kujifungua
'Mabonge' wakerwa kukataliwa katika ndege
Hdoa jinsia moja ilivyoanzia kujificha zama hizo hadi uzazi
KICHOCHO
'Kinawawinda' watoto wawapo majini, kukabili kinahitaji 'misuli'

UKURASA 13

## NEC yaombwa kutoa mwongozo ulinzi wenye ualbino uchaguzi

UKURASA 3

# Sugu asimulia kuteta kwa simu na Bashiru

• **Asema** hashtushwi madiwani 11 kutimkia CCM, atamba bado ana mtaji wa kura 250,000 uchaguzi Oktoba...*Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 8

**SAMIA ATAKA AJENDA YA 50/50 ILANI ZA VYAMA**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amesema katika mchakato wa uchaguzi mkuu unaotarajiwa...


## Ugonjwa corona waingia Algeria

UKURASA 25

## Jumatano ya Majivu



Rais Dk. John Magufuli, akipakwa majivu na Paroko wa Kanisa Katoliki la Mtakatifu Petro, Parokia ya Oysterbay, Padre Dk. Alister Makubi, aliposhiriki Ibada ya Jumatano ya Majivu, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni mkewe Mama Janeth Magufuli. **PICHA: IKULU**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store




## Wachina waliomhonga bosi wa TRA wapigwa faini ya milioni 2/-

UKURASA 2


**MICHEZO** KILI CANVAS HABARI YA MJINI MOSHI UK.31 **MAONI, KATUNI** UK.6

## Waliomhonga Kamishna TRA watozwa faini mil. 2/-

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, imewahukumu raia wawili wa China, mke na mume, kulipa faini ya Sh. milioni mbili na kutaifisha Dola za Marekani 5,000 (sawa na Sh. milioni 11.5) walizotoa rushwa kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Dk. Edwin Mhede.

Kadhalika, mahakama hiyo imewataka washtakiwa hao , Zheng Rongnan (50) na Ou Ya (47), kurudi TRA kufanya makubaliano ya kulipa kodi ya Sh. bilioni 1.3 wanayodaiwa.

Hukumu hiyo dhidi ya watuhumiwa wakazi wa Kinyambo Mafinga C, Iringa ilisomwa na Hakimu Mkazi Mkuu Huduma Shaidi.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Ipyana Mwakatobe, alidai kuwa Februari 24, mwaka huu, washtakiwa wote wakiwa katika Makao Makuu ya TRA, Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam, walitoa rushwa ya Dola za Marekani 5,000 sawa na Sh. milioni 11.5 kwa Kamishna Mkuu, Dk. Mhede kama kishawishi kwamba awasaidie kampuni yao kutolipa kodi ya Sh. bilioni 1.3 kiasi ambacho kilipaswa kuilipa mamlaka hiyo.

**Washtakiwa walikiri mashtaka yao.**

Mwakatobe aliwasomea maelezo ya awali kwamba mshtakiwa wa kwanza ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Ronglan Intranational Industry Ltd., inayojishughulisha na uzalishaji wa Marine Plywood na pia ni msimamizi wa shughuli zote za kampuni hiyo.

Alidai kuwa kampuni hiyo inayomilikiwa na washtakiwa kama mke na mume, ilikaguliwa na maofisa wa TRA na kubainika kwamba wanatakiwa kulipa kodi ya Sh. bilioni 1.3, kiwango ambacho kilitakiwa kulipwa au kuwekewa pingamizi kama walikuwa hawajaridhishwa na makadirio hayo yaliyofanywa Februari 21, mwaka huu. Upande huo wa Jamhuri ulidai kuwa Februari 24, mwaka huu, washtakiwa walikwenda Makao Makuu ya TRA kwa Mkurugenzi Mkuu, wakidai kuwa kampuni yao imekadiriwa kiwango kikubwa ambacho kilipaswa kulipwa kwa mamlaka hiyo.

Ilidaiwa kuwa siku ya tukio, saa 10 alasiri washtakiwa walikutana na Dk. Mhede ofisini kwake akiwa na msaidizi wake, walimweleza tatizo hilo la kodi pamoja na kuwasilisha nyaraka mbalimbali wakionyesha wamekadiriwa kiwango kikubwa cha kodi na kumwomba atatue mgogoro huo.

Upande huo wa Jamhuri ulidai kuwa baada ya kuwasilisha maombi kwa Kamishna Mkuu, walichukua burungutu la fedha za kigeni na kumkabidhi kama kishawishi cha kuwasaidia katika suala la kodi kiasi kilichostahili kulipwa TRA.

Baada ya washtakiwa kutoa burungutu hilo, bosi huyo namba moja wa TRA alimwelekeza msaidizi wake kuhesabu na kubaini ni Dola za Marekani 5,000 noti 50 za Dola 100 kila moja.

Ilidaiwa kuwa Dk. Mhede alitoa taarifa za tukio Takukuru na washtakiwa wote walikamatwa na maofisa wa taasisi hiyo wakiwa na nyaraka pamoja na fedha hizo. Februari 25, mwaka huu washtakiwa walifikishwa katika Mahakama hiyo na kusomewa shtaka la kujihusisha na rushwa. Upande wa Jamhuri uliwasilisha vielelezo vinne ikiwamo, nyaraka za ukamataji, nyaraka waliyowasilisha kwa kamishna, Dola na barua ya mshtakiwa aliyomwandikia bosi wa TRA.

Washtakiwa walikiri maelezo yote ya awali.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa washtakiwa ni wakosaji wa mara ya kwanza hawana kumbukumbu za makosa ya zamani, mahakama itoe adhabu kali ikiwamo kutaifishwa Dola 5,000 kuwa mali ya serikali.

Upande wa utetezi ulidai kuwa, washtakiwa ni wakosaji wa mara ya kwanza, wawekezaji hapa nchini na wana familia ambayo imebaki nchini China iko katika kipindi kigumu wakati wa mlipuko wa maradhi ya Corona inawategemea wao.

Hakimu alisema washtakiwa watalipa faini ya Sh. milioni moja kila mmoja, fedha walizotoa rushwa zinataifishwa kuwa mali ya serikali na kwamba wakifanikiwa kulipa wapelekwe TRA kufanya makubaliano ya kulipa kodi wanayodaiwa.



Raia wa China, Zheng Rongman na mkewe Ou Ya, wakiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana, kabla ya mahakama hiyo, kuwahukumiwa kulipa faini ya Sh. milioni mbili na kutaifisha Dola za Marekani 5,000 (sawa na Sh. milioni 11.5) walizotoa rushwa kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Dk. Edwin Mhede. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Sugu asimulia kuteta kwa simu na Bashiru

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

SIKU chache baada ya madiwani 11 wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) jijini Mbeya kujiunga na Chama Cha Mapinduzi, Mbunge wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi 'Sugu', amedai kuzungumza kwa simu na Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ali, kuhusu suala hilo.

Jumatatu, Dk. Bashiru akiwa jijini Dodoma, aliwapokea madiwani hao 11 kutoka Chadema waliongozwa na Meya wa Jiji la Mbeya, David Mwashilindi, huku sababu kuu ya kutimkia kwao CCM ikidaiwa kuwa kuvutiwa na utendaji wa Rais John Magufuli.

Baada ya kuwapokea, Dk. Bashiru alisema mitambo aliyoweka ya majaribio kwenye mikoa jirani, imemfikia Mbunge wa Mbeya Mjini (Sugu), akifafanua zaidi kuwa:

"Wamenieleza kwanini wanafanya uamuzi huo mzito, nimefurahi sana kwa kuwa kazi yangu ni kuhakikisha chama kinafurahiwa na Watanzania wote, nadhani sasa ratiba yangu ya kwenda Mbeya itabidi iwahi, niwahi haya maji bado ya moto nikutane na rafiki yangu Sugu.

"Mwaka jana nakumbuka nilimtumia salamu kuwa nakuja 'kuseti' mitambo, kumbe hii mitambo ninayofunga mikoa ya jirani inafika hadi Mbeya, ila lazima niende kufunga Mbeya mitambo maana kila mkoa una mitambo yake."

Akizungumza jana kwenye mkutano wa viongozi waandamizi wa Chadema Kanda ya Nyasa uliofanyika jijini Mbeya jana, Sugu alidai kupigiwa simu na Dk. Bashiru baada ya madiwani hao kujiuzulu uanachama wa Chadema na kujiunga na CCM.

Sugu alidai madiwani wote walioondoka Chadema, walikuwa wamekata tamaa ya maisha ya siasa.

"Juzi alinipigia simu Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ali, akitaka kujua hali yangu na nilichomjibu nilimwambia 'wewe ni rafiki na mtani wangu, lakini kwa sasa umekuwa ndugu kwa sababu umeniimarisha kisiasa kuliko wakati wowote,' nilimwambia hivyo kwa sababu ametuondolea mizigo," alisema.

Sugu alisema kuhama kwa madiwani hao 11 akiwamo Meya, Mwashilindi na Naibu Meya, Fanuel Kyanula, hakujakidhoofisha chama hicho, bali kumekiimarisha zaidi.

Alisema awali baada ya kupata taarifa ya madiwani hao kutimka, alipata wasiwasi kwamba chama hicho kitakuwa kimepoteza mwelekeo, lakini alipofanya utafiti mdogo kwenye baadhi ya maeneo, alibaini bado kinakubalika kwa wananchi.

Msanii huyo wa Hip Hop alisema hofu yake ilikuwa huenda madiwani hao walihama pamoja na wanachama, lakini utafiti wake ulibaini wameondoka peke yao na familia zao na sio wanachama wa Chadema ambao ndiyo wapigakura wake.

Alidai Meya wa Jiji la Mbeya, Mch. Mwashilindi, alikuwa hashiriki kwenye shughuli za chama hicho kwa muda mrefu, akieleza kuwa hata mkutano mkuu wa Chadema uliofanyika mwishoni mwa mwaka jana jijini Dar es Salaam hakuhudhuria.

Mbunge huyo alidai Chadema ina mtaji wa wapigakura zaidi ya 250,000 ndani ya jiji hilo, akibainisha kuwa 200,000 ni wanachama wa chama hicho na wengine zaidi ya 50,000 ni wanachama wa CCM na vyama vingine.

Alisema kupitia kampeni yao ya Chadema ni Msingi, chama hicho kimeandikisha wanachama zaidi ya 60,000 na kwamba mpaka kufikia Juni mwaka huu, kitakuwa kimeandikisha wengine 100,000 na mpaka kufikia tarehe ya uchaguzi mkuu Oktoba mwaka huu, kitakuwa na uhakika wa wanachama 200,000.

Kuhusu picha ambayo imekuwa ikizunguka mitandaoni ikimwonyesha yeye na baadhi ya vijana wa CCM, Sugu alisema ni ya mwaka 2017 wakati wa ziara ya Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ambayo vijana hao walimwomba apige nao picha.

"Wale vijana baada ya kuniona mimi mbunge wao, waliniomba tupige picha, mimi nisingeweza kukataa kwa sababu najua wale ni wanachama wa CCM mashati, lakini mioyoni mwao ni wapigakura wangu japokuwa ile picha imeanza kutumika vibaya," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Nyasa, Joseph China, alidai madiwani 11 waliohamia CCM, walianza muda mrefu kufanya majaribio ya kukihama chama hicho na kujiunga na chama tawala, lakini wakawa wanazuiwa na viongozi.

Alidai mwaka 2018 wakati wa ziara ya Katibu Mwenezi wa CCM Taifa, Hamphrey Polepole, baadhi ya madiwani hao walikuwa wanatakiwa kuhudhuria mkutano wake ili wapokewe, lakini alilazimika kujifungia nao kwenye ofisi za kanda siku nzima ili kuzuia jaribio hilo.

"Mwaka jana, Meya wa Jiji alikuwa anatakiwa aongozane na madiwani wote wa chama kwenda bungeni jijini Dodoma kwa mwaliko wa Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson, lakini tulizuia na madiwani wetu watatu walienda na baada ya siku chache wakahamia CCM," alidai.

# NEC yaombwa mwongozo ulinzi kwa wenye ualbino

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la kimataifa la Under The Same Sun (UTSS) limetoa wito kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec) kuweka mwongozo na kanuni ambazo zitawezesha wagombea wenye ulemavu wakiwamo wenye ualbino wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu kutokejeliwa na wenzao.

Mwanasheria wa Shirika hilo, Maduhu William, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati UTSS ikiadhimisha miaka 11 tangu kuanzishwa kwake.

William alisema Ibara ya tano ya Katiba inatoa haki ya mtu kuchagua na kuchaguliwa hivyo wagombea wenye ulemavu wa aina zote wasikejeliwe bali washindane kwa hoja majukwaani.

"Tume ya uchaguzi iweke mwongozo na kanuni ambazo zitasaidia wagombea wenye ulemavu wakiwamo wenye ualbino, walindwe kwa sababu ipo tabia ya wagombea wakati wa kujinadi kutoa lugha za kejeli au kashfa, matusi au kumuainisha mtu kwa ulemavu alionao.

"Tulishuhudia jambo hili mwaka 2015 Lindi Mjini kulikuwa na mgombea ubunge wa Chama cha Wananchi (CUF) mwenye ualbino alilalamika alikuwa akikejeliwa na mpinzani wake."

Alisema kumuainisha mtu ulemavu alionao kunashusha ari ya kuendelea na uchaguzi.

William alisema miaka ya nyuma wameshuhudia matukio ya kujeruhiwa ama kuuawa watu wenye ulemavu wa ngozi.

"Tunaamini uchaguzi huu unaotarajia kufanyika mwezi Oktoba utaisha bila ya kusikia tukio lolote la mtu mwenye ualbino kuzuriwa ama kuuawa," alisema.

Kuhusu miaka 11 ya shirika hilo, William alisema elimu iliyoendelea kutolewa kwenye jamii imewezesha kupunguza matukio ya wao kukatwa viungo au kuuawa.

"Wahalifu badala ya kutuua au kutujeruhi wamebadilisha mbinu, hivi karibuni huko Mbeya na Njombe kumejitokeza matukio ya kufukuliwa makaburi ya zamani ya ndugu zetu waliozikwa na wahalifu kuchukua viungo na kwenda navyo kusikojulikana, tunaomba vyombo husika viwachukulie hatua wahusika wote," alisema.

Vile vile shirika hilo limemshukuru Rais John Magufuli pamoja na serikali kwa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha hakutokei matukio ya kuuawa ama kujeruhiwa.

William alisema tangu mwaka 2009 Shirika hilo lilipoanzishwa limewanufaisha kielimu jumla ya watu wenye ualbino 420 ambao miongoni wamo waliohitimu vyuo vikuu na kupata ajira kwenye taasisi, idara na mashirika mbalimbali.

Alisema elimu inayoendelea kutolewa kwa makundi mbalimbali imewezesha wazazi wenye watoto wenye ualbino kwenda katika shirika hilo kupata elimu namna ya kuwalea ili wasipate saratani ya ngozi.

"Kwa mwaka huu hadi sasa jumla ya familia sita zimejitokeza na mwaka jana zilikuwa zaidi ya 30, wanakuja kuomba ushauri wa malezi ya watoto wao na wengi wanataka kujua matumizi ya losheni ili kuzuia mionzi ya jua," alisema.

Aliiomba serikali kuharakisha kesi za wenzao zilizopo mahakamani ambao walipatwa na majanga ya kuuawa au kujeruhiwa kuanzia miaka ya 2008 ili haki itendeke.

# Mchakato bucha nyamapori waiva

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori (Tawa), imemaliza mchakato wa uandaaji wa kanuni za kuanzisha bucha za wanyamapori.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Naibu Kamishna wa Mamlaka hiyo, Imani Nkui, alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli kuanzishwa kwa uuzaji wa nyama hiyo ili kupunguza tatizo la ujangili na uwindaji haramu katika hifadhi na mbuga za wanyamapori nchini.

"Kwa kuwa kanuni zimetoka siku 10 au 15 zilizopita, mchakato wa kumshauri waziri maeneo haya, unapaswa kufanywa na kamati ambayo inatokana na wataalamu wa sekta mbalimbali kama afya, Chuo cha Sokoine cha Kilimo (SUA)," alisema.

Aliongeza kuwa kuna mambo yanayotakiwa kuzingatiwa kwenye biashara ya wanyamapori, kubwa ikiwa ni ulinzi wa afya ya jamii.

"Tutapendekeza haya maeneo kwa kuzingatia afya ya jamii na ndiyo maana hii timu imewekwa chini ya kanuni kwamba ni lazima wataalamu wa aina hii wawapo kwa ajili ya ushauri huo," alisema.

Kamishna huyo alisema wataalamu hao watamunda kamati ya kumshauri Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hiyo.

Alisema kanuni zinaelekeza kutolewa leseni mara nne kwa mwaka ya ugawaji vitalu vya uwindaji.



# Jenerali Mabeyo aitaka JKT kuharakisha miradi ya serikali

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

MKUU wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo, ameitaka Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kukamilisha miradi inayopewa na serikali kwa wakati pamoja na kuzingatia ubora na thamani ya fedha.

Mabeyo aliyasema hayo jana kwenye hafla fupi ya ufunguzi wa jengo la makao makuu ya Jeshi hilo katika eneo la Buigili wilayani Chamwino mkoani Dodoma.

Alisema serikali imekuwa ikilitumia jeshi hilo katika miradi mbalimbali hasa ile ya ujenzi hivyo lazima kuhakikisha kuwa inakamilika haraka na katika ubora uliopangwa.

"Lazima mtekeleze majukumu yenu kwa haraka na kwa ufanisi mkubwa hii ni sifa kubwa ya kupatiwa kandarasi nyingi zaidi na serikali" alisema Mabeyo. Aidha, aliitaka JKT, kuzingatia sheria ya manunuzi katika bidhaa mbalimbali ambazo wamekuwa wakizitumia katika miradi hiyo ya serikali ili kukabilina na ongezeko la gharama za utekelezaji.

"Inatakiwa vifaa hivi ambavyo mnavitumia katika ujenzi wa miradi hii kuvinunua moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji badala ya mtu kati," alisema.

Pia Mabeyo, alilitaka jeshi hilo kutumia fursa wanazopata kutoka serikalini kwa kukabidhiwa miradi mikubwa ya kutekeleza kujiimarisha na kujijengea uwezo. "Katika utekelezaji wa miradi hii ya serikali lazima ni sisi tubadilike kwa kuanza kumiliki vifaa vyetu wenyewe na siyo hivi vya kukodi, ambavyo tunatumia sasa, kwani miradi hii inatupa uzoefu wa kutambua kazi gani inafanywa na kifaa gani, "alifafanua Jenerali Mabeyo.

Vilevile, alisema kuwa katika ujenzi wa makao makuu ya Jeshi la Wanachi wa Tanzania (JWTZ), katika eneo la Kikombo jiji Dodoma, wamepanga kuitumia JKT.

"Wakati Rais anazindua eneo la ujenzi wa makao makuu alitupatia fedha kiasi cha Sh. bilioni 10, lazima tujenge makao makuu nzuri ambayo kwa mara ya kwanza itakuwa imejengwa na sisi wenyewe, tofauti na hizi nyingine ambazo ni za kurithi,"alisema

Mkuu wa JKT, Brigedia Jenerali Charles Mbuge, alisema ujenzi huo ulianza rasmi Machi 2017.

Mbuge alisema kuwa matokeo ya jengo hilo la makao makuu, ni agizo la Rais kuzitaka ofisi za serikali kuhamia makao makuu ya nchi jiji Dodoma.



Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo, akipanda mti baada ya kuzindua majengo ya makao makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), yaliyopo Chamwino Buigiri, mkoani Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mstaafu aeleza mikakati kumlinda mtoto wa kike

**Na Hellen Mwango**

WAZAZI na walezi nchini wametakiwa kushirikiana na walimu katika malezi ya wanafunzi hasa wa kike ili kupunguza na kumaliza mimba za utotoni.

Rai hiyo aliitoa Mkuu wa kwanza wa Shule ya Sekondari ya Songea Girls, Hindu Kila (85), mwisho wa wiki wakati akifungua mkutano wa umoja wa wanafunzi waanzilishi wa shule hiyo kutoka Tarime, mkoani Mara na Msalato Mkoa wa Dodoma (TAMSALA).

Alisema pamoja na kupita vituo mbalimbali vya kazi akiwa mwalimu wa shule ya msingi, alipata uhamisho kutoka Shule ya Tabora Girls kwenda kuwa Mkuu wa Shule ya Songea Girls, ilipoanzishwa mwaka 1972.

"Nikiwa kama Mkuu wa Shule wa kwanza wa Songea Girls, nilihakikisha nazuia mimba za utotoni kwa wasichana waliokuwa chini yangu, sikukubali utaratibu waliojiwekea viongozi kuwatumia vibaya mabinti kutoka shuleni kwangu," alisema na kuongeza; "Niliweka msimamo kuhakikisha mnafikia malengo yenu, ninashukuru Mungu kila mmoja wenu alisoma kwa bidii na kufikia malengo mpaka mmestaafu utumishi wa umma."

Alisema maisha ya sasa yamebadilika wazazi, walezi na walimu hawana ushirikiano hali inayosababisha mimba kwa wanafunzi kushindwa kukomeshwa.

"Tukemee, tushirikiane, kuondoa mimba shuleni, watoto wa kike wasome wafikie malengo na kwa manufaa ya taifa zima kwa kuwa mtoto wa kike ana nafasi muhimu kwenye jamii," alisema Mwalimu Hila.

Alisema Muungano wa TAMSALA uwe chachu kupambana na wazazi wanaofanya ukatili kwa watoto wa wenzao wa kike kwa kuwaharibia maisha.

Akifafanua alisema ana uchungu na maisha ya wasichana wadogo kwa sababu wanaume wamekuwa maadui kwa elimu ya mwanamke.

Mbali ya ualimu, mwalimu Hila ameshika nyadhifa mbalimbali ikiwamo mkaguzi wa elimu na Mbunge wa Taifa tangu 1975 kwa miaka tisa na nyadhifa mbalimbali katika Wizara ya Elimu kabla ya kustaafu.

Naye Mwenyekiti wa TAMSALA, Jaji mstaafu, Pellagia Khaday, alisema umoja huo unaundwa na wahitimu wa Songea Girls wa 1976, 77,78 na 79 wenye taaluma mbalimbali kwa lengo la kupanga mikakati ya kusaidia elimu ya mwanamke.

Alisema TAMSALA wote ni wastaafu kutoka taaluma mbalimbali ikiwamo, madaktari, walimu, wanasheria, wauguzi, mainjinia, wahasibu na maofisa kilimo ambao wote kwa sasa ni wastaafu wa utumishi wa umma.

## Watakiwa kufanya toba Kwaresima

**Na Ndalike Sonda,** KAHAMA

ASKOFU mteule wa Jimbo Katoliki la Moshi na msimamizi wa kitume wa Jimbo la Kahama, Mhashamu Ludovick Minde, amewataka waamini wa kanisa hilo kukitumia kipindi cha mfungo wa Kwaresima kufanya toba na kuacha dhambi na matendo yote mabaya.

Akihubiri jana katika misa ya asubuhi ya Jumatano ya Majivu katika kuanza kwa kufungo wa Kwaresima, Kanisa Kuu la Mtakatifu Karoli Lwanga Parokia ya Kahama, aliwataka waumini kukipokea kipindi hichi kwa kufanya toba na mabadiliko.

Askofu Minde alisema kipindi cha Kwaresma ni cha kufunga na kufanya toba kwa kufanya mabadiliko ya kiroho na kimwili, kuacha mambo mabaya, kufanya toba na kumrudia Mungu.

Alisema Kwaresima ni kipindi cha unyenyekevu na kuondoa dhambi na kuwataka waamini kuwa wapya katika maisha yao, kukaa vizuri na jamii na kujitoa kuwasaidia wenye uhitaji.

Askofu Minde alisema kipini hicho ni kigumu kinamtaka kila muumini kufanya mabadiliko na kuwa wapya katika maisha popote ndani ya jamii.

"Waumini siyo kuishia kupakwa majivu tu kitumieni kipindi hichi kumrudia Mungu kujirekebisha kwa kufanya toba na kuacha mambo ya unafiki, majungu, chuki binafsi na tusirudi katika maisha ya zamani ya dhambi, alionya.

Kadhalika alisema mabadiliko watakayoyafanya yawe ndiyo maisha yao ya kila siku na kushika kwa kufauta maandiko ya neno la Mungu.

Nao baadhi ya waamini wa kanisa hilo walisema kipindi cha Kwaresima kinawarejesha katika Imani, hivyo ni jukumu la kila Mkristo kusali kwa toba na kuwa karibu na mwenyezi Mungu.

HABARI KITAIFA

## Wakutubi walilia maslahi na ajira wenye taaluma

**Na Pendo Thomas**

CHAMA cha Wakutubi Tanzania kimeiomba serikali kusimamia maslahi yao ya kazi kwa kuajiri watu wenye taaluma ya ukutubi katika maktaba mbalimbali nchini zikiwamo za shule za msingi na sekondari.

Akiongea wakati wa mkutano wa chama hicho uliofanyikia mkoani Kigoma Februari 26, Mwenyekiti wa chama cha wakutubi Tanzania, Dk. Juliana Manyerere, alisema kuwa wahitimu wengi wa fani hiyo wako mtaani kutokana na kukosa kazi.

Manyerere alisema changamoto ya ajira kwa wakutubi ni kubwa kwa kuwa shule nyingi za msingi na sekondari hazina maktaba, lakini chache zilizo na maktaba zinatumia watu wenye taaluma zingine.

"Tunao wakutubi wengi ambao wanafuzu vyuo kila mwaka tunavyuo zaidi ya kumi vinavyotoa taaluma hiyo nchini sisi tunaona hiyo ni fursa ya ajira kwa wakutubi, lakini hatuipati," alisema.

Kwaupande wake Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Willium Ole Nasha, alisema sio sahihi watu wasio na taaluma ya ukutubi kufanya kazi hiyo wakati wakiwa hawana kazi na kuahidi kuwa serikali itafanyia kazi suala hilo ili kuwezesha wakutubi kunufaika.

Ole Nasha alisema watalamu wa maktaba wanapaswa kubadilika kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia ya karne ya 21 kwa kuwa kundi kubwa lililo kuwa likihudumiwa kwenye maktaba kwa sasa linapata taarifa mbalimbali kupitia mitandao.

"Mlizoea mnahudumia wateja mnao waona, lakini sasa mambo yamebadilika, mnapaswa kujipanga kuhudumia watu msiowaona kupitia mifumo ya mtandao," alisema.

Aliwataka wakutubi kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa kupunguza mlolongo mrefu unaochosha wateja na kusababisha watafute njia mbadala ya kupata taarifa.

Mlezi wa Chama cha Waktubi Tanzania, Prof. Rweyabura Mugyabuso, alieleza kuwa kwa mujibu wa Sera ya Elimu, kila shule ya msingi na sekondari iwe na maktaba, lakini suala hilo halijatekelezeka hivyo kuwakosesha fursa wanafunzi ya kujenga utamaduni wa kujisomea.

"Naona jambo hili bado serikali hamjalipa kipaumbele kwa kuwa shule zinaanzishwa bila kuwa na maktaba," alisema.



Wafanyakazi wa kujitolea wa Shirika la Time to Help la Uholanzi, wakipaka rangi kuta za madarasa ya Shule ya Msingi Kawe B, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Serikali kujenga kiwanda cha vifaa tiba

**Na Mwandishi Wetu,**
BARIADI

SERIKALI imekamilisha mipango ya kujenga kiwanda kikubwa cha vifaa tiba, kuchakata pamba na bidhaa zinazotokana na zao hilo mkoani Simiyu ili kuongezea thamani zao hilo na kukuza soko la ndani na nje nchi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu(Uwekezaji), Angela Kairuki, alibainisha hayo jana mjini na kueleza kuwa sambamba na hilo kiwanda hicho ambacho jiwe lake la msingi litawekwa Mei mwaka huu, kitamaliza kabisa tatizo la uingizaji wa vifaa tiba kutoka nje.

"Serikali imekuwa ikiingia gharama kubwa kuagiza viuatilifu na pia kukosa soko la uhakika la zao la pamba kutokana na ukosefu wa viwanda, hivyo kiwanda kitakachojengwa kitamaliza tatizo hilo,"alisema Waziri Kairuki.

Akizungumza katika mkutano wa majadiliano kati ya sekta ya umma, wawekezaji na wafanyabiashara katika Mkoa wa Simiyu uliolenga kujadili changamoto na kupata mapendekezo yatakayosaidia kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji jana, Kairuki alisema serikali imeyapa kipaumbele mazao ya kimkakati ikiwamo zao la pamba.

"Lengo la serikali ni kupunguza uagizaji wa bidhaa na pia usafirishaji wa malighafi nje ya nchi na kuikosesha nchi mapato stahiki na kupunguza uwezo wa wawekezaji wa ndani kushindana na kukuza mitaji yao ya uwekezaji," Waziri Kairuki alisema.

Alisema azma ya serikali ya kufikia uchumi wa kati na viwanda itafanikiwa tu pale bidhaa kutoka nje zitapungua na ndiyo itakuwa silaha ya kuvilinda viwanda vya ndani.

Kairuki alitoa wito kwa Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) kuangalia namna bora ya kufikisha huduma pande zote za nchi ili kutoa fursa ya wananchi kuwekeza katika soko la hisa kwa lengo la kukuza mitaji.

"Ni lazima soko la hisa lione haja ya kujitanua na kutoa fursa kwa Watanzania wenye mitaji kuwekeza katika soko hilo ambalo litasaidia ukuaji wa uchumi na kuchochea maendeleo kwa kasi," alisema Waziri Kairuki.

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, amesema Mkoa wake umejipanga kuhakikisha fursa zilizopo za biashara na uwekezaji mkoani humo zinafanyiwa kazi ili kuleta maendeleo haraka na pia

kuziomba mamlaka za serikali kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuondoa kero kwa wawekezaji na wafanyabiashara.

"Muhimu mamlaka zilizopo nchini kuwa na utaratibu maalum wa kufanya ukaguzi kwa wawekezaji na wafanyabiashara ili viwanda viendelee na kazi na siyo muda mwingi kutumika kwa ajili ya ukaguzi pekee," alisema RC Mtaka.

Naye Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alisema Simiyu inafursa kubwa ya utalii hivyo ni jukumu la mkoa kushirikiana na wadau pamoja na Wizara kutangaza vivutio vilivyo ili mkoa uweze kunufaika na rasilimali utalii.

"Simiyu ipo karibu zaidi na Mbuga ya Serengeti hivyo ni fursa kwa wawekezaji kujenga nyumba za kulala wageni, viwanja vya michezo na burudani ili kuvutia watalii na wageni mbalimbali," alisema Naibu Waziri Kanyasu.

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima, aliwahimiza wafanyabiashara kutumia fursa zilizopo kuwekeza kwa kuzingatia misingi ya kanuni na sheria ili uwekezaji uwe uendelevu bila kuathiri mazingira.

## Bil. 1/- hutumika kila mwaka kifuta machozi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amesema serikali inatumia Sh. bilioni moja kila mwaka kwa ajili ya kifuta jasho na machozi kwa wananchi walioathiriwa na wanyamapori wakali na waharibifu. Mahitaji halisi yakiwa ni Sh. bilioni tatu. Aliyasema hayo jana wakati wa mkutano wa mashauriano kati ya serikali, wafanyabiashara na wawekezaji wa Mkoa wa Simiyu uliohusisha mawaziri na manaibu mawaziri kutoka sekta mbalimbali ikiwamo viwanda na biashara na masuala ya fedha, wakiongozwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Uwekezaji,

Angellah Kairuki, uliofanyika Wilaya ya Bariadi, mkoani Simiyu. Katika mkutano huo wenye lengo la kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi, wameeleza malalamiko hayo kuwa licha ya kulipwa vifuta jasho na vifuta machozi, malipo hayo yanachelewa na madogo yasiyoendana na maisha halisi ya sasa.

Akijibu hoja hizo, Kanyasu alisema serikali hailipi fidia bali hutoa kifuta jasho au kifuta machozi kwa wananchi walioathiriwa na wanyamapori wakali na waharibifu.

Alisema serikali haiwezi kuwalipa kwa mara moja watu wote walioathiriwa kwa kuharibiwa mazao au kwa kuwapoteza ndugu zao madai yanapowasilishwa wizarani kwa sababu madai ni mengi ambayo wizara inayafanyia kazi kila siku.

Kanyasu alisema baadhi ya malipo ya waathirika hao huchelewa kwa sababu bajeti inayopangwa kwa ajili ya malipo hayo hushindwa kukidhi mahitaji kutokana na ufinyu wa bajeti.

Alieleza kuwa serikali inapitia kanuni za viwango vipya vya malipo ya vifuta jasho na vifuta machozi kutokana na malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa viwango vya malipo hayo ni kidogo na hakiendani na uhalisia wa maisha ya sasa.

Akifafanua kuhusu madai hayo, Kanyasu alisema serikali hailipi fidia kwa familia iliyopoteza mpendwa wao kwa sababu hakuna fidia yenye thamani sawa na uhai wa binadamu bali hutoa kifuta machozi.

Katika hatua nyingine, Kanyasu ameziagiza taasisi za uhifadhi nchini kuunda vikosi ya kupambana na ujangili vitakavyotoa msaada unapohitajika wakati wanyamapori wakali na waharibifu wanapovamia mashamba au makazi ya watu.

Alizitaja taasisi hizo kuwa ni Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS). Alisema wizara imeamua kuchukua uamuzi huo kutokana na shughuli za uhifadhi kuimarika hivyo wanyamapori kama tembo wamekuwa huru kutembea kila sehemu bila hofu ya kuuawa.

Pia kuundwa kwa vikosi hivyo kutasaidia kupunguza gharama kubwa ambayo serikali huingia kila mwaka kwa ajili ya kuwalipa wananchi waliokumbwa na mikasa ya wanyamapori.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Vyama vya siasa vifuate ushauri wa Samia ilani za 2020

**SUALA** la usawa wa kijinsia duniani, ni ajenda kubwa kwa sasa, huku kwa Tanzania wanawake wakipigania asilimia 50 kwa 50 katika vyombo vya maamuzi kati ya wanawake na wanaume.

Hitaji hilo linatokana na nchi yetu kuridhia mkataba wa wa Maputo wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (Sadc), ambao pamoja na mambo mengine, unataka nafasi za uongozi wa kuchaguliwa na kuteuliwa kugawanwa sawa kati ya wanaume na wanawake.

Hata hivyo, kwa kiasi fulani Tanzania ilianza kutekeleza suala la kuongeza nafasi za wanawake katika vyombo vya maamuzi baada ya Mkutano wa Dinua wa Wanawake wa mwaka 1995 uliofanyika Beijing, China, ambapo baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 1995, wanawake walianza kupewa nafasi hizo kwa asilimia 20.

Baadaye mwaka 2005 idadi iliongezeka kufikia asilimia 30 kabla ya Mkataba wa Maputo kuelekeza nafasi hizo ziwe asilimia 50 kwa 50. Kwa hiyo alichokisema jana

Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, kuvitaka vyama vya siasa kuhakikisha vinaweka ajenda hiyo kwenye ulani zao za uchaguzi mkuu wa 2020, ni mwendelezo wa kuhakikisha kwamba idadi ya wanawake inaongezeka katika vyombo vya kufanya maamuzi ili yawe na manufaa kwa jamii nzima.

Samia alitoa, kauli hiyo aliitoa jijini Dodoma alipokuwa akizindua Mtandao wa Viongozi Wanawake wa Afrika tawi la Tanzania (AWLN Tanzania) unaoratibiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linalojihusika na usawa wa jinsia na uwezeshaji wa mwanamke (UN Women).

Alisema wanawake waingize ajenda hiyo kwenye ilani za vyama vya siasa ambazo zitatumika kwenye uchaguzi huo.

Pia, Makamu wa Rais aliwataka wanawake kujitokeza kwa wingi na kushiriki kikamilifu katika kugombea nafasi za uongozi katika nyanja mbalimbali ikiwamo siasa, biashara, huduma za umma au asasi za kiraia, huku akieleza kuwa nchi nyingi duniani bado usawa wa kijinsia haujafikiwa katika nyanja nyingi ikiwamo uongozi.

Ushauri wa Samia utakuwa ni changamoto kwa vyama vyetu vya siasa, ambavyo bila shaka vitakuwa katika maandalizi ya ilani zao za uchaguzi unaotarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwaka huu.

Litakuwa jambo la ajabu kama kuna chama cha siasa ambacho kitatoa ilani ambayo haina ajenda ya kuongeza nafasi za wanawake. Hivyo basi, tunaamini kuwa ushauri wa Samia utavikumbusha vyama ambavyo vilikuwa vimelisahau suala hilo muhimu.

Ikumbukwe kwamba vyama vya siasa ndilo chimbuko la wanawake katika uongozi wa kisiasa. Tunalisema hili kwa kuwa katika nchi yetu sheria ya uchaguzi inazuia raia kugombea nafasi yoyote ya uongozi wa kuchaguliwa bila kupitia chama cha siasa.

Kutokana na hali hiyo, vyama vya siasa ndivyo vinavyofanya uteuzi wa wagombea wa nafasi zote kuanzia serikali za mitaa, udiwani, ubunge na urais. Pia nafasi maalum ukiwamo udiwani na ubunge wa viti maalum wahusika huteuliwa na vyama vya siasa.

Kwa lugha nyingine tunaweza kusema kuwa vyama vya siasa ni tanuru la kuwapima wanawake viongozi, hivyo tunaamini kuwa kama vitatekeleza jukumu hilo kwa haki, bila shaka nafasi za wanawake zitaongezeka, zikiwamo za uongozi ndani ya vyama vyenyewe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Inakuwaje tunagombea urembo bandia unaokaribisha saratani?

Na Sabato Kasika

**KATIKA** muundo wa afya ya mwanadamu, ngozi ni kiungo kimojawapo muhimu.

Kama ilivyo pande nyingine za mwili wa binadamu, hata wanyama ngozi inaundwa na seli zinazozaliwa, kukua na kufa kila kukicha, katika mfumo wa asili unaojiendesha.

Nini vinaathiri chembehai? Hivyo vinatajwa kuwa msongo wa mawazo, jua kali, ukosefu wa mlo mzuri, kutokunywa maji ya kutosha, kujichubua, umri mkubwa, uchafu, vipodozi visivyo salama, magonjwa, maambukizi ya maradhi na kujeruhiwa.

Inaelezwa vitu hivyo vikitokea kwa kiasi kidogo hudhoofisha seli za binadamu na vikiondolewa, hujijenga upya kurudia hali ya kawaida.

Inapotokea kwa kiasi kikubwa au kuendelea kuwapo kwa muda mrefu hali hiyo, inadhoofisha zaidi seli na kuziua kabisa, hata kuharibu ngozi ya eneo hilo. Nadharia rasmi na tafiti zinazoendelea zinasema hivyo. Kumekuwapo mtindo na tabia ya kuingiza nchini vipodozi vyenye kemikali hatari, licha ya serikali kupiga marufuku kutokana na madhara yake kwa watumiaji.

Imekuwa kawaida kusikia serikali imeteketekeza vipodozi feki kwenye mkoa fulani, lakini bado vinaendelea kuingizwa nchini, licha ya madhara yake kujulikana na kutangazwa zaidi ya mara moja.

Wapo Watanzania wanaoingiza vipodozi hivyo kwa njia za panya na kuziuza katika maduka ya dawa za binadamu na wengine katika njia nyinyine za kinyemela mitaani, bila ya kujali madhara yaliyopo.

Ni kilio kisichokoma. Nadhani umefika wakati wale wanaopenda 'kujichubua' wajali afya zao kwanza, kuliko urembo huo wenye madhara. Waachane na uthubutu wa kutumia vipodozi feki vilivyopigwa marufuku, kuingizwa nchini.

Inadaiwa, wapo wanaopenda urembo wakiwa wamefika hatua ya kujitengenezea mchanganyiko wa tindikali za maji ya betri ya gari, dawa za meno na sabuni ya unga, ili kupata mkorogo maalum wa kujipaka.

Ni hatari wanayoiendekeza. Hivyo, jambo la msingi ni kuzingatia matumizi ya vipodozi vilivyothibitisha kwamba havina madhara, kuliko kung'ang'ania urembo unaoishia hatarini.

Katika harakati zinazofananishwa na hayo, kuna anayedaiwa kuwa mdau wa nyendo hizo, alikamatwa mkoani Pwani, akiangukia tuhuma za kusafirisha shehena za vipodozi feki.

Kwa tukio hilo na mengine ya aina hiyo tunayosikia kutoka maeneo mbalimbali nchini, ni ishara kwamba vipodozi feki bado vina wateja wengi, ambao huenda bado hawajatambua madhara yake au elimu sahihi haijatua vichwani mwao.

Kimsingi, vipodozi feki ni muuaji aliyejificha kwenye urembo, ambaye jamii itakapomwelewa vyema na kumwepuka, itakuwa njia mojawapo ya ushindi.

Tunapozungmzia njia ya ushindi, ujumbe unasimama katika dhana kwamba, umuhimu wa kuzingatia ushauri na elimu inayotolewa kuhusu hatari ya matumizi ya kemikali hizo.

Siyo vyema kuendelea kukumbatia dhana potofu ya kwamba 'kuwa mweupe ni urembo.' Hilo ndilo limewafanya baadhi ya wapenda urembo, kutumia vipodozi vyenye madhara kwa kipaumbele cha urembo, bila ya kujali afya zao?

Ikumbukwe, madhara ya awali ya vipodozi hivyo huonekana kwa mtumiaji kwa kubabuka ngozi, kuwa na mabaka meusi au ngozi kuwa nyekundu, lakini utakuta bado anaendelea kutumia pasipo kushtuka kengele ya umma inayojaribu kuiwamamsha.

Watumiaji urembo wanapaswa kutambua, serikali inapopiga marufuku matumizi ya vitu hivyo, inavitambua kitaalamu kuwa vina madhara kwa binadamu.

Ni bahati nzuri, elimu sahihi inatolewa kwa umma wananchi wake na tena bahati nzuri elimu inatolewa kwa umma, ambao baadhi yao ni wazito kunasa somo.

Ni wazi, elimu na ushauri unahitajika zaidi kuwatoa katika mazingira hayo ambayo ni hatari kwa afya zao, hata wakatambua 'weupe wa bandia' siyo urembo bali madhara kiafya.

Mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha Georgia, Atlanta nchini Marekani, Kelly Lewis, alisema wanawake wengi nchini wanajihatarisha kuugua saratani kupitia vipodozi, pia kukaribisha madhara kwa watoto kuwa na mtindio wa ubongo.

## BARUA & MJADALA

# *Mafia tunahitaji maendeleo*

**Mhariri**

*SISI wakazi wa Kisiwa cha Mafia, tuna kilio chetu kuhusiana na maendeleo duni tulio nayo hapa kwetu.*

*Kwa kutumia gazeti letu pendwa la Nipashe, rasmi tunakujulisha kuwa Mafia ikilinganishwa na kwingineko mkoa wa Pwani, hapa kwetu tuna dhiki.*

*Hivyo, sisi wananchi tunatoa kilio chetu kwa viongozi wetu madiwani, mbunge na wengineo wa kiserikali, chini ya mkuu wa wilaya, waongoze kutukwamua kutoka umasikini usiotupa haiba nzuri hata kidogo kitaifa na maisha yetu ya kila siku.*

*Ni hata katika ukusayaji wa mapato kitaifa, hatupo katika hatua ya kupendeza hata kidogo. Sasa kama ndio hivyo, hatua ya mafanikio yetu inafikia wapi?*

*Vilevile tutoe wito kwa mawaziri wetu mabao ni wadau wakubwa katika maendeleo yetu, akiwemo mchapakazi Mhesimiwa Selemani Jafo, ajaribu kuwa karibu sana nasi kusukuma maendeleo yetu kufuatilia mahali ambako Mafia inakwama na nama gani tunaweza kusonga zaidi.*

*Ni hata tukirejea, Mafia ni kisiwa cha kihistoria na vigumu sana kuzungumzia ukanda wa Pwani, halafu usitutaje.*

*Hata mkoa Pwani, unaweza kufika hatua ukabuni mkakati wake kimkoa kuhusu namna ya kuikwamua wilaya yake ya Mafia ikapiga hatua ya kusonga mbele, kama zinavyonyanyuka kama vile Bagamoyo, Mkuranga, Rufiji na wageni Kibiti, Bado naamini inawezekana hilo kwa Mafia.*

*Viongozi wetu wa kuchaguliwa chagamkeni na muwajibike wananchi tufurahi, maana msimu wa kuhukumu ni mwisho wa mwaka.*

**Juma Ally,**
**Kilindoni, Mafia**

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Hakuna wa kujiweka kando katika hili la kujenga zahanati




**Na Lazaro Mateko**

**HUDUMA** ya afya kwa wote, ni lengo kuu la Shirika la Afya Duniani (WHO), kwamba hatua muhimu ya kufanikisha ni kuhakikisha kila mtu anapata huduma anayohitaji, pale pale anakoishi kwenye jamii yake.

WHO inasema, licha ya kuwepo hatua iliyopigwa katika baadhi ya nchi duniani, pia kuna changamoto kadhaa zinazotokana na umaskini na kusababisha baadhi ya jamii kutopata huduma hiyo.

Lengo ni kuhakikisha kila mtu anapata huduma ya afya, bado mamilioni ya watu wanalazimika kuchagua kati ya huduma ya afya na mlo, mavazi au hata makazi.

Katika kauli yake kwenye Maadhimisho ya Siku ya Afya Duniani, ni haki na wala si upendeleo, kwamba watu wote wanastahili huduma ya afya pale wanapoihitaji.

Kwa kutambua umuhimu huo, serikali nchini ilikuja na mkakati wa kujenga zahanati kila kijiji na pia kujenga kituo cha afya kila kata, kwa lengo la kusogeza huduma za afya karibu na wananchi.

Hiyo ni chini ya mwamvuli wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) nchini, iliyoanza kutumika rasmi mwaka 2008, baada kupitishwa mwaka 2007.

Mkakati huo umekuja kutokana na ukweli kwamba, ukosefu wa huduma ya afya vijijini, ni miongoni mwa changamoto zinazovikabili vijiji mbalimbali nchini na asilimia kubwa ya Watanzania wanaishi huko.

Ukosefu huo wa huduma ya afya unawalazimu kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo kwenye maeneo mengine, hali ambayo ni changamoto inayohitaji kutafutiwa ufumbuzi. Ni kutokana na uamuzi huo, ujenzi wa zahanati na vituo vya afya unaendelea kwa kasi kwenye maeneo mbalimbali nchini, ili kuhakikisha huduma za afya zinasogezwa karibu na wananchi.

Hiyo ni sera ya serikali kwamba, kila kijiji kiwe na zahanati na kila kata iwe na kituo cha afya na kila wilaya iwe na hospitali na mkoa unakuwa na hospitali ya rufani. Hivyo, kinachotakiwa ni wananchi katika maeneo yao kuunga mkono sera hiyo.

Hatua hiyo inaweza kusaidia kuharakisha ujenzi huo unaondelea katika vijiji na kata mbalimbali nchini. Bila ya kufanya hivyo, inaweza ikasababisha ucheleweshaji unaosogeza huduma hiyo kwenye maeneo yao.

Kila mmoja anapaswa kutambua kuwa, huduma za afya zikiwa karibu zinaweza kumfanya mgonjwa akapata matibabu haraka, kupunguza muda wa kusafiri umbali mrefu na kuokoa gharama za ziada.

Vilevile, kuna wakati mwingine siyo lazima serikali ianzishe ujenzi wa zanahati, bali wananchi wenyewe wanaweza kujenga, kisha wakaiomba iwaunge mkono katika juhudi zao hizo.

Wapo baadhi ya wananchi walishaonyesha mfano huo kwa kujitolea kujenga zahanati yao na kufikia hatua ya kuomba kuungwa mkono katika juhudi hizo, kukamilisha ujenzi.

Kwa hiyo, wakati ujenzi ukiendelea kwenye vijiji na miji mbalimbali nchini, jambo la msingi ni wananchi kushiriki kikamilifu na kwa kutambua kuwa ni zahanati na vituo vya afya ni mali ya umma na umma wenyewe ni wao.

Ushiriki wa wananchi katika ujenzi unaweza unachangia kukamilisha lengo la serikali la kutaka kila kijiji ya kitongoji kuwa na zahanati, kila kata kuwa na kituo cha afya na wilaya kuwa na hospitali.

Utaratibu wa ushirikishaji wa wananchi kwenye mambo ya maendeleo, ni jambo muhimu na unasaidia kupunguza baadhi ya gharama binafsi na kitaifa, kutokana na ukweli hao ndio nguvukazi kwenye ujenzi wa nchi. Njia iliyopo ni kwamba, wananchi wanaanzisha ujenzi wa zahanati na kisha wanaomba serikali iwaunge mkono pale wanapoishiwa nguvu au wao kuunga mkono kile kilichoanzishwa na serikali, kwa kizingatia taratibu maalum.

Suala la afya limekuwa likisisitizwa na Rais Dk. John Magufuli, kwamba sekta ya afya inatakiwa kuimarishwa ikiwa ni maandalizi ya kuelekea kuwa nchi yenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Hiyo maana yake ni kwamba, kuna haja ya kuhakikisha kila Mtanzania anakuwa na afya bora, itakayomuwezesha kutekeleza majukumu yake kikamilifu katika jamii inayomzunguka.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed





Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akizungumza katika uzinduzi wa Mtandao wa Viongozi Wanawake Afrika, Tawi la Tanzania, jijini Dodoma jana, ambapo kauli mbiu ya Mtandao huo ni Wananwake na Uongozi Twende Pamoja Wakati ni huu. **PICHA: OMR**

# Samia ataka ajenda ya 50/50 ilani za vyama

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amesema katika mchakato wa uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwaka huu, wanawake wahakikishe ajenda ya 50 kwa 50 inaingizwa kwenye ilani za vyama vya siasa.

Kauli hiyo aliitoa jana jijini hapa, alipokuwa akizindua Mtandao wa Viongozi Wanawake wa Afrika tawi la Tanzania (AWLN Tanzania) unaoratibiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linalojihusika na usawa wa jinsia na uwezeshaji wa mwanamke (UN Women).

Alisema wanawake waingize ajenda hiyo kwenye ilani za vyama vya siasa ambazo zitatumika kwenye uchaguzi huo.

"Ngoja niwaibie siri, hivi sasa vyama vya siasa vipo katika mchakato wa kutengeneza ilani za uchaguzi... ni vyema wanawake tukasimama kidete katika kuhakikisha vyama vinaingiza agenda ya 50 kwa 50 katika ilani zao na hata kama sio kwenye maoneo yote basi baadhi ya maeneo 50 kwa 50 ionekane," alisema.

Pia makamu huyo aliwataka wanawake kujitokeza kwa wingi na kushiriki kikamilifu katika kugombea nafasi za uongozi katika nyanja mbalimbali ikiwamo siasa, biashara, huduma za umma au asasi za kiraia.

Aidha, alisema nchi nyingi duniani bado usawa wa kijinsia haujafikiwa katika nyanja nyingi ikiwamo uongozi.

"Hali hii inaigusa nchi yetu, ingawa kwa kiasi kikubwa tunafanya vizuri tukilinganishwa na nchi nyingine barani Afrika, tuna wabunge wanawake 126 kati ya 393 sawa na asilimia 36.7, huku Baraza la Wawakilishi Zanzibar ni asilimia 38, kiwango hichi ni juu ya uwiano uliowekwa na nchi za SADC cha angalau asilimia 30," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa upande wa Mahakama, idadi ya majaji wanawake kwa Mahakama Kuu ni asilimia 30, Mahakama ya Rufani ni asilimia 38, Baraza la Mawaziri Wanawake ni asilimia 18, wakati Naibu Mawaziri ni asilimia 33.

"Kwa mara ya kwanza nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeshikwa na mwanamke. Kwa takwimu hizo utaona bado hatujaweza kufikia usawa wa kijinsia kwa kiwango kikubwa sana," alisema.

Alisema takwimu za idadi ya watu nchini zinaonesha wanawake ni wengi zaidi ya wanaume.

"Naamini kama wanawake tukiamua na tukishirikiana vizuri na kuaminiana basi tunaweza kupunguza wigo wa uwiano wa kijinsia kwa kiasi kikubwa," alisema.

Kadhalika, alisema tafiti zinaonyesha ongezeko la idadi ya viongozi wanawake wa kisiasa limesababisha kuboreshwa kwa sera, sharia pamoja na bajeti.

"Kadhalika, imebainika kuwa uwapo wa wanawake zaidi katika usimamizi wa mashirika katika sekta binafsi umethibitika kusaidia kukuza faida za biashara kutokana na ujuzi, ufanisi, uaminifu na ustadi wa kipekee," alisema.

Aliutaka mtandao huo kuwawezesha wasichana kujifunza na kuhusudu kufanya kazi kwa bidii na kuleta mabadiliko chanya kwenye maeneo yao.

Samia aliwaomba wanaume kuwa wavumilivu kwa wanawake viongozi kwa kuwa wapo kwenye orodha ya watu wanaowajali.

"Sisi ni wanawake, maisha yetu yamezungukwa na mambo mengi mwanamke, mama na kiongozi, ukweli ni kwamba hatuwezi kufanya yote wenyewe, hatuwezi kufanya haki na kuwajibika ipasavyo kwa kila anayetutegemea," alisema na kuongeza:

"Waathirika zaidi ni wanaume zetu, kuweni wapole na wavumilivu. Nayasema haya si kwasababu mimi ni mahiri sana ila waswahili wanasema 'Hakuna Kungwi mchafu."

Naye, Katibu Mkuu, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. John Jingu, alisema serikali imetekeleza baadhi ya mambo katika kumuwezesha mwanamke.

Mwakikishi maalumu wa Mwenyekiti wa Kamisheni ya Amani na Usalama kwa Wanawake ya Umoja wa Afrika, Bineta Diop, alitaka Mtandao huo kutumika kupeana uzoefu na kutatua changamoto za uongozi za mwanamke.

Akitoa salamu kutoka ubalozi wa Ujerumani nchini, Mkuu wa Ushirikiano Kikanda, Norzin Grigoleit-Dagyab, alisema Tanzania imepiga hatua katika suala la usawa wa kijinsia na kuwa kuanzishwa kwa mtandao huo ni jambo jema na kusisitiza kuwa ni imani yake kuwa mtandao huo utaleta mafanikio bora.

Naye Balozi wa Norway nchini, Elizabeth Jacobsen, alisema pamoja na nchi yake kuisaidia Tanzania katika masuala ya wanawake, ana imani kuanzishwa kwa Mtandao huo utakuwa ni sauti ya wanawake.

Balozi wa Sweden nchini, Anders Sjoberg, alisema suala la usawa wa kijinsia ni vita inayohitaji ushirikiano kuikabili na kuondoa vikwazo vya kufikia usawa wa kijinsia.

## Kigogo Chadema ajiuzulu uanachama

**Na Enock Charles**

ALIYEKUWA Katibu Mwenezi wa Baraza la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Edward Simbeye, amejivua uanachama wa chama hicho, akidai kutokukubaliana na baadhi ya mambo yanayoendelea ndani ya chama.

Amedai kuwa moja ya mambo asiyokubaliana nayo ni kuvunjwa kwa kanuni za chama hicho na kuongozwa kama kampuni ya mtu binafsi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Simbeye alidai chama hicho kimepoteza lengo la kuchukua dola na kutekeleza malengo ya watu binafsi kinyume cha kanuni na miongozo yake.

Alisema kitendo hicho ndicho kinachagiza viongozi na wanachama kuhama na kujiunga na vyama vingine, hasa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Chama changu Chadema kwa sasa kimepoteza malengo ya kushika dola na kimebaki kutekeleza maagizo ya mtu binafsi, kuna ubinafsi na umimi kwa sasa ndani ya Chadema," alidai.

Simbeye alidai kuondoka kwa aliyekuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Vicent Mashinji, kumesababishwa na uamuzi wa Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, kumweka msomi huyo nje ya majukumu yake ya kikatiba na kanuni za chama.

Alidai Mbowe aliunda Kamati Ndogo ya Kamati Kuu ya chama hicho na Kamati Ndogo ya Sekretarieti ambazo Katibu Mkuu ambaye ndiye mtendaji mkuu wa chama, hakuwa mjumbe.

"Mwenyekiti wa chama, Freeman Mbowe alikosea kwa Katibu Mkuu wake kwa kuunda kamati ambazo ziliendesha chama na ambazo Katibu Mkuu hakuwa mjumbe," alidai.

Aliendelea kudai kuwa hata kuondoka kwa mawaziri wakuu wastaafu; Edward Lowassa na Fredrick Sumaye ni matokeo ya udhaifu wa kiuongozi ndani ya chama, ubinafsi na ukosefu wa demokrasia na kukitaka chama hicho kuwaomba radhi viongozi hao kwa kile anachokiona wamedhalilishwa.



Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Tanzania Bara, Japhet Mangula, akikagua mkorosho, alipotembelea mradi mkubwa wa shamba la pamoja la korosho lenye zaidi ya ekari 12,000, eneo la Masagati, wilayani Manyoni, mkoani Singida juzi, akiwa katika ziara ya kikazi ya siku saba mkoani humo. **PICHA: JOHN MAPEPELE**

## Wazalishaji wahimizwa mafunzo kuboresha bidhaa

**Na Felix Andrew**

UONGOZI wilayani Kongwa mkoani Dodoma, umewataka wajasiriamali kuzingatia mafunzo yanayotolewa na serikali pamoja na taasisi zake yenye lengo la kuboresha bidhaa wanazozizalisha, kukuza mitaji yao na hatimaye kupata uhakika wa soko.

Kauli hiyo ilitolewa hivi karibuni na Katibu Tawala wa Wilaya ya Kongwa, Audiphace Mushi, akimwakilisha Mkuu wa Wilaya hiyo, Deogratius Ndenjembi, wakati akifungua mafunzo kwa wazalishaji wa mafuta ya alizeti na wauzaji wa bidhaa za chakula na dawa katika ukumbi wa Halmashauri ya Mji mdogo wa Kibaigwa, wilayani Kongwa.

Mushi alisema washiriki watumie fursa hii kuelewa masuala mbalimbali yanayofundishwa ili watakapomaliza wakawe mabalozi wazuri kwa wale ambao hawakupata fursa ya kushiriki katika mafunzo yenye lengo la kuwataka wazalishaji kufuata taratibu na sheria za nchi zilizopo.

"Serikali ya sasa inatutaka tufuate utaratibu ili kuepuka matatizo mbalimbali, mafunzo haya yawe ni chachu ili kuwafikia wengine," alisisitiza Mushi, na kuongeza kuwa wanapaswa kuwa wadadisi ili waweze kupata manufaa yatokanayo na mafunzo haya ili hatimaye waweze kuboresha bidhaa zao ziweze kupatiwa alama ya ubora na kuweza kumudu ushindani katika soko.

Vilevile, aliwasisitiza washiriki kuwa mabalozi kuhusu Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na mafunzo waliyopata kwa ujumla kwani ubora na viwango ni jambo lisilokwepeka katika dunia ya sasa. Alisema TBS imefanya uamuzi mzuri kuandaa mafunzo katika Halmashauri ya mji mdogo wa Kibaigwa kwani mji huu ndiyo kitovu cha wazalishaji wa mafuta ya alizeti na wauzaji wa bidhaa za chakula na vipodozi na ni mara ya kwanza kwa TBS kufanya mafunzo ya aina hii na shirika linatakiwa kufanya tathmini ya mafunzo kwa wadau waliopatiwa mafunzo.

# NHC yatakiwa kuongeza kasi ujenzi wa hospitali

**Na Munir Shemweta,** MUSOMA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amelitaka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), kuongeza kasi ya ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kwangwa wilayani Musoma mkoani Mara ili ikamilike kwa muda uliopangwa.

Hospitali hiyo ni ya ghorofa tano yenye sehemu tatu (Wing A, B na C) na inarajiwa kuanza kutoa huduma kwa baadhi ya idara mwezi ujao.

Dk. Mabula alitoa agizo hilo juzi mjini Musoma alipokagua maendeleo ya ujenzi wa jengo hilo unaofanywa na NHC akiwa katika ziara yake ya siku moja.

Alisema licha ya NHC kufanya vizuri katika ujenzi wa jengo la hospitali hiyo kulinganisha na makandarasi waliotangulia, inapaswa kuongeza kasi ili likamilike katika muda uliopangwa na kuanza kutoa huduma.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, Hospitali ya Kwangwa ambayo wameamua iitwe Mwalimu Nyerere Memorial Hospital, ina historia ndefu kwa kuwa pamoja na kuasisiwa na Rais wa Kwanza, Mwalimu Julius Nyerere, utekelezaji wake unakamilishwa na serikali ya awamu ya tano.

"Ni vyema NHC mkaongeza bidii katika ujenzi wa hospitali hii ili ikamilike kwa haraka kwa kuwa hospitali hii ina historia ndefu na Rais John Pombe Magufuli ameamua ujenzi huu ukamilike kwa kutoa Sh. bilioni 15," aliagiza.

Katika kuhakikisha ujenzi wa hospitali hiyo unakamilika kwa wakati, Naibu Waziri Mabula alimtaka Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Dk. Maulid Banyani, kusimamia kwa karibu maendeleo ya ujenzi huo sambamba na kupatiwa ratiba ya mpango wa ujenzi na maendeleo yake kila baada ya siku mbili kwa nia ya kufuatilia kwa karibu.

Mkurugenzi huyo alimhakikishia Dk. Mabula kuwa ujenzi wa hospitali hiyo utakamilika kwa wakati baada ya vikwazo kadhaa kikiwamo cha Mshauri Mwelekezi kupatiwa ufumbuzi.

Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, aliisifu NHC kwa kufanya mabadiliko makubwa ya utekelezaji wa mradi huo uliokuwa umekwama.

"Toka Shirika la Nyumba la Taifa lianze ujenzi wa hospitali hii mwezi Agosti mwaka jana, kuna mabadiliko makubwa ya kasi ya ujenzi na tunataka mjenge kwa wakati na viwango na Machi mwaka huu huduma ya mama na mtoto ianze kutolewa," aliagiza.

Kwa mujibu wa Mkuu huyo wa Mkoa, hospitali hiyo itatoa huduma kwa wananchi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa pamoja na nchi jirani sambamba na kutumika kama sehemu ya utalii kutokana na mazingira ya hospitali.

Ujenzi wa hospitali hiyo ulianza mwaka 1977, Rais Nyerere alipotoa wazo la kujengwa kwake, lakini umekuwa ukikwama kwa nyakati tofauti hadi Rais Magufuli alipotoa Sh. bilioni 15 ili ukamilike.

# RC ashtukia ulaji milioni 100/- za ujenzi wa choo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, ametoa siku tatu kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Wilaya ya Kahama, kufanya uchunguzi wa matumizi ya fedha za ujenzi wa choo kipya katika Shule ya Msingi Bukondamoyo na kuwasilisha taarifa hiyo ofisini kwake.

Telack alitoa agizo hilo juzi alipofanya ziara ya kushtukiza katika shule hiyo iliyoko Halmashauri ya Kahama Mji ili kuona maendeleo ya ujenzi wa choo na kubaini fedha zilizotolewa, zilitumika vibaya na kusababisha ujenzi kutokamilika kwa wakati.

Alisema Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Anderson Msumba, amechukua hatua za haraka kupeleka vyoo vya dharura (mobile toilets) katika shule hiyo licha ya serikali kutoa fedha zaidi ya Sh. milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa vyoo shuleni hapo lakini haujakamilika.

"Nilipata taarifa za upotoshaji katika mitandao ya kijamii zilizowekwa na watu wasiokuwa na nia nzuri na maendeleo ya shule hii... kuwa shule hii haina choo.

"Nimefika ili nijiridhishe, nimebaini kamati ya shule hii imetumia fedha za wananchi vibaya katika ujenzi wa choo kipya," Telack alisema.

Aliutaka uongozi wa Takukuru kuhakikisha unafanya uchunguzi wa kina ili kubaini ni nani aliyehusika katika matumizi ya fedha za ujenzi wa choo hicho na kuwataka watu wanaosambaza taarifa kwenye mitandao ya kijamii kuwa shule hiyo haina choo, kuacha mara moja kwa kuwa serikali tayari imeshachukua hatua.

Awali, akitoa taarifa ya ujenzi wa choo hicho, Diwani wa Viti Maalum Bukondamoyo, Scholastika Danford, alisema wananchi wa kata hiyo wamegoma kuendelea kuchangia ujenzi wa choo hicho kutokana na kamati ya shule kutokuwa wazi kwenye ujenzi na kushindwa kusoma taarifa za mapato na matumizi.

"Siyo kweli kwamba wananchi hawataki kuchangia maendeleo katika shule hii. Tatizo hapa hakuna uwazi, shimo pekee la choo hiki linadaiwa kutumia zaidi ya Sh. milioni mbili, jambo ambalo linawatia shaka wananchi kuendelea kuchangia ujenzi huu," alisema.

Alidai kuwa kamati ya shule hiyo imeshindwa kusimamia ipasavyo ujenzi wa choo hicho, huku ikitambua kwamba vyoo vilivyokuwapo awali vimebomoka na kuilazimu Halmashauri ya Mji kuingilia kati kwa kutoa fedha kwa ajili ya kujenga vyoo ili kuwawez-

# Wafanyabiashara mkoa wa Mara waipa tano serikali

**Na Mwandishi Wetu,** MUSOMA

WAFANYABIASHARA na wawekezaji mkoani Mara wameihakikishia serikali kuwa watazitumia fursa za biashara zilizopo mkoani humo kuwekeza na kujenga uchumi imara sambamba na kufanikisha azma ya serikali ya kufikia uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025.

Mwenyekiti wa TCCIA mkoa wa Mara, Boniphace Ndengo, amesema sekta binafsi kupitia mikutano ya wazi ya majadiliano kati ya serikali, wafanyabiashara na wawekezaji, changamoto nyingi ambazo zilikuwa kikwazo kwa ukuaji wa sekta za uwekezaji na biashara zinapatiwa ufumbuzi kwa pamoja kupitia mikutano.

Akizungumza kwa upande wa sekta binafsi kwenye mkutano wa majadiliano kati ya sekta ya umma, wawekezaji na wafanyabiashara wa Mkoa wa Mara ukilenga kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kukuza uwekezaji katika mkoa huo, Ndengo aliishukuru serikali kwa dhamira yake ya kuiimarisha sekta binafsi hapa nchini.

"Tunaimani kubwa na serikali ya awamu ya tano kwani maboresho ya mazingira ya biashara yanayofanywa yanatuhamisha na kutupa moyo wa kuendelea kufanya kuwekeza na biashara zaidi katika mkoa wetu," alisema Ndengo.

Alisema ushiriki wa mawaziri katika mkutano huo ni ishara serikali inawajali wafanyabiashara kwani hawakuwahi kuona mazingira hayo kipindi cha nyuma kwa serikali hasa ngazi ya mawaziri kukaa meza moja na wafanyabiashara kujadili changamoto zinazowakabili kwa pamoja. Mkuu wa Mkoa huo, Adam Malima, alisema mkutano ulikuwa ni fursa pekee kwa wafanyabiashara na wawekezaji kutoa kero zao ili serikali itolee majibu lengo likiwa ni kuhakikisha mazingira ya kufanya biashara mkoani Mara yanakuwa rafiki na wezeshi kwao kufanya shughuli zao.

"Mkutano huu ni uthibitisho tosha kuwa serikali ipo kazini katika kuboresha mazingira ya biashara nchini ili kufikia uchumi wa kati na viwanda, hivyo tutaendelea kutoa ushirikiano ili kufikia azma hiyo na kukuza maendeleo nchini," alisema Malima.

RC Malima alisema mkoa wake umejipanga kuhakikisha wananchi wanatumia fursa zilizopo kuanzisha biashara ili kuleta maendeleo katika mkoa.

Meneja wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) Kanda ya Ziwa, Pendo Gondwe, alisema watashirikiana na mkoa kuhakikisha vivutio vya uwekezaji vilivyopo vinatangazwa kupitia tovuti ya TIC ili kuhamasisha wawekezaji ndani na nje ya nchi kuja kuwekeza katika mkoa wa Mara.

Wadhamini wakuu wa mkutano huo walikuwa Benki ya NMB na NBC ambao kwa pamoja walipongeza mwitikio mkubwa wa wafanyabiashara na wawekezaji kwenye mkutano wa majadiliano na serikali yatakayoleta tija katika sekta ya uwekezaji na kukuza uchumi nchini.

Alimpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki, kwa hatua mbalimbali anazozichukua kurejesha imani ya uwekezaji na wafanyabiashara kwani zinalenga kufanikisha azma ya serikali ya awamu ya tano ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025.



Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye (kushoto), akipata maelezo kuhusu utengenezaji wa vichwa vipya vya treni kutoka kwa Meneja wa Mradi wa kampuni ya SMH RAIL ya Malaysia, Mhandisi Wenceslaus Kamugisha, alipofanya ziara katika karakana ya reli, mjini Morogoro. **PICHA: WUUM**

# Kadenge aridhishwa miradi barabara Ilemela

**Na Geofrey Kazaula**

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Josephat Kandege, amesema ameridhishwa na miradi ya barabara iliyotekelezwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura) katika Manispaa ya Ilemela, jijini Mwanza.

Aliyasema hayo wakati wa ziara yake ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo mkoani Mwanza na kuwa mafanikio yanayopatikana katika Manispaa hiyo hasa katika miradi ya barabara yanatokana na ushirikiano mkubwa uliopo kati ya wataalamu wa Tarura na watumishi wengine wa manispaa kwa kufanya kazi pamoja na kuwaletea maendeleo wananchi.

"Wote tumeshuhudia barabara hizi zilivyo kwenye kiwango, mafanikio haya yanatokana na umoja uliopo kwa watumishi wote wa Manispaa ya Ilemela pamoja na watumishi wa Tarura kwa kuwa wanafanya kazi kwa pamoja ili kuwaletea wananchi wetu maendeleo, kiujumla wanafanya vizuri," alisema Kandege.

Alisisitiza kuwa miundombinu ya barabara inapokamilika ilindwe kwa nguvu zote na kuwaagiza viongozi husika huhakikisha barabara hizo zinafanyiwa usafi mara kwa mara na kulinda miundombinu ya barabara hizo.

Naye Meneja wa Tarura Manispaa ya Ilemela, Mhandisi Clement Kihinga, alisema kuwa barabara hizo zilizotekelezwa chini ya mradi wa Tanzania Strategic Cities Project (TSP), zimekuwa na mafanikio makubwa ikiwamo kuinua uchumi wa wananchi na kuboresha kiwango cha maisha ya wananchi.

Alitoa wito kwa wananchi kuhakikisha wanailinda miundombinu ya barabara ili zidumu na ziendelee kuboresha maisha yao na kurahisisha suala la usafiri na usafirishaji katika Manispaa ya Ilemela.

"Serikali inatumia gharama kubwa sana kujenga barabara hizi hivyo nitoe wito kwa wananchi kuhakikisha kila mmoja wetu anashiriki kulinda miundombinu hii ya barabara," alisema mtaalamu huyo.

Mmoja wa wananchi wa Kiseke A Ilemela, Issa Shabani, alisema awali usafiri ulikuwa changamoto sana katika barabara yao kwa kuwa miundombinu ilikuwa mibovu, lakini baada ya barabara ya Kiseke Busweru, kukamilika maisha yamepanda kiuchumi.

"Sasa nafanya biashara yangu ya matunda hapa Busweru, nayabeba salama na hayaharibiki kwa kuwa barabara ni nzuri na hata kipato changu kimeongezeka hivyo naishukuru sana serikali kwa kujenga barabara hii," alisema Shabani.

## Aagiza maeneo uwekezaji yapangwe miji inayokua

**Na Munir Shemweta,** SIMIYU

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameziitaka halmashauri nchini kuanza kupanga maeneo ya uwekezaji katika sehemu ambazo miji inakua kwa kasi.

Dk. Mabula alitoa agizo hilo juzi katika mkutano wa mashauriano baina ya serikali na sekta binafsi kuhusiana na vikwazo vya uwekezaji katika Mkoa wa Simiyu.

Alisema kuna maeneo mengi nchini ambayo miji inaendelea kwa kasi, hivyo halmashauri kupitia wakurugenzi wake, zinapaswa kuhakikisha zinatenga maeneo ya uwekezaji kwa lengo la kumwezesha mwekezaji kutopata tabu.

"Ni vizuri katika kipindi hiki ambacho baadhi ya miji inakua kwa kasi, halmashauri zikatenga maeneo ya uwekezaji na kuyahaulisha kwa lengo la kuwarahisishia wawekezaji watakapokuja kuwekeza katika halmashauri husika," aliagiza.

Naibu Waziri Mabula pia aliizitaka halmashauri kuhakikisha zinapanga maeneo yaliyoko pembezoni kwa kuainishwa matumizi yake kama vile kilimo, ufugaji na maeneo ya kuchezea kwa kutumia watendaji wa ngazi za chini badala ya kusubiri wataalamu wa mipango miji.

Alisema upangaji miji mapema kwa kutumia watendaji wa ngazi za chini, utasaidia wataalamu wa mipango miji watakapokuja baadaye kutopata shida katika kupanga maeneo hayo hasa katika ile miji inayokua kwa kasi kwa kuwa miji hiyo itakuwa imepangwa na kuainisha matumizi mbalimbali.

"Hawa watendaji wa chini wakipewa elimu, wataweza kuipanga miji yao kama ilivyokuwa wakati wa vijiji vya ujamaa maana sasa hivi mtu anaweza kujenga kiwanda katikati ya makazi ya watu," alisema.

Katika mkutano huo, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, alitoa ufafanuzi wa riba kubwa kwa taasisi za fedha na kubainisha kuwa serikali ya awamu ya tano imesikia kilio hicho na imekuwa ikisisitiza taasisi hizo kupunguza riba kufikia asilimia 11.

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Musa Sima, alisema lengo la serikali si kufungia biashara, bali kutafuta njia itakayowawezesha wawekezaji kufanya biashara katika mazingira mazuri na kubainisha kuwa mtendaji wa ofisi yake atakayekwamisha jitihada hizo, taarifa itolewe ili hatua zichukuliwe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elias Kwandikwa, alisema wizara yake inafanya jitihada kubwa kuunganisha mikoa katika masuala ya miundombinu sambamba na kushughulikia maeneo korofi ili wawekezaji wafanye kazi zao kwa urahisi.

# Waona fursa uhifadhi, utalii

**Na Cynthia Mwilolezi,** LONGIDO

WANANCHI wa vijiji 33 vya Tarafa za Engarenaibo, Longido na Kitombeini wilayani Longido, wameanza mchakato wa kuunda Hifadhi ya Jamii ya Wanyamapori (WMA), ili kushiriki katika uhifadhi, kupunguza migogoro ya ardhi na kujiingizia vipato kupitia utalii.

Akizungumza jana na Nipashe baada ya kikao cha vijiji hivyo, kujadili kuanzisha WMA, Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, alisema wazo la vijiji kuanzisha hifadhi hiyo limeibuliwa na wananchi wenyewe ili washiriki katika uhifadhi.

Mwaisumbe alisema wamekubaliana kuanzisha WMA na sasa wameanza mchakato wa vikao na baadaye watafikia makubaliano ya jina na kuanzisha ofisini zao kwa kuwa vijiji vyao vina wanyamapori wengi na vivutio vya utalii.

"Mchakato huo utahitimishwa na Mamlaka ya Wanyamapori (Tawa), ambayo ndiyo msimamizi mkuu wa hifadhi za jamii, mapori ya akiba na mapori tengefu nchini," alisema.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Gilai Lumbwa, Richard Mollel, alisema WMA pia itasaidia kuondoa mgogoro na wawekezaji katika kitalu cha uwindaji cha Lake Natron (East) ambacho kilikuwa kinamilikiwa na Kampuni ya Green Miles iliyoondolewa na serikali.

Alisema wanaona bora kuwa na WMA ili wakaribishe wawekezaji wazuri na wanaojali wananchi wa eneo husika kwa kuwa kwa muda mrefu wamekuwa na mwekezaji aliyeshindwa kukaa vizuri na vijiji na kusababisha migogoro.

"WMA itatuwezesha kuanzisha mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji vyetu na kutenga maeneo ya uhifadhi, malisho ya mifugo, makazi na maeneo ya shughuli za kijamii," alifafanua.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, mkoani Manyara, Hudson Kamoga (kulia), akikagua ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri hiyo, katika Kata ya Dongobesh juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# RC Gambo asaka dawa tatizo ajira

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, ameitaka Benki ya Standard Chartered, kuwekeza zaidi katika sekta ya viwanda ili kuondoa tatizo la uhaba wa ajira kwa vijana nchini.

Pia, ameishauri benki hiyo kuangalia jinsi ya kuwakwamua kiuchumi wajasiriamali wadogo, kwa kubuni shughuli zitakazowawezesha kukuza mitaji yao sanjari na kurejesha mikopo.

Gambo aliyasema hayo jana jijini hapa, alipozungumza na ujumbe wa benki hiyo ulioongozwa na Mkurugenzi wake, Sanjay Rughani, kuhusiana na masuala ya kifedha na huduma wanazotoa.

"Naamini endapo benki hii ikiwekeza katika viwanda, vijana wengi watapata ajira. Mkoa wa Arusha umetenga zaidi ya ekari 4,000 eneo la Nakula wilayani Arumeru kwa ajili ya uwekezaji, hivyo vyema mkatumia fursa hii kupata eneo hapo," alisema. Aliongeza kuwa kwa sasa tayari Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) na Shirika la Reli Tanzania (TRC) wamewekeza katika eneo hilo na ifikapo Aprili mwaka huu, safari za treni zitaanza mkoani Arusha.

"Naipongeza benki hii kwa kuangalia fursa za kuinua uchumi sambamba na kushirikiana na serikali katika miradi mikubwa kama ule wa ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR, hivyo wekezeni zaidi katika viwanda, ili kuondoa tatizo la ajira kwa vijana," alisema.

Kiongozi huyo wa mkoa alisema wanajivunia zaidi utalii na kuiomba benki hiyo kufanya utafiti zaidi ili kubaini vikwazo vilivyopo katika utoaji wa huduma kwa wateja, ili kuvutia watalii wanaofika nchini.

Aliwaomba watoe mikopo kwa wajasiriamali wadogo, ili wajikwamue kimaisha kwa kuanzisha shughuli zao za kujiingizia kipato.

Mkurugenzi wa benki hiyo, Sanjay, alisema benki itaendelea kushirikiana na serikali na wadau mbalimbali ili kuboresha huduma zake sambamba na kuangalia vipaumbele katika kuwezesha vijana kupata ajira. Alisema benki hiyo ni moja ya benki zinazotoa huduma mbalimbali za kibenki mkoani Arusha, hivyo atalifanyia kazi suala la utoaji mikopo kwa wajasiriamali wadogo, ili kuwanyanyua kiuchumi.

## DC awaonya viongozi wachochea migogoro

**Na Mwandishi Wetu,** MBULU

MKUU wa Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, Chelestino Mofuga, ameongoza kamati ya ulinzi na usalama kutembea kilomita 14 kwenye mpaka wa Kata za Endahagichan na Silaloda, ili kuzuia mapigano ya kugombea mpaka yaliyotaka kutokea.

Wananchi wa Kata ya Silaloda walibeba silaha za jadi na kwenda mpakani, ili kuhamisha mpaka wa serikali uliowekwa kwa ukuta, wakitaka waweke mpaka wao wenyewe.

Mofuga, akizungumza mgogoro huo, alikemea vikali baadhi ya viongozi walioshawishi wananchi juu ya mgogoro huo na kuchochea uvunjifu wa amani.

Alisema viongozi wote wanapaswa kuzingatia viapo vya maadili na uadilifu wa kulinda rasilimali za nchi na kulinda amani na utulivu.

Alitoa onyo kwa mtu yeyote atakayerudia kufanya hivyo kuwa atachukuliwa hatua kali kwakuwa uvunjifu wa amani si jambo zuri na halikubaliki.

"Wote waliohusika kwenye tukio hilo mnapaswa kufika ofisini kwangu kesho saa mbili asubuhi, bila kukosa," Mofuga aliagiza.

Aliwataka viongozi kujenga tabia ya kuandaa vikao na kuzungumzia matatizo yaliyoko kwenye maeneo yao badala ya kukimbilia kwa mkuu wa wilaya kupeleka malalamiko ya migogoro yao ambayo wanao uwezo wa kuitatua wenyewe kwa kushirikiana na viongozi wa kata na vijiji.

"Pia, waatalamu wa ardhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, nawaagiza kufika hapa ili wabaini mpaka kati ya kata hizi mbili zenye mgogoro wa mpaka na kuwakabidhi wananchi kusimamia," alisema.



# Kampeni kutokomeza ukame Same yaja

**Na Godfrey Mushi,** SAME

SERIKALI imetangaza Machi mosi mwaka huu itazindua rasmi kampeni yake ya kutokomeza ukame katika Wilaya ya Same.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Rosemary Senyamule, amesema awamu ya pili ya kampeni hiyo itahusisha upandaji wa miti katika maeneo oevu na katika maeneo ambayo hayana miti kabisa.

"Kampeni yetu ya kutokomeza ukame ndiyo ambayo itaokoa hali iliyopo Same kwa sasa. Tumemuita Balozi wa Utalii, Nangasu Warema, ambaye Wakala wa Misitu Tanzania atatoa mwongozo wa nini kitafanyika siku chache zijazo," alisema.

Kampeni hiyo huenda ikatekelezwa kwa mafanikio, baada ya awamu ya kwanza kupanda miti umbali wa kilomita 90 kando kando ya barabara kuu ya Moshi/Arusha/Tanga.

Kwa mujibu wa Senyamule, nia ya serikali ni kubadili fikra za wananchi kuhusu mazingira hasa wanaopita katika barabara hiyo kudhani mji huo hauwezi kubadili taswira yake kutokana na ukame. "Kampeni hii inalenga kuhakikisha tunabadilisha mtazamo wao na wapitaji wa njia hiyo kuwa Wilaya ya Same ni kame," alisema Senyamule.

Zaidi ya watu 11,000 wanapita njia hiyo kwa siku.

Upandaji miti huo unaunganishwa na mpango mkakati wa mazingira wa wilaya na maagizo ya Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan aliyotoa Oktoba, 2018 alipofanya ziara wilayani humo.

Katika taarifa yake, Senyamule alisema wananchi wafurahia mpango huo na kutoa ushirikiano mkubwa wa kuchimba mashimo 32,000 kwa kujitolea na sasa wanapanda miti hiyo iliyotolewa na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS).

Senyamule ameeleza zaidi kuwa: "kazi kubwa iliyopo mbele yetu ni kuhakikisha miti hiyo inakuwa haijalishi ukame, mchwa wala mifugo. Tunataka kuondoa fikra kuwa Wilaya ya Same ni kame, tuanze kuona Same ya kijani."

# Kinapa, vijiji kujadili baionuai Mlima K'njaro




Mwongoza watalii wapanda mlima, Joseph Chadel (kushoto), akiwa na mtalii katika eneo la maporomoko makubwa ya maji ya Materuni katika Kijiji cha Materuni, Kata ya Uru Mashariki, wilayani Moshi Vijijini, juzi. PICHA: JAMES LANKA

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

HIFADHI ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (Kinapa), imeitisha kikao chake cha pamoja cha ujirani mwema na wenyeviti wa vijiji 44 vinavyopakana na hifadhi hiyo ili kujadili suala la ulinzi na uhifadhi wa baionuai ya Mlima Kilimanjaro.

Mhifadhi wa ikolojia na ujirani mwema wa hifadhi hiyo, Imani Kikoti, alisema jana kuwa mazungumzo kuhusu uhifadhi na ulinzi wa rasilimali zilizopo katika eneo hilo yaliwahusisha wenyeviti hao kwa siku moja.

"Jana tulikutana na wenyeviti wa serikali za vijiji kwenye majimbo ya Moshi Vijijini na Vunjo katika Wilaya ya Moshi na katika kikao hicho cha pamoja cha wenyeviti wa vijiji 44, tumezungumza masuala ya ujirani mwema kwa maeneo yote yanayozunguka Mlima Kilimanjaro katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi," alisema Kikoti.

Katika kikao hicho, Kinapa ilimwalika pia wakili wa kujitegemea, Emanuel Mlaki, kutoa elimu ya kisheria juu ya suala la utunzaji, uhifadhi na utumiaji sahihi wa mazingira.

Aidha, Kikoti alisema Kinapa iliwaita viongozi hao ili kuunganisha nguvu ya uhifadhi wa rasilimali asili na vita dhidi ya uharibifu wa mazingira ambao umegeuka tishio kwa ustawi wa jamii katika mkoa huo.

Alisema kwa kuwa hifadhi inagusa maisha ya watu ya kila siku, wameona ni vyema kukutana na viongozi hao ambao wakizungumza watu wanashindwa kubishana nao na wakisema wanaaminiwa na kusikilizwa.

"Ingawa tulishakutana na kamati 60 za uhifadhi wa mazingira na wadau wengine, tumewaita na nyie tuwashirikishe hili la kulinda hifadhi yetu isiharibiwe.

"Ushirikishwaji wa namna hii umekuwa kichocheo kikubwa katika kujenga uelewa wa pamoja baina ya wadau wa hifadhi na hivyo kuboresha ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa hifadhi zetu," alisema.

"Ukataji miti ovyo kwa ajili ya matumizi mbalimbali, mioto holela, kilimo, mifugo kupita kiasi, utupaji taka ovyo, ni baadhi ya mambo yanayochangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira.

"Suala la uhifadhi ni mtambuka linahusisha sekta mbalimbali, hivyo ni muhimu sisi sote kwa pamoja kuunganisha nguvu ili kuhakikisha kwamba uhifadhi unakuwa endelevu na unaoleta tija kwa wananchi kiuchumi na kijamii. Ni ukweli usiopongika kuwa uharibifu wa mazingira ni tishio kwa ustawi wa jamii katika mkoa wetu wa Kilimanjaro, taifa na dunia nzima."

Kwa mujibu wa Kikoti, Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ina bioanuai kama aina 2,500 za mimea, aina 140 za wanyama na aina za ndege 177.

"Vivutio vya urithi wa dunia ambayo tunatakiwa kuvilinda kwa hali na mali ni kama mimea adimu na isiyopatikana sehemu nyingine duniani, barafu ya kudumu karibu na Ikweta (300km), maporomoko ya maji kama Lauwo na Kinukamori Water Falls. Pia tunahifadhi kwa sababu kuna kasoko kuu ya mlima (crater) na uwanda wa shira," alieleza Kikoti.

# Hai walia kuibuka upya mafuriko

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

WAFANYABIASHARA na baadhi ya wakazi wa kijiji cha Kwa Sadala, wilayani Hai mkoani Kilimanjaro, wamelalamikia kuibuka upya kwa matukio ya wizi katika eneo hilo.

Kutokana na tatizo hilo, wafanyabiashara hao wamemwomba Mkuu wa Wilaya hiyo, Lengai Ole Sabaya, kuingilia kati na kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo.

Akizungumzia malalamiko hayo, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha kwa Sadala, Edmen Massawe, alisema tatizo hilo limeanza kuibuka katika baadhi ya maeneo na wanaolengwa zaidi ni wananchi wanaokwenda sokoni kutafuta mahitaji.

"Hili sasa ni tatizo hapa kwa Sadala, ndio maana tunamwomba mwenyekiti wa kamati ya ulinzi ya Wilaya yetu atusaidie kudhibiti hali hii.

"Vibaka wanapora watu vitu mbalimbali ikiwamo simu za mkononi na fedha, kwa watu wanaofika katika soko la Sadala kwa ajili ya kupata mahitaji."

Hata hivyo, baadhi ya wakazi wa kijiji hicho waliozungumza na Nipashe, walisema kwa sasa eneo hilo vibaka wameongezeka toauti na awali na kwamba kunahitajika jitihada za makusudi za kudhibiti matukio hayo.

Ahamidiwe Mushi, mkazi wa Machame na Amina Abdallah, mkazi wa Sadala, alidai kuwa hivi karibuni alikwenda sokoni hapo kwa ajili ya kujipatia mahitaji muhimu, lakini wakati akiwa amenunua baadhi ya vitu na kutakiwa kulipa fedha, alijikuta akikabwa na vibaka hao.

"Hawa vibaka wanafahamika na wakazi husika lakini watu wanaogopa kuwataja wakati wanawapora watu vitu vyao, kwa kuwa wanaweza kuwadhuru baadaye, muhimu ni kuwapo walinzi katika eneo la kituo cha kupandia magari na hata sokoni kwani ndiyo haswa maeneo yao," alisema Mushi.

Elvis Joseph Bomang'ombe, yeye alidai katika kituo cha daladala cha Kwa Sadala, alishangaa kuporwa simu tena mchana na vijana wawili na kukimbia.

"Hili soko la Sadala ni katika masoko makubwa katika mkoa huu na wafanya biashara wengi wanakuja kufanya biashara zao zikiwamo ndizi, viazi karoti, maharage na maparachichi na kusafirishwa kwenda kwenye masoko ya Arusha, Dar es Salaam na maeneo mengine nchini lakini hao vikaba ni tishia tunamwomba mkuu wa wilaya kutuwekea ulinzi tufanye biashara kwa amani," alisema.

ama

ALHAMISI FEBRUARI 27, 2020

AFYA NA MAZINGIRA





Ukurasa 20

**Ndoa jinsia moja ilivyoanzia kujificha zama hizo hadi uzazi**



Ukurasa 17

**Maboresho Hospitali Temeke yatokomeza vifo kujifungua**



Ukurasa 14

‘Mabonge’ wakerwa kukataliwa katika ndege



# KICHOCHO

# ‘Kinawawinda’ watoto wawapo majini, kukabili kinahitaji ‘misuli’

Ukurasa 18



Mama Huhana (kulia), akiwa na wanawe. **PICHA: MTANDAO.**

## ‘Mabonge’ wakerwa kukataliwa katika ndege

**Aucland,** New Zealand

KUKALIA viti daraja la kwanza katika ndege kurudi Aucland, New Zealand kulilenga kuwafurahisha Renell na Tere, baada ya kufanyiwa upasuaji wa kupunguza uzito jijini Bangkok, Thailand.

Dada hao wawili na mama yao, Huhana waliwashangaa wafanyakazi wa kampuni ya ndege waliowafuata na mkanda wa kipimo, walipowaambia wanene kupita kiasi, wasimudu kukalia viti vya fahari.

Ni miezi sita sasa, Mama Huhana (59) na wanawe wakieleza kwa uchungu: “Wafanyakazi walipiga kelele wakisema mara kwa mara na kusema ‘tumenenepa sana.’ Watu walitutazama tukipimwa katika eneo la kuingia ndani ya uwanja wa ndege.”

Kutojua lugha waliotumia, iliwafanya wasifahamu kila neno, lakini wafanyakazi walikataa kuwaruhusu kukalia viti, hata ikawalazimu kukalia viti vya kawaida.

Huhana anaapa hatosafiri tena kwa ndege hadi atakapopunguza uzito, kuzuia uchungu uliowakuta.

Kampuni za ndege zinadaiwa kuwa na kawaida ya kuongeza urefu wa mikanda ya viti kwa abiria wenye uzani mkubwa, lakini kampuni tajwa ilisema mikanda katika viti vyake ni ya kifahari, haiwezi kuongezwa urefu, hata ikawashangaza waliokerwa.

AFYA

# Wafugaji ni moto usiozimika katika vita ubakaji Manyara?

• Vijana, walevi watuhumiwa maarufu



Kundi la jamii ya wawindaji, kati yao wamo watoto. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

SIKU hizi katika maeneo mengi nchini, suala la kusikia matukio ya ubakaji watoto wa miaka hata wadogo zaidi si jambo geni masikioni. Hapo kuna swali la kujiuliza, jamii inakwama wapi kutokomeza ukatili huo, ambao haukuwapo zamani?

Katika sura ya pili, ni kwamba kuna wanajamii wamepokea vita hivyo kwa mikono miwili kushirikiana na mamlaka zinazohusika kudhibiti maovu hayo, kuhakikisha usalama wa watoto hao?

Wapo wanaosema, wazazi wanakumbatia utandawazi na ndio chanzo cha watoto kukosa ulinzi na usalama, hata wakaangukia kwenye kadhia ya kubakwa na kusababisha kushindwa kufikia ndoto zao kimaisha au kuzifikia, tayari wamekwishaumia kisaikolojia.

> “...lakini siku hizi ukichapa mtoto wa mtu, utaambiwa ‘haki za binadamu.’

**MZEE AELEZA**

Mzee Musa Rehani, ni mstaafu anayesema wazazi wa hivi siku hizi wanajiweka katika mtazamo wa kisasa zaidi, kuliko zama zilizopita na chanzo kikubwa ni kukumbatia mtazamo wa kisasa, kwa maana ya utandawazi, kuliko jamii ilikotoka mtoto alikuwa wa watu wote katika jamii.

“Mzee ambaye hata humfahamu, alikuwa anakukemea akikukuta unafanya ujinga, lakini siku hizi ukichapa mtoto wa mtu, utaambiwa ‘haki za binadamu’ na utaenda kushtakiwa polisi, watu wengi wanaacha,” anaeleza.

Anaendelea simulizi kuwa zamani, mtoto alitumwa na asiyemjua na aliweza kurudi nyumbani na kuwaeleza wazazi wake, waliopokea hilo kwa mikono miwili. Ni zao la malezi mema inayozaa maadili.

Mstaafu huyo anaiasa jamii kuacha tabia ya kuwakemea walimu na wazazi wanaowaadhibu watoto, kwa kile anachokiita ‘kisingizio cha kumlinda mtoto’ akisema ina mwelekeo wa kuzaa tabia chafu kwa mtoto huyo, wengine wakihofu kuwasaidia kuwalinda kisheria.

“Sisi nyumbani iwe sikukuu, huwezi kurudi nyumbani zaidi ya saa 12 jioni, kwa kuwa baada ya muda huo ni ‘majanga’ na nikwambie mwanangu, mimi nimewalea hivyo watoto wangu,” anasema na kuendeleza msimamo:

“Na mimi huwezi kunikuta nje ya nyumbani saa moja, labda iwepo dharura na hii inasaidia kuwapo ulinzi wa mtoto, asikumbane na watu wenye nia ovu.”

**MWANASHERIA**

Mratibu wa Kituo cha Wasaidizi wa Kisheria na Haki za Binadamu cha Babati (BAPACE), Issa Mnyaruge, anaiambia Nipashe, tatizo kubwa la wenye umri wa miaka minane na kushuka kubakwa, linatokana na wazazi kutingwa na shughuli, hali inayofanya uangalizi wa ziada kubaki kwa wanaowatunza nyumbani.

“Unakuta mzazi mwingine anauliza mtoto wake umeenda shule leo, basi? Kumbe mzazi hatengi muda wa kuzungumza na mtoto wake, ili mtoto aweze kumwambia aliyokutana nayo na mzazi aweze kuona namna ya kumsaidia,” anaeleza.

Mnyaruge anasema, mzazi anapokosa muda wa kuongea na mtoto, anawapa nafasi wenye nia mbaya kufanya mambo mabaya kwa mtoto, kama vile zawadi batili zikiwamo pipi, biskuti na kalamu, inayoishia ukatili kwake.

Msaidizi huyo wa kisheria, anasema wako katika hatua za kukosa habari za watoto majirani zao na wakishindwa kuwakemea watoto wanapokosea au kuona mazingira mtoto anakoelekea, si mahali salama.

“Jamii imefeli kabisa, maana zamani jirani aliogopwa kama baba, lakini sasa tuwaelimishe watoto haki zao ni zipi wazifahamu na watoto wakielimika, tutapata kizazi kizuri na wazazi au jirani. Wewe na tabia ya kuuliza watoto wanakwenda wapi ili waweze kuwasaidia,” anasisitiza.

Mtaalamu huyo anasema, ni mara nyingi watu wa karibu na watoto akitoa mifano mjomba, babu, binamu na ndio wanaofanya ukatili kwa kutumia nafasi waliyo nayo, wakijua hawawezi kuwagundua.

Kuhusu mamlaka zinazohusika, anazitetea kufanya kazi inavyotakiwa, huku akitoa mfano Polisi inavyofungua kesi mahakamani, ila mashahidi hawatoi ushirikiano.

Anatumia fursa hiyo kuishauri jamii, kwamba iwe tayari kwenda mahakamani kutoa ushahidi, ili waathirika wa ubakaji na ulawiti

AFYA

# Wafugaji ni moto usiozimika katika vita ubakaji Manyara?

wapate haki zao na siyo kukubali kumalizana kienyeji huku jamii ya kukubali kumalizana.

**WADAU WANENA**

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Manyara, Anna Obed, anasema kwa kipindi cha mwaka 2019, kuna jumla ya matukio 226 ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto kuhusu ubakaji na ulawiti, yaliripotiwa katika vituo vya kutolea huduma za afya mkoani Manyara na wahusika wanapatiwa huduma stahiki.

Aidha, kwa kipindi hicho watoto walio na umri chini ya miaka nane wako zaidi ya 40 waliobakwa na anasema m mbinu inayotumika kudhibiti ubakaji na ukatili huo, ni kuzitumia Kamati za Mkakati wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Watoto na Wanawake (Mtakuwa).

Mtaalamu huyo anasema, ni kamati inayoanzia ngazi ya kijiji, ambako wahusika ni watendaji kijiji, wasaidizi wa kisheria, wataalamu wa afya na wazee maarufu wao na jukumu la kuripoti matukio yanayotokea katika maeneo yao.

Obed anasema, Mtakuwa ilianzishwa katika mwaka wa 2017/2018 na inafika kikomo mwaka 2021/2022, mpango unaojipima na kusaidiwa kwa kiasi kikubwa.

Anasema, majukumu makubwa ya Mtakuwa ni kutoa elimu katika jamii na kuhakikisha ulinzi kwa ngazi za vijiji na mitaa, ili inapotokea ukatili, wanapaswa kuripoti lifanyiwe kazi suala hilo.

Kwa mujibu wa Obed, changamoto waliyo nayo ni ufinyu wa bajeti za kutekeleza mpango huo, unaolenga kuwalinda watoto na kudhibiti ukatili unaojitokeza katika jamii.

**DOLA YANENA**

Ofisa Ustawi wa Jamii katika Halmashauri ya Hanan'g, Martha Sulle, anasema kuanzia Oktoba mpaka Desemba, watoto wenye umri hadi miaka nane waliobakwa idadi yao ni 24 na waliolawitiwa wawili.

Sulle anasema kesi zilizofikishwa mahakamani kwa ubakaji ni ni tisa na ulawiti una kesi tatu, akitaja sababu zinazokwamisha kutolewa uamuzi, ni jamii inashindwa kutoa ushahidi kesi zinapofika mahakamani.

Martha analalamika kwamba, hali ya ulinzi na usalama kwa watoto bado siyo nzuri, kutokana na familia nyingi kutelekeza watoto wasiotunzwa vyema na wazazi au walezi, sababu kuu wazazi hao ni wafugaji na muda mrefu wanatumia kuhamisha mifugo kunakohatarisha watoto.

"Mfano, unakuta wazazi wa jamii ya kifugaji wanamtafuta mchungaji na wanapoenda kuhamisha mifugo, wanawaacha



Kiongozi wa kiserikali wilayani Mbulu mkoani Manyara, alipowatembelea wanafunzi wa Shule ya Msingi Harka. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> **Majukumu makubwa ya Mtakuwa ni kutoa elimu katika jamii na kuhakikisha ulinzi kwa ngazi za vijiji na mitaa, ili inapotokea ukatili, wanapaswa kuripoti lifanyiwe kazi suala hilo.**

watoto na wachungaji anambaka mtoto au kumlawiti," anasema Sulle na kuongeza "kingine kinasababisha ni unywaji pombe."

Ofisa Ustawi Jamii huyo anasema, rika kuu inayohusika zaidi na matendo hayo dhidi ya watoto ni vijana wenye umri wa miaka kati ya 17 hadi 40 na baadhi ya wazee, japo anawateta ni wachache, baadhi yao wsakiangikia katika kundi la kuhusika na ushirikina.

Sababu nyingine aliyoitaja ni baadhi ya familia kuwa na ugomvi, hivyo wengine kuamua kuwafanyia ukatili wa ubakaji watoto kama sehemu ya kuwakomoa mahasimu wao ili waumie zaidi.

Kwa mujibu wa Sulle, athari za kisaikolojia anazoweza kuzipata mtoto baada ya kubakwa ni katika hali ya woga, na, hata kuhofu kurudi kwao, kutokana na historia ya unyama waliofanyiwa.

Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, inatoa wajibu kwa serikali, wazazi, walezi na jamii kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vyote vya ukatili na ubaguzi, ingawaje suluhisho la kupatikana ulinzi limebaki kitendawili.

Mkuu wa Wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu, alipotafutwa na Nipashe, anakiri kuwapo matukio mengi ya ubakaji kwa watoto umri uliotajwa na kwamba alishamwagiza Mkuu wa Polisi wa Wilaya, kuwasaka wote wanaodhaniwa kuhusika na ukatili huo.

Waziri wa Afya, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alipozungumza bungeni mwaka juzi, alisema takwimu zilizotolewa na Jeshi la Polisi Dawati la Jinsia, mikoa ya kipolisi inayoongoza kwa ukatili kwa watoto na hasa ubakaji, ni Kinondoni, Temeke, Arusha, Tanga na Dodoma.

Utafiti uliofanywa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) mwaka 2017 kupitia vy-



Mfugaji wa umri mdogo akiwa kazini, mkoani Manyara.

ombo vya habari, magazeti na runinga, ulionyesha asilimia 85 ya matukio ya ukatili dhidi ya watoto wa shule za msingi ni kuanzia miaka saba, kukiwapo mkasa uliomhusu mtoto mwenye umri miaka mwili.

**WAZAZI WANAVYOSEMA**

Mkazi wa Babati, Imelda Lucas, anawaainisha wabakaji wengi ni vijana wasio na kazi, hukua akishauri mamlaka za serikali za mitaa, zitunge sheria ndogo za kuwabana wanaokunywa pombe na kuzurura ovyo saa za kazi wawajibishwe kisheria.

Amina Abdalla, anasema wazazi kushindwa kutoa kipaumbele kwa ulinzi na usalama wa mtoto, ndicho chanzo cha wengi kubakwa, huku akitoa mfano wa mkasa unaomhusu mzazi asiyejua anakocheza mwanawe, hata akiulizwa jibu lake ni 'mtoto analindwa na Mungu.'

Mama huyo anawahiji wazxaszi wenziwe kwa kauli kama wao ni wazazi, matarajio yao yanasimama wapi katika kutimiza wajibu wa kuilinda zawadi hiyo waliopewa na Mungu.

Yusuph Idrisa, anasema kinachosababisha ubakaji ni tamaa zisizokuwa na msingi zinazowatawala baadhi ya watu na hatimaye kusababisha watoto kuumia, pasipo kuwa na hatia.

Neema John, anasema chanzo cha ukatili mwingi ni kukosekana maadili ya kiimani, ambayo ingeweza kuwasaidia wakaepuka maadili hayo mabaya.

Patrick Elias, anaitaka serikali kutokuwafumbia macho watu wa namna hiyo kwa kuwa serikali haishindwi, inapoamua kushughulikia jambo, akitoa mithili ya vita kwa wanaohujumu uchumi wa nchi.

AFYA

# Hospitali Bugando sasa bingwa wa kukabili figo za Watanzania

• Daktari Bingwa: Kila siku tunawatibu 45 • Inazalisha gesi, majitiba ya wagonjwa wake • Kila kitu kwa elektroniki, makubwa 'kibao'

**Na Mary Geofrey, aliyekuwa Mwanza**

KUKITHIRI idadi ya wagonjwa wa figo katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando iliyoko jijini Mwanza, imejipanga zaidi kwa tiba ya figo, kuwa sehemu mojawapo ya kitaifa inakonusuru afya ya umma.

Ni juhudi ya kuongeza idadi ya mashine za kusafisha figo kutoka 10 hadi 23 katika kipindi cha miaka minne sasa, hapo ikimaanisha kuletwa ukombozi dhidi ya ugonjwa huo unaotajwa kuwasumbua wananchi wengi.

Sehemu sugu zaidi inatajwa ni katika tiba ya kupandikiza figo mpya na wa unaohusu mshituko unaowapata wajawazito wanaojifungua na waliopata ajali, ambao tiba yake ni kuisafisha.




Mandhari ya mapokezi ya wagonjwa wa dharura wa Hospitali Bugando. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

### KUTOKA MADAKTARI

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa hospitali hiyo, Dk. Bahati Wajanga, ananasema ni kampeni hiyo inayolenga kuangazia mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya afya katika maeneo mbalimbali nchini, akisema kuwapo mashine hizo kumesaidia kupunguza muda wa kusubiri huduma hiyo kwa wagonjwa.

Bingwa wa Magonjwa ya Figo, Dk. Ladius Rudovick, anasema kitengo hicho kilianzishwa mwaka 2016 na kwa sasa wanatoa huduma kwa wagonjwa kati ya 40 hadi 45 kwa siku.

Anasema awali walianza na chumba kimoja na sasa wana vyumba viwili na wagonjwa wanafika hospitali hapo kusafishwa figo kila siku kwa awamu tatu ambazo ni asubuhi, mchana na jioni.

Dk. Rudovick anasema, tiba yao inawafikia wenye tatizo sugu la figo, linalotokana na shinikizo la damu, sambambana kisukari na wenye tatizo la mshtuko wa figo ghafla.

Anaeleza, wagonjwa wenye mshituko wa figo, wanasafishwa ndani ya wiki mbili na kurejea katika hali yao ya kawaida na wale sugu tiba yao ni kupandikizwa figo mpya.

Kuhusu uwiano wa wagonjwa waliopo, anasema idadi kubwa ni wenye tatizo sugu, kulinganisha na wale wa ghafla ambao idadi ndogo na wanapona kwa muda mfupi.

Anasema hospitalini Bugando, kunatolewa huduma ya usafishaji figo kwa wagonjwa wenye maambukizi ya virusi vya homa ya ini na maambukizi ya ukimwi na wasio na maambukizi. Kwa mujibu wa daktari huyo, maambukizi ya ukimwi wanapewa huduma katika chumba chao maalum na mashine ambazo hazitumiwi na wagonjwa wasio na maambukizi.

Aidha, anasema matumizi ya dawa za miti shamba ni chanzo cha kuwapo magonjwa ya figo na matumizi ya muda mrefu ya dawa za maumivu kwa wazee.

> **Kwa mujibu wa upatikanaji dawa katika hospitali, ni asilimia 98 na uwapo wa kiwanda hicho umesaidia kutoa tiba bora kwa bei nafuu, ukizingatia uzalishaji dawa kadhaa ambazo hazipatikani sokoni.**

### MAJI TIBA

Dk. Wajanga anasema, mafanikio mengine waliyopata hospitalini ni kupanua kiwanda cha kuzalisha maji-tiba aina 17 tofauti na idara hiyo, ikizalisha wastani wa chupa 400 kwa siku, zinazoweza kukidhi asilimia 60 kwa mahitaji ya hospitali.

Anasema, faida wanazopata wananchi kutokana na kuwapo kwa kiwanda hicho, ni kuzalisha aina ya dawa zisizopatikana sokoni na kuzizalisha kwa bei nafuu, inapunguza gharama kwa wagonjwa.

Lingine analolitaja ni kwamba, wanakarabati kitengo cha uchanganyaji dawa na wamekigeuza kuwa cha kisasa na kuchanganya dawa zaidi ya aina 50, ambazo ni aina nadra kupatikana sokoni.

Anasema dawa hizo ni za kunywa na kupaka na ni mahsusi kwa watoto wenye magonjwa ya moyo, figo, ngozi. Vivyo hivyo, kuna zilizoandaliwa kwa watu wazima.

"Kwa mujibu wa upatikanaji dawa katika hospitali, ni asilimia 98 na uwapo wa kiwanda hicho umesaidia kutoa tiba bora kwa bei nafuu, ukizingatia uzalishaji dawa kadhaa ambazo hazipatikani sokoni," anasema Dk.Wajanga.

### UFUAJI HEWA

Dk. Wajanga anasema, wamefunga mtambo wa kufua hewa ya oksijeni unaowasaidia kutoa huduma bora kwa wagonjwa wahitaji na umepunguza gharama ndani ya hospitali, iliyokuwa ikinunua hewa ya oksijeni kutoka nje ya ofisi.



Mitambo ya Oksijeni ambayo mgonjwa anapata moja kwa moja, iliyounganishwa wodini

Mtaalamu huyo wa tiba anasema, kwa wastani hospitali hutumia mitungi kati ya 20 hadi 30, kila mmoja kwa siku na mtungi mmoja ukipatikana kwa bei ya Sh. 45,000. Maana yake ni kwamba bajeti kati ya Sh. 900,000 na Sh.1, 350,000.

Anasema, ni mafanikio yanayofikisha hatua ya kuzalisha mitungi 2,100 kwa mwezi na gharama za uzalishaji wao hospitalini, ni nusu ya bei kamili ya soko la mtungi.

Daktari Wajanga anasema, kupungua kwa gharama za uendeshaji kwa hospitali, kumefanya kiwango cha fedha kinachookolewa, kitumike kuboresha miundombinu kwa wananchi wanaopata huduma Bugando.

Anaeleza matarajio yaliyopo sasa, ni kwamba watapokea mashine kubwa ya uchunguzi aina ya MRI, kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, itakayosaidia kubaini vyema matatizo ya wagonjwa wa Bungando.

"Kwa sababu ugonjwa unapogundulika mapema katika hatua za awali, tiba huanzishwa mapema na kupunguza madhara au vifo kwa wagonjwa, hivyo uwapo wa mashine hii ya kwanza kwa Kanda ya Ziwa na Magharibi, utapunguza adha kwa wagonjwa kufuata huduma hizi mbali," anasema Dk. Wajanga.

### AJIVUNIA MAFANIKIO

Daktari huyo anaendelea kueleza kuwa, hospitali hiyo ilipokea mashine kwa ajili ya matibabu ya macho kutoka Wizara ya Afya na kwa sasa Idara ya Macho, imeimarika zaidi kwa kuwa na madaktari bingwa wanne wanaohudumia wagonjwa wengi kwa mara moja.

Kuhusu orodha, mwaka jana walihudumia jumla ya wagonjwa 12,000 wenye matatizo ya shinikizo la macho, kisukari na wanaohitaji miwani ya kusoma. Hadi mwezi Oktoba mwaka, waliwafanyia upasuaji jumla ya wagonjwa 900.

Pia, Dk. Wajanga anasema, wanatoa tiba ya kibingwa na kisasa kwa wananchi wenye matatizo ya kinywa na meno, kutoka na madaktari bingwa kwa kutumia mashine za kisasa.

Anasema, Bugando imekuwa hospitali ya pili nchini kutoa huduma kamili ya saratani, baada ya kusimika mitambo ya kisasa ana anafafanua: "Hiyo, imesaidia wananchi wa Kanda ya Ziwa na Magharibi kupata huduma bora, sehemu wanayoishi na kwa haraka."

Pia, anasema kupitia Wizara ya Afya kuna fedha Sh. bilioni 5.5 ilitolewa na serikali kwa ajili ya kujenga jengo la saratani na kwa kushirikiana na wafadhili ambao ni serikali ya India, Bugando imenunua mashine nne za mionzi.

Anazitolea ufafanuzi kwamba, katika mashine hizo, mbili ni za kupanga na kutoa matibabu ya mionzi ya nje, yenye thamani ya Sh. bilioni 3.1 na mashine mbili za kupangia na kutoa matibabu ya ndani, kwa thamani ya Sh. milioni 700.

Eneo linguine la mafanikio analolitaja ni kujengwa na kuwezesha kuwepo jumla ya vyumba 13 vya kisasa vya upasuaji, kutoka vitano vya awali.




Majitiba, iliyokwishatengenezwa Bugando tayari kwa matumizi, katika Kitengo cha Kuzalisha Majitiba katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Ziwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Kwa mujibu wa Dk. Wajanga, uwapo wa vyumba hivyo utasaidia kupunguza muda wa kusubiri upasuaji kwa wagonjwa na wakati huo huo, kutatolewa matibabu ya kibingwa kupitia mitambo ya kisasa.

Anasema, kuanzishwa kliniki za wagonjwa wa bima na mikataba ya huduma zilizozinduliwa na Rais Magufuli, Julai 15 mwaka jana, jambo analojivunia hivi sasa imevutia takribani wagonjwa 300 hadi 350 kupata huduma kwa siku za kazi.

Katika Idara ya Viungo, kunatajwa kuwapo mafanikio ya kutolewa huduma maalum, kwa njia ya kikundi kwa watoto wenye mahitaji maalum, wakiwamo wenye utindio wa ubongo.

Dk. Wajanga anasema, hospitali imefanya ukarabati wa upanuzi wa Idara ya Dharura na Majeruhi, kwa sasa ina uwezo wa kuhudumia wagonjwa 100 kwa mpigo, kutoka 50 iliyokuwapo awali na kwamba imekuwa msaada bora jamii yote kwa ujumla.

> **Kitengo hicho kilianzishwa mwaka 2016 na kwa sasa wanatoa huduma kwa wagonjwa kati ya 40 hadi 45 kwa siku.**

Ni maboresho hata katika mfumo wa huduma kuendeshwa sasa kielekroniki, wakihama kutoka utaratibu wa zamani wa kulipia hela dirishani na matumizi ya mafaili kila hatua, sasa ikiongeza uharakishaji na ubora wa huduma zenyewe.

• Taarifa hii nii kwa mujibu wa ziara maalum iliyoandaliwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto, kwa wanahabari kupata ushuhuda wa hatua za maboreseho hospitalini na maendeleo ya afya kitaifa.

## Maboresho Hospitali Rufani Temeke yatokomeza vifo kinamama kujifungua



Waziri Ummy Mwalimu(mwenye kilemba), akipata maelezo kutoka kwa watumishi wa Hospital ya Rufani Temeke, hivi karibuni. **PICHA: YASMINE PROTACE**

**Na Yasmine Protace**

KUIMARISHWA miundombinu katika mhimili wowote wa kuhudumia umma una maana kubwa katika sura ya maboresho. Hiyo inaenda mbali hadi katika huduma nyeti, ambayo ni afya ya umma.

Inapoangaliwa hilo kwa kina, ina maana kubwa katika miradi ya maendeleo ya afya na hivi sasa ujumbe wenye tafsiri unajionyeha katika Hospitali ya Rufani Temeke, jijini Dar es Salaam.

Hivi sasa imeboresha miundombinu yake, kwa kujipanga kuokoa maisha ya kinamama wajawazito, hususani katika kipindi cha kujifungua. Ni lengo linalotimizwa kwa kuboresha miundombinu yake, vifaa, pia huduma za afya kwenye ngazi za msingi kama zahanati na vituo vya afya.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, katika ziara yake hospitalini hapo hivi karibuni, kusikiliza maoni na changamoto kutoka kwa wananchi na watumishi wa hospitali hiyo, anasema:

"Mwaka 2018 vilikuwa vifo 19 vya wajawazito na 2019 walikuwa na vifo vinane tu, lakini kwa takwimu za kuanzia Novemba 2019, hadi leo hakuna mwanamke mjamzito aliyekuja hospitalini hapa na kupoteza maisha," anasema.

Waziri Ummy anashukuru mafanikio, kwamba yanatokana na kazi nzuri ya kiserikali kuwekeza kwenye huduma za afya nchini, ikiwamo ujenzi wa vituo vya afya na ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa.

"Hivi sasa, hapa Temeke kuna huduma za kibingwa za meno ambazo zamani hazikuwepo," anasema na kuongeza serikali kupitia wizara husika, inanuia kuhakikisha huduma zote za kibingwa zinapatikana kwenye hospitali za rufani za mikoa.

Anasema, kuna wastani wa wanawake 15 kati ya 100 nchini, wanaohitaji kupelekwa kujifungua katika hospitali za rufani za mkoa, kutokana na changamoto za ujauzito, akitoa mfano wa kitaalamu 'mtoto amekaa vibaya' au viashiria vya uzazi pingamizi.

Kuhusu vipimo, waziri anasema wizara yake imeongeza vipimo vya aina 'utra sound' na hivi sasa serikali imeboresha vituo vya afya vinavyoanza kutolewa kuanzia ngazi vituo vya afya vya umma na hospitali za wilaya nchini.

Anasema, ni hatua inayolenga kuhakikisha wananchi wanapata huduma, kuanzia ngazi ya msingi na hospitali za rufani za mikoa, kwa wagonjwa watakaopata rufaa.

"Kwa yeyote atakayefanya makusudi kukorofisha vipimo ili watu waende kupima kwenye vituo binafsi, tutawachukulia hatua, kwani ni wahujumu uchumi.

"Tunataka vipimo vyote vifanyike ndani ya hospitali, ila pale mashine haipo tutaruhusu. Lengo letu ni kujitosheleza kwa vipimo vyote kwenye vituo vya afya vya umma," anasisitiza Waziri Ummy.

### SAUTI HOSPITALINI

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Yudas Ndungile, anasema kutokana na maboresho ya miundombinu, hivi sasa wataalamu na vifaa tiba kwa mkoa wamepunguza wastani wa vifo 40 kila mwaka.

Takwimu za mwaka juzi (2018), ni kwamba ulikuwa na vifo186, huku mwaka uliopita ilikuwa 140 na matarajio walio nayo sasa ni kupunguza zaidi.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa Temeke, Dk. Meshack Shimwela, anasema hospitali hiyo imeondoa msongamano wa wajawazito, kwa sababu hivi sasa wananchi wengi wanafuata mfumo wa rufaa.

"Hivyo, kinamama wajawazito wanaofika kwenye hospitali hii, ni wale wenye changamoto ya uzazi. Kwa maana hiyo, wengi wanajifungua kwenye ngazi za chini ambako huduma za afya nazo zimeboreshwa," anasema.

AFYA

KICHOCHO

# ‘Kinawawinda’ watoto wawapo majini, kukikabili inahitaji ‘misuli’

• Taasisi Ifakara yajibebesha jukumu • Wilaya tano, Visiwa Victoria hatari • Mtafiti Levira: Tuko pabaya Afrika



Mazingira ya maji yanayotumika kusababisha kusambaa kichocho. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Beatrice Philemon**

***IKIWA ni mwendelezo wa makala kutoka kwa mwandishi wetu na wataalamu wa Taasisi ya Utafiti Ifakara (IHI), kuhusu uhalisia wanaokagua kitafiti kuhusu mazingira na afya nchini. Endelea:***

NENO kichocho si geni kwako kuanzia hospitalini na nje ya hapo. Mrejeo wa pili unaibua tena swali, unafahamu vyema maana yake?

Hapo ndipo Ofisa Mtafiti kutoka Taasisi ya Afya Ifakara (IHI), Mhandisi Mazingira, Beda Levira ana ufafanuzi wake wa maana halisi.

Anaanzisha maelezo ya tafsiri akitumia lugha ya kawaida, kwamba kichocho ni ugonjwa unaosababishwa na vimelea aina ya minyoo kutoka jamii ya ‘Schistosoma’ wanaoingia ndani ya mwili wa binadamu, kupitia ngozi hadi mfumo wa fahamu.

Mhandisi Levira anasema, madhara mojawapo kwa mgonjwa ni kukabiliwa na maradhi ya tumbo, husussan kuharisha kinyesi na mkojo wenye damu.

Anasema kuna ushahidi kichocho kinapatikana sana kwenye mazingira ya Ziwa Victoria, pamoja na visiwa vyake kama vile kisiwa cha Kome, Ukerewe, Rubondo, Ukara na Mwaisome.

Mtaalamu huyo anaeleza kwamba, ni ugonjwa unaonekana kwenye sehemu zenye maji yaliyosimama au kutuama akitoa mfano wa uzoefu halisi katika mikoa Pwani na Morogoro.

> **Kabla ya kutumia dawa, lazima ujue hivi vimelea vina shambulia sehemu gani ya mwili wako. Baada ya hapo daktari anaweza kukushauri utumie dozi ipi, tiba ipi na kwa dozi ya kiasi gani.**

Anasema, vimelea hivyo vya magonjwa vinakuwa ndani ya konokono wanaopatikana kwenye maji yaliyotuama na ndiko kichocho kinapenda kushambulia sana watoto, wakulima wa kilimo cha mpunga wakiwamo wavuvi.

“Ukienda kuogelea kwenye hayo maji au wale watu wanaolima mpunga kwenye hayo maji, wale vimelea (parasite) ndio wanaingia ndani ya miili yao kupitia kwenye ngozi na kwenda kushambulia sehemu zote za mwili ikiwamo ini,” anasema.

Anasema, inapotokea kichocho kimeingia kwenye mfumo wa mwili, kuna maeneo mbalimbali wanaweza kwenda kujishikiza na ndipo zinaweza kuanza kujitokeza.

Mara nyingi, vimelea hivyo vinaenda tumboni, halafu wanakaa baada ya wiki mbili na kuanza kutaga mayai, kisha baada ya mayai kutotolewa, vimelea vinaanza kuingia kwenye mfumo wa damu hadi kwenye eneo la ini na zinginezo mwilini.

“Wadudu hawa wanapenda kushambulia sehemu zote za mwili ila wakiingia mwilini, pia wanapenda kwenda sehemu za ini,” anasema.

Mhandisi Levira ana ufafanuzi kwamba ni kawaida watu wanapougua kichocho inawagharimu muda mrefu kugundua wanaumwa, kati ya miezi kadhaa hadi mwaka mzima, pasipo mtu kugundua anaumwa.

Anaendelea kwamba, mtu anapodumu na kichocho kwa muda mrefu, inamkaribishia madhara makubwa kiafya, kwa sababu vimelea vya minyoo kusafiri kwenye mifumo ya damu na kushambulia maeneo muhimu mwilini, ikiwamo ambayo kazi yake ni kuchuja sumu mwilini na kichwani kwenye ubongo na mfumo wa fahamu.

Ushauri wake ni kwamba, walima mpunga wajihami dhidi madhara, kwa kuhakikisha wanatumia mabuti kwenye majaruba ya kilimo cha mpunga hakuna vimelea au mayai ya kichocho kwa kutumia wataalamu kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kuhakikisha kama hakuna maambukizi ya vimelea.

Vilevile walima mpunga wanapaswa kujikinga kwa kuvaa mabuti ya mvua wawapo shamba wawazuie watoto wasicheze maji yaliyotuama muda mrefu.

Anasema takwimu za dunia zinaonyesha Tanzania ni Taifa la pili Afrika kuwa na mazingira ya kuvutia kichocho, ikifuatiwa na Nigeria.

Katika hilo, Kanda ya Ziwa, hasa mikoa ya Mara na Mwanza ndiyo inayoathirika zaidi, kutokana na takwimu za Taasisi ya Utafiti ya Magonjwa ya Binadamu, inayoonyesha asilimia 70 ya wagonjwa Tanzania wanatokea huko .

Msingi wa ugonjwa unaosababishwa na maji yasiyo salama na yametuama kwenye maeneo mengi.

### MADHARA YAKE

Hapo mtafiti Levira, anataja madhara ya ugonjwa makuu ni matatu, kwa kauli: “Mgonjwa wa kichocho inawezekana kupata ugumba, saratani ya kizazi au maambukizi ya ukimwi, kwa sababu inategemea mgonjwa alikosa huduma ya matibabu kwa sababu yupo vijijini sana ambapo hakuna huduma za matibabu.”

Pili, anasema wakati mtu anakuwa amedhurika pasipo kufahamu kitu anachoumwa, halafu anapuuzia kuishia kunywa vidonge, akidhani ni jambo la kawaida na uhalisia unajitokeza katika hatua ya baadaye, hali imeshakuwa mbaya.

Mtafiti Levira anasema, kuna wakati mgonjwa anakuwa na nia sahihi, lakini mazingira ya matibabu si rafiki kutokana na uhalisia wake, walakini wa miundombinu iliyopo na hata hali ya kipato kinapokuwa duni, anaishia katika vidonge vya tiba isiyoendana.

Anavieleza vimelea vilivyo, kwamba vina ncha kali na vinapoendelea kutoboa mishipa ya damu, vinasababisha ugumba kwa mwanamke.

“Sisi kama IHI (Ifakara) tunachokifanya katika kupambana na ugonjwa huu, ni kuelimisha jamii kuhusu madhara yatokanayo na ‘gonjwa’ hili hususani kuelezea vyanzo au mazalia ya vimelea vya ugonjwa’ na kuwashauri wananchi kutokomeza au kujikinga na madhara,” anasema.

### ELIMU ILIYOPO

Anasema, ni elimu waliianzisha katika mwaka 2014 hadi 2018 na mpaka sasa, kuna miradi iliyofanyika katika mikoa ya Mwanza, Pwani - Bagamoyo na Kilombero - Morogoro.

Mtafiti Levira anasema, lengo lao Taasisi Ufakara ni kujikita katika kutoa elimu, ili kuongeza ufahamu unaohusu ugonjwa huu na programu endelevu kwa maeneo husika, yanayoonekana ama tatizo au yameathirika na ugonjwa, ikiwamo elimu endelevu kwa wakazi wake.

Kuhusu wilaya za mkoani Mwanza zilizoathirika sana na kichocho kitaifa, idadi ya wagonjwa ikiwa katika mabano ni Buchosa (1,000), Ukerewe (1765), Nyamagana (600) na Ilemela (572).

Pia, anaeleza mwaka 2018 kuna jumla ya watu 17,000 walioathirika na ugonjwa huo klitaifa.

### ALIVYO MUATHIRIKA

Mhandisi Levira, anasema mgonjwa anajionyesha kwa kuwa na dalili kadhaa ikiwamo joto la mwili hadi zaidi ya sentigredi, anataja dalili za awali ni kuumwa kichwa, viungo na tumbo na dalili za baadaye zinajumuisha, mtu kukohoa kila mara, kuharisha na hata kukojoa damu.

Anashauri mgonjwa wa kichocho ni vizuri awaone wataalamu wa tiba ili kupata uhakika wake, kama ni kichocho au la na asikimbile kumeza dawa .

AFYA

# ‘Kinawawinda’ watoto wawapo majini, kukikabili inahitaji ‘misuli’

“Kabla ya kutumia dawa, lazima ujue hivi vimelea vina shambulia sehemu gani ya mwili wako. Baada ya hapo daktari anaweza kukushauri utumie dozi ipi, tiba ipi na kwa dozi ya kiasi gani,” anasema.

Kichocho kwa ujumla kilikuwa tatizo kubwa kipindi cha nyuma kabla ya mwaka 1997, hasa wanafunzi wa shule za msingi kwenye watoto wengi waliugua na tafiti nyingi zimewalenga, kwa sababu watoto wengi wanapenda kuogelea na kuchezea maji yaliyotuama, kuliko watu wazima.

Anarejea takwimu za kitafiti, kwamba mwaka 1992 kuna jumla ya wanafunzi 2,338 walifanyiwa uchunguzi, kuona kama wana vimelea vya kichocho na kati yao, asilimia 25 waligunduliwa kuwa navyo.



Watoto wakioga na kucheza katika maji yanayotumika kama haya napo kusababisha kusambaa kichocho. **PICHA: MTANDAO.**

### OPERESHENI RASMI

Mhandisi Levira anasema, hivi sasa tatizo la ugonjwa huo limepungua, kutokana na serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa afya, ikiwamo Shirika la Afya Duniani (WHO), walitumia njia kadhaa kutibu waathirika.

Pia, anasema ni hatua iliyoendana na kutibu mazalia ya vimelea hao, kupitia mbinu iliyojulikana kama ‘Massive Dosage Treatment’ (MDA) mwaka 1997.

“Hili lilifanyika Kanda ya Ziwa yote, iliunganisha Mkoa wa Mwanza na visiwa vinavyopatikana Ziwa Victoria, ikiwamo kisiwa cha Kome, Ukerewe, Rubondo, Ukara na Mwaisome, ila ufuatiliaji ulifanyika zaidi katika kisiwa cha Kome ambacho ni cha tano kwa ukubwa,” anaeleza

Mtafiti huyo wa IHI anasema kwa kutumia sensa ya mwaka 2002, Kisiwa cha Kome kilikuwa na watu 38,024 na ufuatiliaji, pia udhibiti kulianza mwaka 2009 kwa kutumia MDA iliyofanywa na serikali kupitia Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR)- Mwanza.

Anasema walioathirika na ugonjwa huu walipewa dawa na operesheni ya kuua mazalia ya vimelea vya ugonjwa wa kichocho, sehemu ambazo kuna maji yaliyotuama.

Mhandisi Levira anasema hivi sasa kichocho katika maenedo hayo kimepungua kwa kiasi kikubwa, sababu mojawapo ni wananchi kuelimishwa madhara yatokanayo na kuendesha shughuli au matumizi ya maji yaliyotuama kwa muda mrefu.

Pia, anasema operesheni ya kuua mazalia ya vimelea vya kichocho, juhudi zilizofanywa na serikali na WHO katika ufuatiliaji na matibabu kwa wanaoonekana kuugua hasa kwenye maeneo ya shule za msingi.

“Kulikuwa na programu maalum za kuelimisha wananchi kuhusiana na ugonjwa wa kichocho, kwa mfano Zanzibar kulikuwa na kitu kinaitwa ‘Zanzibar Elimination of Schistosomiasis Transmission - ZEST’ yaani Tokomeza ‘Gonjwa’ la Kichocho Zanzibar na serikali ilifanya hili mwaka 2011,” anatamka na kuendelea:



Wakulima wa mpunga katika majaluba yao, ambayo ni maeneo rafiki wa kueneza kichocho. **PICHA ZOTE: BERTRICE PHILEMON.**



Mhandisi Beda Levira, Ofisa Utafiti kutoka Taasisi ya Utafiti Ifakara.

“Tanzania Bara ilijumuisha masuala ya ‘dosing’ kwenye maeneo ambayo vimelea wanazaliana kwenye mabwawa na majaruba kulikuwa na programu inayoitwa Tokomeza Gonjwa la Kichocho na heninthiasis Tanzania (2004).”

Inaelezwa kuwa ni mradi uliofanyika katika mikoa 21 ya Tanzania Bara na ulisaidia kutokomeza mazalia ya vimelea, watoto walipewa dawa za minyoo kutoka mwaka 2004 hadi 2017.

Kwa mujibu wa takwimu zilizopo kuna jumla ya vidonge milioni 36.75 vilipokewa na serikali kutoka WHO kwa ajili ya kutibu kichocho Tanzania Bara .

### PICHA RASMI

Mhandisi Levira anasema ripoti ya mwaka 2017, inaonyesha kupunguzwa tatizo la kichocho kutoka asilimia 65 ya jamii mwaka 1981 mpaka asilimia mbili mwaka 2015.

> **Takwimu za dunia zinaonyesha Tanzania ni Taifa la pili Afrika kuwa na mazingira ya kuvutia kichocho, ikifuatiwa na Nigeria.**

Anasema, kichocho mara nyingi kinatokea vijijini, ambako kuna masikini wengi na inashauriwa kuboresha maisha ya watu yaendane na utokomezaji kichocho.

“Kwa mfano serikali inaweza kuamua kuboresha miundo mbinu ya barabara, shule au maji, kwa hiyo haya yanapofanyika yaendane sambamba na kutokomeza ugonjwa wa kichocho,” anasema.

Kwa mujibu wa mtafifi huyo, kabla ya serikali kuanzisha jitihada za kipekee, watu wengi walikufa kwa mwaka na taarifa zinaonyesha kichocho na madhara yake, bado ipo, ingawaje imepungua sana.

Mtafiti Levira, analalamika kuwapo pengo la kupatikana taarifa kamili za kuthibitisha uwepo wa kichocho, katika maeneo nchini.

Anasema mwaka 1992, jumla ya wanafunzi 3478 katika wilaya ya Ifakara walichunguzwa kama wana vimelea vya kichocho na kati yao asilimia 21 waligunduliwa kuwa na vimelea hivyo.

Pia, mwaka huo huo, jumla ya wanafunzi 2,500 katika mkoa wa Dar es Salaam walichunguzwa na kati yao asilimia 26 waligundulika kuwa na vimelea. Kisiwani Unguja, wanafunzi 517 waliochunguzwa, asilimia 17.4 walithibitishwa kuwa na vimelea vya ugonjwa huu.

Levira anasema baadaye mwaka 2012 uchunguzi ulifanyika kwa wanafunzi 360 katika wilaya ya Ukerewe ambapo kati ya hao, asilimia 28.5 waliathirika.

Vile vile kuna wanafunzi 238 wilayani Mafia walifanyiwa uchunguzi na kati yao, asilimia 4.2 waligundulika kuwa na kichocho.

Katika kutekeleza mkakati wake ndani ya mwaka 2020, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ina ajenda ya serikalni kuhakikisha kila mmoja anatoa ushirikiano katika kuelimisha jamii, vikiwamo vyombo vya habari kuhusu tiba za kujikinga na ugonjwa wa kichocho.

AFYA

# Ndoa jinsia moja ilivyoanzia kujificha zama hizo hadi uzazi

• Leo ni mabibi, mtoto ana miaka 45



'Wanandoa' wa jinsia moja wakiwa na mtoto wao Avrom (katikati). Kushoto ni 'mume' Phyllis Irwin na kushoto ni 'mke'Profesa Lillian Faderman. Chini, wakiwa pamoja. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**California, Marekani**

MWAKA 1971, kutokana na kuzinduliwa vuguvugu la wanawake liitwalo Women Liberation Movement , Profesa wa Chuo Kikuu katika jimbo la California, Lillian Faderman, aliwasiliana na mkurugenzi mmoja wa kituo hicho aitwae Phyllis Irwin, kufungua programu ya utafiti wa wanawake.

Ilikuwa mwanzo wa mapenzi yaliyodumu nusu karne , lakini yakakumbwa na changamoto nyingi. Wakati walipokutana kwa mara ya kwanza, mapenzi ya jinsia moja yalikuwa haramu.

"Tulionekana kuwa wahalifu karibia katika kila jimbo," ni kauli ya wanandoa hao na kuiendelea:"Wapenzi wengi wa jinsia moja walikuwa wakijificha."

Ni hatua ya pingamizi, japo halikuwazuia kuanzisha familia, huku wakijificha nyuma ya sheria kwa ajili ya kutambuliwa kuwa kundi rasmi la kifamilia.

Wanawake hao wanasimulia namna walivyopata mbinu za kutumia sheria ili familia yao iweze kutambuliwa, katika zama hizo jamii ilikuwa inalipinga.

Phyllis, mwenye miaka 91 sasa, anasema walipoanza uchumba, hawakujionyesha moja kwa moja kuwapo mapenzi ya jinsia moja kati yao, kwani walilifanya hilo kwa kuendesha uhusiano kwa siri kubwa.

> **"Lakini wengine walidhani kwamba walijua uhusiano wetu katika chuo kikuu. Walituita Phyllis na Lills kwa sababu tulikuwa pamoja kila mara.**



"Lakini wengine walidhani kwamba walijua uhusiano wetu katika chuo kikuu. Walituita Phyllis na Lills kwa sababu tulikuwa pamoja kila mara," anasimulia, huku akiangua kicheko.

"Nadhani wenzetu walituelewa na nilipoanza kuchapisha vitabu kuhusu historia ya wapenzi wa jinsia moja, niliona kana kwamba kila mmoja wetu alielewa kwamba tulikuwa wanandoa," anaeleza.

Miaka mitatu ya kudumu uhusiano wao, waliamua kupata mtoto. Lilian ambaye ni mdogo kwa miaka 11, alienda kumuona mtaalamu wa masuala ya ujauzito.

Hata hivyo, kupewa ujauzito kwa njia ya kisayansi, halikuwa jambo la kawaida, hususan kama mtu hana uhusiano wa kimapenzi na mwanamume, lakini Lillian alifanikiwa kumshawishi daktari amsaidie.

Alijenga hoja pasipo kueleza ukweli wa kilichomfanya yeye kutaka mtoto bila ya kuwa na uhusiano na mwanaume, akisimulia ilivyokuwa: "Daktari aliniuliza kwa nini sijaolewa iwapo nataka kuwa na mtoto?, anakumbuka.

"Nilimjibu, nina umri wa miaka 34, nina shahada ya udaktari na wadhifa wa Naibu wa Rais wa Elimu katika chuo, nadhani inagharimu kupata wanaume," anasema.

Anakumbusha namna daktari alivyomjibu kirahisi kwa kauli: "Naelewa unachosema na alinipachika mimba hiyo kupitia mbinu hiyo ya kisayansi ambayo ilifanikiwa." Kwa mujibu wa Lilian, wakati huo sheria haikuwaruhusu wanawake kuoana. Anaendelea: "Tungefurahia kuoana, sheria inasema haiwezekani mtoto kuwa na wazazi wa jinsia moja na tulijua kwamba ilikuwa muhimu kuwa na mshikamano wa kisheria, kwa sababu ya Avrom (mtoto wao)."

Anataja faida ya kumchukua mtoto Avrom na kuishi naye ni kwamba, alizaliwa wakati hapakuwapo watoto wengi wenye wazazi wa jinsia moja na njia rahisi ya kubadilisha hilo ni kumtambulisha mtoto Phyllis ni bibi yake, huku mtoto naye alimuona ni rafiki wa mama yake.

**WAMEKUWA WATATU**

Mzaliwa huyo wa mwaka 1975 hivi sasa ana umri wa miaka 45, mama yake Lilian alijifungua mtoto kwa jina Avrom na aliyempeleka hospitalini alikuwa 'mumewe' Lilian alipotaka kujifungua, huku akijawa na hofu.

Kila kitu kilifanyika ilivyopangwa na mwanamke huyo alirudi nyumbani, kuanza maisha mapya ya watu watatu.

Hata hivyo, wakaanza kugundua vikwazo vya familia yao kisheria, Lili akieleza: ""Kile kilichotutia wasiwasi zaidi ni kwamba, Avrom alikuwa mgonjwa na Phyllis alilazimika kumpeleka kwa daktari. Hakuwa mzazi wake kamili, hivyo basi nililazimika kumpatia barua rasmi aliyobeba."

Kilichonikwaza hasa ni kwamba, iwapo kitu kingenitokea, asingekuwa na haki kisheria kudai kuwa mwanawe, kwani 'mume' huyo hakujulikana kisheria.

Lilian anarejea mwongozo wa kisheria jimboni California, iwapo kuna tofauti ya miaka 10 au zaidi kati ya watu wawili wazima, mmoja anaweza kumchukua na kuishi naye, jambo lililompa fursa Phyllis, kwa kuwa pengo la kiumri lipo.

Lilian anasema, uhusiano wake na Phyllis ulikuwa na sura ya 'kuchumbiana' na anasimulia zaidi: "Hatukuliona suala hilo kuwa baya (tofauti ya kiumri) kwa sababu hatukujihisi kama mama na mwanawe, tulifanya hivyo kama njia ya kukwepa sheria."

***Habari na picha ni kwa mujibu wa BBC***



# Viongozi waagizwa usimamizi sheria

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Ruben Mfune, amewaagiza wenyeviti wa vijiji na vitongoji kusimamia kanuni na sheria za uongozi ili kuondoa malalamiko kutoka kwa wananchi, ambayo yamekuwa yakihusishwa na matumizi mabaya ya madaraka.

Mfune alitoa maagizo hayo juzi kwenye Baraza la Mamlaka ya Mji Mdogo wa Rujewa ambalo lilikuwa linajadili masuala mbalimbali ya maendeleo ikiwamo mapitio ya bajeti na utekelezaji wake.

Alisema kumekuwa na malalamiko kadhaa kutoka kwa wananchi kuhusu matumizi mabaya ya madaraka, ambayo yanahusisha manyanyaso, hivyo alisisitiza wenyeviti wa vitongoji na vijiji waliochaguliwa hivi karibuni wawe wa mfano katika uongozi.

"Mliwaomba wenyewe wananchi wawachague hamkulazimishwa hivyo watumikieni kwa nguvu zote bila kujali itikadi za kisiasa na hatimaye kuleta maendeleo," alisema Mfune.

Aliwasisitiza wenyeviti hao kutojenga matumaini ya kunufaika na chochote kupitia uongozi huo badala yake wawe tayari kuwaongoza wananchi pamoja na kutekeleza maagizo ya serikali ikiwamo kufanya vikao vya kisheria na kufanya mikutano ya hadhara. Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Aswege Kaminyoge, aliwashauri wenyeviti wa vijiji na vitongoji kuhakikisha wanafanya vikao vya kisheria vinavyotakiwa kufanyika kwa wananchi pamoja na kupeleka taarifa kwa uongozi wa mamlaka ya mji mdogo Rujewa.

Aliwaambia kuwa viongozi waliopita walikuwa wanaitisha mikutano yao kila mwezi kwa asilimia 100 hivyo na wao wasimamie hilo sambamba na kutekeleza ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwenye masuala ya afya na elimu.

Mwenyekiti wa Mamlaka Mji Mdogo Rujewa, Chameta Godigod, aliwakumbusha wenyeviti hao kuendelea kusimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa kwenye baadhi ya shule pamoja na ujenzi wa stendi mpya ya Igawa ambayo ukarabati wake unaendelea.



Baadhi ya wajasiriamali wa Jiji la Mbeya, wakiendelea na shughuli zao, kwenye vizimba vya Soko la Kimataifa la Mwanjelwa jijini humo, jana, ambapo wanawalalamikia wenzao wanaopanga bidhaa zao nje ya soko hilo, kwa maelezo wanawazuia wateja wasiingie sokoni humo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Kichocheo mimba shuleni chaanikwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TABIA ya baadhi ya wazazi kufanya mazungumzo na wanaume wanaowapa mimba wanafunzi na kukubaliana katika ngazi ya familia bila watuhumiwa kufikishwa kwenye vyombo vya dola, imetajwa kuwa chanzo cha watoto wa kike kukosa haki ya kupata elimu mkoani Mbeya.

Hayo yalisema juzi na Mratibu wa Chama cha Wasaidizi wa Kisheria Mkoa wa Mbeya (Mbepace), Laiki Ndagile, alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu changamoto mbalimbali zinazowakabili watoto wa kike.

Alisema Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa inayoongoza nchini kwa kuwa na mimba nyingi za utotoni.

Alidai familia nyingi zinafanya mazungumzo na wanaume waliowapata mimba wanafunzi wakishinikiza kupewa mahari ili suala hilo walimalize.

Alisema kitendo hicho ni cha kumdhulumu mtoto wa kike kupata haki yake ya kielimu licha ya familia kutaka kunuifaika hivyo aliitaka jamii kubadilika na kuachana na mtindo huo ambao unalenga kumkandamiza mtoto. "Wazazi wamekuwa chanzo cha wanafunzi wa kike kushindwa kutimiza ndoto zao hii inatokana na tamaa za kupata mali haraka na kusahau wajibu wao na kuwaachia huru wanaume wanaowapa mimba mabinti," alisema Ndagile.

Alikemea vikali tabia ya wanaume kufanya ngono na watoto wa kike akiwataka kuwaacha wasome ili wafikie malengo yao.

Alisema mara nyingi kinababa wamekuwa wakiwasisitiza watoto wa kike kujitunza na kusoma kwa bidii lakini tena wanaanza kuwarubuni kwa zawadi na ahadi nyingi hatimaye wanakatisha ndoto zao.

Mmoja wa wasaidizi wa kisheria, Neema Joseph, ambaye ni mkazi wa Uyole jijini Mbeya, alieleza vikwazo vinavyomkabili msichana katika kutimiza malengo yake kuwa ni suala la usawa wa kijinsia.

## Vijana wahimizwa kuchangamkia fursa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

VIJANA wamehamasishwa kuzitumia fursa mbalimbali za kiuchumi zilizoko maeneo yao kwa kuanzisha miradi ya maendeleo badala ya kukaa vijiweni kupiga soga au kujiingiza kwenye vitendo vya uhalifu.

Wito huo ulitolewa jana na Mratibu wa Shirika lisilo la kiserikali la Shop, Maria Dominick, wakati akifanya tathmini ya utekelezwaji wa mradi wa 'Saidia wahitaji' ambao unafikia kikomo hivi karibuni.

Dominic alisema ziko fursa nyingi kwenye jamii, lakini vijana wameshindwa kuzitumia ipasavyo lakini wanaendelea kuilaumu serikali kwamba haijawasaidia kitu chochote.

Alisema katika utekelezaji wa mradi wa 'Saidia Wahitaji' walijikita zaidi kutoa elimu kwa vijana na makundi mengine kuwapa maarifa namna ya kujikwamua kiuchumi pamoja na kutoa misaada ya hali na mali kwa makundi maalum.

"Vijana ni tegemeo kwa taifa katika kuleta maendeleo ili kufanikisha hilo lazima kila mmoja atambue wajibu wake badala ya kunyoosheana vidole sisi wadau tumeonyesha jitihada zetu kupitia huu mradi ambao umegusa maeneo mengi ndani ya jamii zetu," alisema Dominic.

Akizungumzia suala la vijana kujikwamua kiuchumi Ofisa Maendeleo wa Jiji la Mbeya, Ilikija Mshana, alisema Halmashauri ya Jiji ikitekeleza agizo la serikali la kuwapatia vijana mikopo kwa ajili ya shughuli za ujasiriamali.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2018/2019 zaidi ya vijana 800 walinufaika na mikopo inayotolewa na halmashauri na kwamba baadhi yao tayari wameanza kutoa ajira kwa wenzao.

Aidha, Mshana aliwasisitiza vijana kutumia vyema maarifa wanayopewa na mashirika kuhusu ujasiriamali kwani yana lenga kuisaidia serikali kupambana na tatizo la ajira.

Ofisa ufuatiliaji kutoka Shirika la Shop, Yusuph Simbaya, alisema licha ya mradi wa 'saidia wahitaji' kufanya vizuri kwa vijana kujikwamua na umaskini ndoto yao kubwa ni kuhakikisha hata kundi la wajane nalo linanufaika na fursa mbalimbali.

Baadhi ya vijana walionufaika na mradi huo, akiwamo Josephat Alinanuswe alisema mafunzo ya ujasiriamali waliyoyapata imekuwa ni njia ya kuzitambua fursa mbalimbali zinazopatikana kwenye maeneo yao.



# Tarura wakimbia 'zigo' la kodi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amesema Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura), sasa utaokoa zaidi ya Sh. milioni 500 zilizokuwa zikitumika kulipia pango kila mwaka baada ya kujenga jengo lake.

Akizungumza baada ya kukagua ujenzi wa jengo hilo jana, Waziri Jafo alisema fedha iliyokuwa ikitumika kulipa kodi ni nyingi, hivyo aliuagiza wakala kujenga jengo lake ili kuondokana na matumizi hayo.

"Tumeokoa kodi ambayo ilikuwa inatumika kila mwaka Sh. milioni 500, ndiyo maana nilisema sitaenda tena bungeni kuomba fedha na nilisema mwaka 2020/21 sitapeleka bajeti bungeni kuomba fedha Tarura wapatiwe kwa ajili ya kulipa pango," alisema.

Jafo alibainisha kuwa aliagiza ramani iliyotumika kujenga jengo la Ofisi ya Tamisemi itumike kujenga jengo hilo jirani na ofisi hiyo kutokana na kuwa na eneo kubwa.

"Nimshukuru Rais John Magufuli kwa kufanya Dodoma kuwa makao makuu ya nchi na kuelekeza kujengwa kwa majengo ya ofisi katika mji wa serikali na alitoa fedha kwa Tamisemi, tulianza ujenzi wa jengo la ghorofa," alisifu.

Aliongeza kuwa kutokana na eneo walilopewa kuwa na ukubwa wa ekari 11, waliamua kujenga majengo mawili ya ghorofa.

"Majengo haya ramani yake ni moja, lakini Tamisemi tulisimamia na kuamua kujenga kwa utaratibu wa 'force account' tukitumia Wakala wa Majengo (TBA) kama mshauri, ofisi yangu imehusika na ujenzi huu kwa kipindi cha kufuatana," alisema.

Jafo alibainisha kuwa jengo la Tamisemi lilitumia Sh. bilioni 1.6 huku Tarura hadi kukamilika kwake itatumia Sh. bilioni 2.7.

"Ramani ya ujenzi wa majengo ni moja, lakini gharama ni tofauti kwa kuwa baadhi ya vitu havikuwekwa kwenye ujenzi wa jengo la Tamisemi, vimewekwa kwenye jengo la Tarura kwa kuwa tumejenga kwa kupumua, kama mnavyoona ni jengo lilolowekwa vioo wakati lile la awali hatukuweka," alisema.

Jafo aliishukuru TBA kwa kushauri na usimamizi kwenye ujenzi huo pamoja na Chuo Kikuu cha Mbeya (MUST) ambacho kimelijenga kupitia utaratibu wa 'force account'.

Aliagiza wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi kujenga majengo kupitia utaratibu huo na kukamilisha kwa wakati.

"Kuna wengine huko ninakoenda wanajenga jengo wanatumia Sh. bilioni 10, jengo halishi miaka minne, wakati hapa kwa kipindi kifupi tumejenga majengo na yamekamilika kwa gharama ndogo, maeneo mengine hawawezi kujenga jengo kama hili kwa Sh. bilioni 2.7, wangejenga kwa Sh. bilioni saba au nane," alisema.

Meneja Matengenezo ya Barabara wa Tarura, Hamidu Mataka, alisema ujenzi ulianza Januari mwaka 2019 na jengo limekamilika kwa asilimia 98 huku asilimia mbili iliyobaki ikiwa ni matengenezo madogo ambayo baada ya wiki mbili yatakuwa yamekamilika na kuanza kutumika.



Baadhi ya wafanyabiashara ndogondogo maarufu kama machinga wa eneo la One Way, jijini Dodoma, wakionekana kubuni utaratibu mzuri wa kupanga bidhaa zao na kuweka mabanda ya muda, ili bidhaa zao zisiharibike na vumbi au kunyeshewa na mvua. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Viongozi wa dini wapewa somo kuepuka wanasiasa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

VIONGOZI wa dini nchini, wametakiwa kujiepusha na wanasiasa wanaovuruga amani na badala yake wahamasishe waumini wao kulinda amani iliyopo.

Rai hiyo ilitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), anayeshughulikia afya, Dk. Dorothy Gwajima, alipozungumza na viongozi wa Jumuiya ya Maridhiano ofisini kwake jijini hapa.

Alisema ni vyema viongozi hao kuwahamasisha waumini wanaowaongoza, kuilinda amani kwa gharama yoyote ili isivurugwe na watu wachache wasiopenda maendeleo ya taifa.

Dk. Gwajima aliwataka viongozi hao kutotumika na wanasiasa wavurugaji wa amani ambao watapita kwao kujipendekeza. "Viongozi wa nchi hii toka enzi ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere tumeizoea kuwa na amani, kwa maana hiyo msikubali kuwaombea wanasiasa hao watakapoanza kujipitisha kwenye maeneo yenu," alisema.

Aliwataka viongozi hao kufanya kazi kwa pamoja na serikali katika kufichua maovu.

Naibu Katibu huyo pia aliwahimiza waumini wao kufanya kazi ili kujiinua kiuchumi.

Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo nchini, Askofu Osward Mlay, alisema wamejipanga kukataa wanasiasa watakaoleta siasa zao za matusi na za kuwagawa Watanzania.

"Kamwe hatutakubali kiongozi yeyote wa siasa atakayekwenda kinyume cha maadili ya nchi yetu, tutapaza sauti zetu kanisani na msikitini kukataa," alisema.

# Skauti yajipanga kuikabili rushwa shuleni na vyuoni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHAMA cha Skauti nchini kimejipanga kuanza kutoa elimu kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu ili kukabiliana na vitendo vya rushwa ikiwamo ya ngono inayowatesa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkuu wa Skauti Tanzania, Mwantumu Mahiza, alisema wameingia makubaliano na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kutoa elimu hiyo ili wanafunzi wapambane na vitendo hivyo.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kutokomeza rushwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Alibainisha kuwa kumekuwa na rushwa ya ngono ambayo ni kubwa na inatesa jamii hususani vijana wadogo ambao ni nguvu kazi taifa, hivyo kuna haja kuwa na mikakati ya kuitokomeza.

"Tumeamua kushirikiana na Takukuru ili kuhakikisha tunatokomeza kabisa rushwa nchini," alitamba.

Mahiza alisema kwa sasa ana kazi kubwa ya kuingia katika shule hadi vyuo ili kutoa elimu kwa vijana.

"Kwa sasa, kuna vuguvugu la siasa, pia sisi skauti tutapambana ili kutokomeza rushwa na niwaase wanasiasa, hakuna sababu ya kukashfiana, kinachotakiwa ni kuandaa mikakati ili kuwashawishi wananchi wawachague," alisema.

Alisema elimu watakayoenda kutoa itasaidia kwa kiasi kikubwa watu kujua si halali kwao kutoa na kupokea rushwa.

Kiongozi huyo alisema rushwa ya ngono inatesa na kusababisha vijana wengine kupata maambukizo ya Virusi vya Ukimwi (VVU).

"Tutasaidiana na klabu za wapinga rushwa ili kuwaokoa wanafunzi, na wahadhiri wa vyuo waache tabia ya kuwarubuni wanafunzi ambao wanategemewa na taifa la kesho," alionya.

Alisema wanatarajia kuzindua kongamano la elimu ambalo litakuwa kichocheo cha utoaji elimu elekezi kwa jamii.

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema wananchi bado wana mwamko mdogo wa kutoa taarifa za rushwa, hali inayosababisha taasisi hiyo kufanya kazi kwa shida.

Kibwengo alitoa wito kwa jamii kuendelea kutoa taarifa pale wanapoona sehemu kuna vitendo vya rushwa.



# Dk. Shein azielekeza wizara kituo cha afya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ameitaka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kushirikiana na Wizara ya Afya na kuwa na mipango ya pamoja itakayowezesha uendelezaji wa Kituo cha Afya Mbuzini na kuwa Hospitali ya Wilaya Magharibi 'A' Unguja.

Dk. Shein alitoa maagizo hayo Ikulu Zanzibar, wakati akipokea taarifa ya utekelezaji ya mpango kazi ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2019/2020.

Alisema jengo hilo linaweza kuendelezwa kupitia bajeti za wizara hizo na ujenzi wake kufanyika awamu kwa awamu, ili liweze kuwasaidia wananchi wa maeneo hayo na vitongoji jirani.

Alisema jengo hilo la zamani lililogharimu fedha nyingi katika ujenzi wake lipo mahala pazuri na linafaa kuendelezwa kwa dhamira ya kuwasaidia wananchi katika upatikanaji wa huduma za afya.

Aidha, Dk. Shein aliwakumbusha wakuu wa mikoa juu ya dhima waliyonayo katika ulinzi na usalama wa mikoa yao kwa kuhakikisha hakuna mgeni au mwekezaji anayefanya shughuli zinazoashiria uvunjifu amani na kuingilia usalama wa nchi.

Rais Dk. Shein ilitoa kauli hiyo kufuatia taarifa ya kuwapo raia kutoka Uingereza aliyetengeneza makazi juu ya mibuyu katika eneo la Pete, huku kukiwa na viashiria kadhaa katika makazi hayo vinavyohatarisha usalama wa nchi.

Kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama, aliagiza kufanyika uchunguzi ili kubaini uhalali wa mgeni huyo kuwapo nchini na kumiliki eneo hilo pamoja na vifaa anavyomiliki, vinginevyo hatua za kiusalama zichukuliwe dhidi yake.

Aidha, aliwataka viongozi wa wizara hiyo pamoja na viongozi wa Mkoa Kusini na Wilaya Kusini kukutana na kinamama wa Shehia ya Kizimkazi wanaojishughulisha na kazi za kuanika dagaa na kuwasikiliza ili kuona vipi wataweza kuwasaidia kuendeleza shughuli zao, huku kukiwa na katazo la kuepukana na uharibifu wa mazingira katika ghuba ya Menai.

# Watoto 13 wahofiwa kufa saratani ngozi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WATOTO 13 wamefariki dunia kutokana na kupata uvimbe unaodhaniwa ni saratani ya ngozi katika Wilaya ya Micheweni Kisiwani Pemba kuanzia Oktoba 2019.

Akiwasilisha taarifa ya serikali kutokana na ugonjwa huo uliibuka katika wilaya hiyo, Waziri wa Afya, Hamad Rashid Muhamed, alisema baada ya kupata taarifa ya kuwapo kwa ugonjwa huo wizara iliandaa timu ya ufuatiliaji kuhusu maradhi hayo.

Alisema jumla ya wagonjwa 628 wenye matatizo mbalimbali ya ngozi waligundulika na walihudumiwa, kati yao 106 walikuwa ni watoto wa chini ya miaka mitano na 522 walikuwa na zaidi ya miaka mitano.

"Watoto 33 waligundulika kuwa na ugonjwa wa ngozi unaojulikana kwa jina la kitaalamu ( Xeroderma Pigmentosum), 13 kati yao walifariki kutokana na kupata uvimbe unaodhaniwa kuwa ni saratani ya ngozi walipokuwa wadogo na 16 kati yao bado wapo hai," alisema.

Alieleza kuwa pia watoto saba waligundulika kuwa na uvimbe unaodhaniwa kuwa ni saratani ya ngozi sehemu mbalimbali na kuhitaji matibabu ya haraka ya upasuaji, na kuwa walipelekwa Hospitali ya Muhimbili kwa ajili ya upasuaji na matibabu zaidi.

Waziri huyo alisema wale wote wanaotaka kusaidia wagonjwa wafuate utaratibu wa serikali uliopo wa rufani na kuhakikisha wagonjwa ambao wanaombewa msaada kuwa wawazi na wawe wanakwenda kunufaika wale wanaohitaji msaada huo.

Aidha, aliwaomba wazazi au watu wanaowahudumia wagonjwa ambao ni watoto watoe ushirikiano wa dhati bila ya kuweka mbele maslahi yao binafsi.

"Wizara inapenda kuwatoa hofu wananchi kuwa ugonjwa wa ngozi (Xeroderma Pigmentosum) si ugonjwa unaoambukiza kwa kugusana au kunywa maji au kwa njia ya hewa," alisema Hamad Rashid.

Hamad alieleza kuwa hatua zinazopaswa kuendelea kuchukuliwa ni kuendeleza kliniki kwa ajili ya watoto wenye ugonjwa wa ngozi Xeroderma Pigmentosum baada ya miezi mitatu ambapo watagaiwa dawa, watachunguzwa viashiria vya saratani na upasuaji utakapohitajika.

Alisema pia kuendelea kutoa elimu juu ya maradhi hayo kupitia vyombo vya habari, kuanzisha uchunguzi wa matatizo ya ngozi shuleni baada ya kugundua maradhi mengi ya kuambukiza yatokea sana kwa watoto pamoja na kutoa matibabu shuleni.

"Pia kufanya kampeni ya uelimishaji wa matatizo ya ngozi na matumizi sahihi ya dawa na sabuni hasa katika uso na kuhakikisha dawa zote zinazohitajika kwa matibabu hayo zinaingizwa katika orodha ya dawa muhimu zinazoagizwa," alisema.



Waziri wa Afya wa Zanzibar, Hamad Rashid Mohammed, akiwasilisha taarifa kuhusu ugonjwa wa ngozi unaodhamiwa kuwa ni saratani ya ngozi ulioenea katika Wilaya ya Michewemi Pemba, wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Changamoto X-ray Pemba yafanyiwa kazi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema kuwa baadhi ya hospitali hasa Pemba zilikuwa na changamoto katika huduma za X-ray, hivyo kwa kuwajali wananchi tayari limeshafanyiwa kazi.

Waziri wa Wizara hiyo, Hamad Rashid Muhamed, aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Paje, Jaku Hashim Ayoub.

Jaku alitaka kujua wizara itatoa tamko gani kuhusu tatizo hilo na hatua gani za haraka zilizochukuliwa kuirekebisha changamoto hiyo. Waziri Hamad alisema waliwatafuta wataalamu na kuwapeleka Pemba ambapo kati ya X-ray katika Hospitali ya Wete na vitongoji zilipatiwa ufumbuzi na zinaendelea na kazi ya kutoa huduma, lakini katika Hospitali ya Micheweni inaendelea na matengenezo.

Alisema wanajipanga kununua X-ray nyingine za kisasa ili kuondoa changamoto za utoaji wa huduma hiyo.

Alieleza kuwa mashine hizo zimekuwa zikiharibika mara kwa mara kutokana na mahitaji makubwa ya wananchi wanaoenda kufuata huduma hiyo hospitali. Alisema wananchi wengi kwenda hospitali kufuata huduma mbalimbali ikiwamo za X-ray ni miongoni mwa mafanikio katika kuimarisha huduma za afya, na kwamba wananchi wamehamasika kufuata huduma za afya na kuwa na imani na serikali yao katika kupata huduma hiyo. "Muheshimiwa Spika, wizara ipo katika hatua za mwisho kukamilisha uajiri pindi tutakapokamilisha tutawapanga katika hospitali ambazo zinachangamoto ikiwamo Hospitali ya Chakechake Pemba.

Akijibu swali la nyongeza aliloulizwa na Mwakilishi wa Mgogoni, Shekhe Hamad Mantar, kuhusu virusi vya corona ambavyo vimeingia nchini Italia na kuitaka serikali kutoa tamko kutokana na Zanzibar kupokea wageni wengi kutoka Italia, Waziri Hamad alisema serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili ugonjwa huo usienee nchini.

Alieleza kuwa serikali imekuwa na tahadhari kubwa na ugonjwa huo na ndio maana imekuwa ikifanya uchunguzi kwa wageni wnaoingia nchini, na imeweka wataalamu wa afya katika viwanja vya ndege na bandari.

# Wavuvi watakiwa kuhama mwalo

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

MVUA zinazoendelea kunyesha zimesababisha kina cha maji ya Ziwa Victoria kuongezeka, hali iliyosababisha Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza, John Wanga, kuwataka wavuvi wa mwalo wa Butuja kuhama eneo hilo na kwenda mialo mingine.

Wanga alitoa ushauri huo alipokuwa akitoa ufafanuzi wakati akizungumza na Nipashe kuhusu suala la mwalo wa Butuja uliokumbwa na mafuriko na kusababisha wavuvi na wananchi wanaofanya shughuli eneo hilo kuwa na wakati mgumu.

Walimwomba Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kuwaboreshea mwalo, huku wakipatiwa eneo la muda lililopo karibu na mwalo huo wakati wakisubiria matengenezo.

Wanga alisema eneo hilo la mwalo wa Butuja siyo rasmi bali ni kwa ajili ya kuendelezwa kwa kujengwa mabwawa ya majitaka ambapo Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Mwanza (MWAUWASA) wanapaswa kuwalipa fidia wananchi wa maeneo hayo ili wapishe eneo hilo, na kuwa hajajua ni lini watalipwa kwani hawezi kuwasemea kwa vile siyo eneo lake la kazi.

Alisema kutokana na hali hiyo, wanapaswa kuhama kwenda kwenye mialo ambayo ni teule ikiwamo Mihama, Kayenze ndogo, Igombe au Igalagala pamoja na Kirumba wakafanye shughuli zao za uvuvi.

Alisema katika eneo hilo kwa sasa kuna mabwawa, lakini wananchi wanaishi huku shughuli za uchumi zikiendelea hasa za uvuaji samaki kutokana na eneo hilo kuwa rahisi kufikika katika masoko.

"Eneo hilo siyo mahususi la kufanya shughuli hizo, siyo kuwa hatutaki wafanye shughuli zao ila halifai kwa sasa kutokana na mvua nyingi, na kina cha maji kuongezeka," alisema.

Mwenyekiti wa Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi ndani ya mita 60 kutoka mwambao wa ziwa (BMU) ya Butuja, Dickson Maila, alisema tangu kupatwa na madhara hayo wamepokea viongozi akiwamo Naibu Meya wa Manispaa ambaye ni diwani wao ambapo walimweleza na kuahidi kulifuatilia suala hilo sambamba na Mkuu wa Wilaya.




Mkurugenzi wa Halmashauri ya Tanga, Daudi Mahej (wa pili kulia), akishikana mikono na Mkurugenzi wa Idara ya Wafanya Biashara wa Benki ya NBC, Elvis Ndunguru, kuashiria uzinduzi rasmi wa Klabu ya Biashara katika Mkoa wa Tanga juzi. Kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Wateja wadogo na wakati wa benki hiyo, Evance Luhimbo na Meneja wa Benki hiyo Tawi la Tanga, Asia Chambega. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Watano mbaroni tuhuma za mauaji ya kikongwe

**Na Edwin Said,** NZEGA

JESHI la Polisi mkoani Tabora, linawashikilia watu watano wanaotuhumiwa kumuua Andrea Kipela (72), mkazi na mkulima wa Kijiji cha Wita, Kata ya Ndala wilayani Nzega.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara kati ya wanakijiji na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Tabora, Rauliani Fabrian, alisema jeshi hilo linawashikilia watu watano kwa ajili ya mahojiano kuhusu mauaji hayo yanayodaiwa kuchagizwa na mgogoro wa ardhi.

Alitoa wito kwa wananchi kushirikiana na jeshi hilo ili wote wanaohusika na ukatili huo wachukuliwe hatua za kisheria.

Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, alisema wote watakaobainika kuhusika na mauaji dhidi ya mzee huyo, serikali haitasita kuwachukulia hatua za kisheria.

Alisema serikali ya mkoa kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama inawaomba wananchi kutoa taarifa za wale wote walioshiriki kutekeleza mauaji hayo.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora, Robart Makungu na Mkuu wa Wilaya ya Nzega, Godfrey Ngupula, walisema watailinda familia ya mzee huyo ulinzi, huku wakiwataka wananchi kuwa walinzi wa kwanza wa familia hiyo na wanafamilia hiyo, kila mmoja kujilinda.

Awali, akielezea eneo linalodaiwa kuwa na mgogoro na kusababisha kifo cha Mzee Kipela, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, Yahaya Sekiete, alisema lina ekari 180 ambazo zilikuwa hazijapimwa, na akaahidi kuwa baada ya mavuno zitapimwa na kukabidhiwa kwa wanafamilia.

Alisema ekari hizo zinatambuliwa na mahakama ya ardhi na Mzee Kipela alishinda kesi ya mgogoro wa ardhi iliyokuwa mahakamani.

Mzee Kipela aliuawa Februari 2 mwaka huu, huku chanzo cha kuuawa kwake kikidaiwa kuwa ni mgogoro huo wa ardhi.

## Zantel yaibuka na 'Bonga Mpaka Basi'

**Na Sabato Kasika**

KATIKA kuimarisha huduma zake, Zantel imezindua bidhaa ya bando liitwalo 'Bonga Mpaka Basi' ili kuwawezesha wateja wake kupiga simu kwenda mitandao yote kwa gharama nafuu.

Uzinduzi huo ambao ulifanyika juzi Visiwani Zanzibar, unalenga pia kuwapa kifurushi kimoja cha 'Bonga Mpaka Basi', na kwamba bidhaa hiyo inatajwa kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii hapa nchini.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, Mkuu wa Biashara wa Zantel, Aneth Muga, alisema bidhaa hiyo imelenga kuboresha huduma za mawasiliano ili wateja wapate mawasiliano ya uhakika wa gharama nafuu.

"Tunatambua kuwa huduma za mawasiliano hasa za sauti na data ni muhimu kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii, na watu wengi hutegemea mawasiliano ili kufanya shughuli za kila siku hasa biashara, kupata huduma za kijamii kama afya, malazi na usafiri," alisema Muga.

Alisema, huduma hiyo itawafanya wateja wa Zantel kupiga simu kwenda mitandao mingine kwa gharama ile ile ya kupiga ndani ya mtandao kupitia kifurushi kimoja cha 'Bonga Mpaka Basi'.

Muga aliongeza kuwa kwa njia hiyo, Zantel inatekeleza mkakati wa kuhakikisha inafikisha huduma kwa watu wengi zaidi na kuchochea maendeleo yao kupitia mawasiliano bora.

Kwa upande wake Mkuu wa Zantel Zanzibar, Mohammed Mussa, alisema kampuni hiyo imeendelea kufanya uwekezaji kwenye miundombinu ya mawasiliano Visiwani Zanzibar, ambako ni eneo kitovu cha biashara kwao kwa lengo la kuboresha huduma za mawasiliano.

Anasema uwekezaji huo umefanyika kupitia teknolojia ya fibre optic cable inayoiunganisha Tanzania na nchi nyingine na imeiwezesha Zantel kutoa huduma za sauti na data kwa kampuni nyingine za simu hapa nchini."

## HABARI KIMATAIFA

# Corona yazidi kusambaa, yaingia Algeria

**ALGIERS,** Algeria

WAZIRI wa Afya nchini Algeria, Abdel Rahman Ben Bouzid, amethibitisha nchi hiyo imepokea kisa cha kwanza cha mtu kuambukizwa virusi vya ugonjwa wa Corona.

Waziri Bouzid alisema kuwa mgonjwa huyo ni mwanamume raia wa Italy aliwasili nchini humo Februari 17. Hata hivyo mtu huyo ameshatengwa kwa sasa.

Algeria imekuwa nchi ya pili Afrika kuthibitisha kupata mgonjwa wa virusi vya Corona.

Misri ilikuwa ya kwanza kuthibitisha kupatika kwa kisa mtu aliyekuwa anaugua virusi vya Corona lakini baadaye ikatangaza kwamba mgonjwa huyo hana tena maambukizi na anaendelea kupata nafuu.

**Algeria imekuwa nchi ya pili Afrika kuthibitisha kupata mgonjwa wa virusi vya Corona.**

Algeria ni moja ya nchi ambazo zimezua wasiwasi mkubwa kwamba virusi vya Corona huenda vikawa janga.

Naibu Waziri wa Afya wa Algeria, Iraj Harirchi, alikanusha madai kwamba nchi hiyo inajaribu kuficha ukweli kuhusu mlipuko wa virusi hivyo.

Iran imeripoti matukio 95 ya virusi vya Corona lakini idadi kamili inadhaniwa kuwa juu zaidi.

Mkurugenzi wa Shirika la Afya Dunia (WHO) alisema kwamba kuongezeka ghafla kwa visa hivyo kwa nchi ambazo ziko nje ya China ni jambo la kutia wasiwasi.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, alisema kwamba Washington ilikuwa na hofu kuwa Iran huenda imeficha taarifa muhimu kuhusiana na mlipuko wa ugonjwa huo na kusihi nchi zote kusema ukweli kuhusu virusi vya Corona.

Wakati huo huo, Naibu Waziri wa Afya na mbunge mmoja nchini Iran walithibitishwa kupata virusi vipya vya Corona, wakati inapambana kukabiliana na virusi hivyo ambavyo vimesababisha vifo vya watu 15.

Idadi kubwa ya watu wamefariki nchini Iran kwasababu ya virusi hivyo kuliko nchi nyingine yoyote mbali na China. Nchi hizo mbili zina uhusiano mkubwa wa kibiashara.

Nchi zingine ambazo kwa sasa zimekumbwa na mlipuko wa virusi vya Corona kwa kiwango kikubwa ni Korea Kusini na Italy ambapo matukio hayo yamekuwa yakiongezeka katika siku za hivi karibuni.

**Wakati huohuo,** Watu 78,064 wameambukizwa virusi vya ugonjwa wa Corona na kusababisha vifo vya watu 2,715 nchini China tangu ugonjwa huo ulipozuka Desemba mwaka jana. **BBC**




Raia wa China wakisalimia kwa kupungiana pasipo kushikana mikono kuhofia kuambukizana virusi vya Corona. **PICHA: REUTERS**

## Waliofariki kutokana na vurugu wafikia 20

**NEWDELH,** India

IDADI ya vifo kutokana na maandamano ya kupinga sheria mpya ya uraia mjini New Delhi, imepanda na kufikia watu 20.

Ghasia hizo ambazo ni mbaya zaidi kuwahi kushuhudiwa katika mji huo mkuu wa India katika miongo mingi, zilianza Jumapili jioni lakini zikaongezeka Jumatatu wakati Rais wa Marekani, Donald Trump alipowasili New Delhi kufanya mazungumzo na viongozi wa India.

Hospitali kuu ya mjini humo imethibitisha idadi hiyo ya vifo ikisema kuwa iliwapokea watu 189 waliopata majeraha. Polisi 40 ni miongoni mwa waliojeruhiwa.

Sheria hiyo mpya inarahisisha mchakato wa kutoa vibali vya uraia kwa jamii za kidini za walio wachache kutoka nchi jirani zenye raia wengi Waislamu, lakini orodha hiyo inawatenga Waislamu.

Wakosoaji wa sheria hiyo wanasema inawabagua Waislamu wa India walio wachache. Waziri Mkuu wa India Narendra Modi ametoa wito wa kurejeshwa utulivu akisema kuwa amani na maelewano ndio utamaduni wa nchi hiyo. **DW**

# Makamu wa Rais Sudan Kusini ajihisi mfungwa

**JUBA,** Sudan Kusini

MKE wa Makamu wa Rais wa Sudan Kusini aliyeapishwa hivi karibuni, Riek Machar, amesema mume wake anahisi ni kama mfungwa.

Angelina Teny, ambaye ni waziri wa zamani katika serikali ya Sudan Kusini, alisema kwamba masharti yaliyowekwa na Mamlaka ya kimaendeleo ya serikali za kikanda (Igad), kwa mume wake juu ya kusafiri ndani na nje ya nchi bado yapo.

Alisema masharti hayo yalilenga kusitisha mapigano na kumwezesha Machar kufanya mazungumzo ya mkataba wa amani. Pia walimuwekea masharti juu ya kuongea hadharani kwa vyombo vya habari.

Mjumbe maalumu wa Igad kwa ajili ya Sudan Kusini, Ismail Wais alisema kuwa masharti hayo yalipitwa na wakati wakati Machar alipochukua mamlaka mapya katika serikali ya umoja Jumamosi.


Lakini Teny alisema kuwa kundi la Machar halijapokea mawasiliano yoyote kuhusiana na hilo. Alisema wanahofia huenda asiweze kutekeleza kazi zake.

Kwa mujibu wa Teny, mume wake hawezi kusafiri kwa uhuru ndani ya Sudan kukutana na wafuasi wake.

Hatahivyo, msemaji wa Rais Salva Kiir amekanusha madai hayo, na kuongeza kuwa Machar anapaswa kufanya mikutano ya umma na rais ili kuonyesha umoja.

Awali Rais wa Sudan Kusini, Salva Kiir na kiongozi huyo wa zamani wa waasi Riek Machar walikubaliana kuunda serikali ya mpito ya Umoja ya Taifa, kabla ya Februari 22.

Inaaminiwa kuwa hatua ya Machar kujiunga na serikali ya muungano na Rais Kiir itasaidia kurejesha amani ya kudumu nchini Sudan Kusini, lakini mikataba mingi ya amani imekua ikivunjwa mara kwa mara. **BBC**




Meneja Mwandamizi wa Bima NMB, Martine Massawe (kulia), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 35 kwa Mkurugenzi Mtendaji wa African Digital Banking Summit Limited, Baraka Mtavangu, kwa ajili ya NMB Bima Marathon itakofanyika tarehe 28 Machi jijini Dar es Salaam. Katikati ni Meneja wa NMB Jogging Club, Elifadhili Mramba. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wazee waiomba serikali bajeti ya dawa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

BAADHI ya wazee katika Wilaya ya Kibaha, mkoani Pwani, wameiomba serikali kuwatengea bajeti kwa ajili ya dawa kuondoa changamoto inayowakabili kwasasa.

Wakiongea na Nipashe kwa nyakati tofauti jana mjini Kibaha, walisema kwasasa wanakabiliwa na changamoto ya kukosa dawa kwenye vituo vya huduma ya afya wanapoenda kupata matibabu.

Getrude Msangule, mkazi wa Mwendapole B, alisema serikali inatakiwa kuandaa mkakati wa kuwezesha uwapo wa dawa kwa wazee, kwa kuwa wengi wao hawana uwezo wa kununua wanapozikosa kwenye vituo vya afya.

Alisema, kwa sasa kila zahanati ina dirisha na daktari kwa ajili ya wazee, changamoto iliyopo kwa sasa ni ukosefu wa dawa jambo ambalo baadhi yao wanashindwa kununua na kuendelea kuugua magonjwa yanayowasumbua.

"Huduma kwenye vituo zinaridhisha, tunapokwama ni pale tukifika dirisha la dawa, utaambiwa hakuna kila siku zinapatikana panadol pekee nyingine unaandikiwa ukanunue nje, wengine hawana uwezo wa kuzinunua hili linatakiwa kuangaliwa na serikali kuwasaidia," alisema.

Vile vile, alisema kitengo kinachohusika na wazee, hawatakiwi kukaa ofisini badala yake wafike kuwatembelea wazee na kupata takwimu halisi ya wale ambao hawajiwezi wasaidiwe namna ya kupata dawa.

Aliomba serikali pia, kutoa semina za mara kwa mara kwa vijana wanaopata mimba mapema, kwa kuwa kwa kukosa kwao elimu wamekuwa wakizaa watoto ambao wanashindwa kuwalea na baadaye wanawatelekeza kwa wazee ambao wanashindwa kumudu kuwalea.

Naye Mohamed Pongwe mkazi wa Mlandizi, aliiomba serikali kusaidia wazee kupata bima iliyoboreshwa, ili waweze kupata dawa wanapoumwa.

Mkurugenzi wa Shirika linalojishughulisha na wazee la Msamaria mwema, Elisha Mwamkinga, alisema kila halmashauri inatakiwa kuandaa utaratibu wa kutenga bajeti kwa ajili ya kuwasaidia wazee wasiojiweza.

"Wapo wazee hata wakiandikiwa dawa uwezo wa kununua hawana, ikiwezekana hata serikali za mitaa zianzishe utaratibu wa kuwakatia bima iliyoboreshwa wazee kuondokana na hii hali," alisema Mwamkinga.

Mwamkinga alisema, pia kwasasa wapo kwenye mchakato wa kudai haki za wazee wasinyanyaswe au kubaguliwa kutokana na umri wao.

# Taasisi yajulikana kimataifa utafiti mbung'o

**Na Dege Masoli,** PANGANI

TAASISI ya Utafiti wa Wadudu na Magonjwa Waenezayo (VVBD) imejitambulisha kitaifa na kimataifa kutokana na kufikisha zaidi ya mbung'o 16,000 wanaofugwa na kituo hicho.

Meneja wa Wakala wa Maabara ya Veterinari (TVLA) Tanga, Dk. Amni Malele, alisema jana kuwa kituo hicho hadi mwishoni mwa mwaka jana, kilifikisha mbung'o 16,143 idadi ambayo imekifanya kufahamika kitaifa na kimataifa.

Dk. Malele alisema ufugaji wa mbung'o hao umekuwa utambulisho wa taasisi hiyo iliyoko chini ya TVLA na kwamba inawatumia mbung'o hao kama sehemu ya utafiti wao.

"Ufugaji wa mbung'o umekuwa ndio utambulisho wa taasisi kitaifa na kimataifa toka ilipoanzishwa. Kwa sasa inajulikana kama kituo cha umahiri katika uzalishaji mbung'o," alisema Dk. Malele.

Alisema ufugaji huo wa mbung'o umeendelea takriban miaka 46 na hadi mwaka jana ilishafikiwa mbung'o pamoja na mabuu 3,895 ambayo hayajaanguliwa.

"Mbun'go hawa wanafugwa kwa ajili ya shughuli za utafiti, mafunzo na mbegu, pia wanaweza kutumika kuondoa mbung'o katika nyanda za malisho ya mifugo chini kupitia madume," alisema.

Meneja huyo alisema mafanikio hayo yametokana na ushirikiano baina ya kituo hicho na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi katika kutekeleza majukumu yake yakiwemo mashirika ya kimataifa, mtandao wa kutokomeza malale, vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi na serikali za mitaa.

# Shule Dar yaomba msaada kompyuta

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya Msingi Kawe B ya jijini Dar es Salaam, imeomba msaada wa kompyuta na mashine ya kudurufia kwa ajili ya kusaidia uchapaji wa mitihani ya majaribio shuleni hapo.

Ombi hilo lilitolewa jana na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Venance Mwasamakwela wakati akipokea madarasa ya shule hiyo yaliyokarabatiwa na asasi ya Time To Help na shule za Feza.

Alisema kwa sasa wamekuwa wakitumia gharama kubwa kwenda kuchapisha mitihani ya majaribio mtaani, wakati hawana kipato cha kuwawezesha kumudu gharama hizo. Mwasamakwela alisema baada ya ukarabati huo, shule hiyo itafanya vizuri zaidi kitaaluma na kwamba imekuwa ikifanya vizuri kitaaluma hivyo msaada huo umekuwa chachu kwao kufanya vizuri zaidi kwenye mitihani ya kitaifa ya darasa la nne na darasa la saba.

Alisema mwaka uliopita shule hiyo ilijitahidi na kufaulisha wanafunzi wote kwenye matokeo ya darasa la saba na kwamba kwa msaada walioupata watafanya vizuri zaidi.

"Msaada ambao Time To Help na shule za Feza mmekuwa mkitupatia umetufanya tuwaone nyinyi ni walezi wetu, shule yetu ilikuwa kwenye hali mbaya sana, lakini nyinyi mmeifanya iwe tofauti kabisa," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

**SHULE YA CHEKECHEA INAKODISHWA**
Shule ya Chekechea inakodishwa au ubia, pia yaweza kubadilishwa na kuwa kituo cha Elimu au kituo cha Afya . Ipo Mbezi Luis. Kwa mawasiliano: **0712 480 836 / 0765 138 779.**


NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI
BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA


## KUPOTEA KWA CHETI



**Honest Evarist** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo;cheti kidato cha nne chenye **index namba S1189-0331** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2009 katika shule ya Sekondari Biafra, cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0101-0636** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2012 katika shule ya Sekondari Azania, cheti cha Degree ya Sheria kilichotolewa na University of Dar es Salaam mwaka 2016.

**Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa: DAR/RB/6776/2020**

115648102

## KUPOTEA KWA CHETI



**LEAH WILFREDY MACHA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **2028/026** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MARINGENI SEKONDARI** mwaka 2012. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MAR/RB/1398/19.**

115647902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo KIMARA**

**Usimamizi wa mirathi No;18/2020**

Ombi la DICKDANIEL GAUDENCE MGUNDA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu GABRIEL GAUDENCE MGUNDA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 6/4/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 03/02/2020.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO KIMARA

215648202

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

TANZANIA CHINA TRADE AND TOURISM DEVELOPMENT ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA SINORAY YENYE NAMBA ZA USAJILIMC856CJG

KWAYOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

TAARIFA YA POLISI
KAH/ /RB/ 1086/2020

156486

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**TANZANIA CHINA TRADE $ TOURISM DEVELOPMENT LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **FEKON** yenye namba za usajili **T 904 CJB.** Chassis no LDAPAKOB 2CGB28204. Engine no 162 FMJ1112030838.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya Polisi
**DOD/DOD/RB/25923/2020**

156485

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF MWANZA AT MWANZA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 01/ OF 2020 IN THE MATTER OF THE PROBATE AND ADMINISTRATION OF ESTATE ACT**
**AND**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE OSCAR LUTHER KAZAULA**
**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR APPOINTMENT OF EXECUTOR OF THE ESTATE OF OSCAR LUTHER KAZAULA BY ESTER MGORE MARONGA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **06th** day of **March, 2020**

The will of the said deceased is deposited and open for inspection at the Court.

Dated at Mwanza this **14 day** of **February, 2020**

RESIDENT MAGISTRATE
MWANZA

COPY TO
Advocate REAGAN CHARLES,
BOX 2369
MWANZA

215648002


Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa
Kutangaza Nasi
Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Nipashe
MWANGA WA JAMII

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# ARSENAL SASA IPO TAYARI KUMUUZA AUBAMEYANG



**LONDON,** England

ARSENAL imeripotiwa kwamba ipo tayari "kusikiliza" ofa kutoka klabu yoyote inayomtaka nahodha wake, Pierre-Emerick Aubameyang wakati wa kipindi cha majira ya joto, baada ya hadi sasa kushindwa kumshawishi mshambuliaji huyo kusaini mkataba mpya.

Aubameyang, ambaye kwa sasa anaongoza kwa ufungaji bora kwenye Ligi Kuu ya England akiwa na mabao 17, amebakiwa na miezi 12 kwenye mkataba wake na Arsenal wapo hatarini kumpoteza akiwa mchezaji huru mwaka 2021 kama hawatamuuza au kushindwa kumshawishi kuongeza mkataba mpya.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail klabu hiyo inapanga kufungua mazungumzo na Aubameyang kujadiliana kuhusu majaliwa yake, kitu kinachoweza kuwafanya waamue kumuweka sokoni mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30.

Arsenal awali walishindwa kumshawishi kuongeza mkataba mpya na Aubameyang alikuwa akihusishwa na mpango wa kujiunga na Barcelona wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari.

Inadaiwa kwamba Aubameyang mchezaji wa kimataifa wa Gabon anataka kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku Arsenal ikiwa shakani kufuzu kwenye michuano hiyo.

Aidha, taarifa zaidi zinaeleza kwamba Aubameyang anataka kulipwa mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki sawa na Mesut Ozil.

# Barcelona yaivutia Napoli pumzi

**NAPLES,** Italia

QUIQE Setien amesema bado ana matumaini ya Barcelona kufuzu kutoka hatua ya 16-Bora kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, licha ya kwamba atawakosa Sergio Busquets na Arturo Vidal kwenye mchezo wa marudiano dhidi ya Napoli wiki tatu zijazo.

Barça walilazimishwa sare ya 1-1 na Napoli kwenye Uwanja wa San Paolo Jumanne, huku bao lao likifungwa na Antoine Griezmann.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa alisawazisha bao la kipindi cha kwanza la Dries Mertens, akiunganisha krosi ya Busquets.

Busquets ambaye alipata kadi ya njano kipindi cha pili, inamfanya kuukosa mchezo wa marudiano, huku Vidal atakuwa benchi pale Camp Nou baada ya kupewa adhabu kwenye tukio la kuzozana na Mario Rui.

Hata hivyo, Setien hana shaka kwani ana imani watafuzu kwenye mchezo ujao ambao pia watamkosa beki wao Gerard Pique aliyeumia.

"Tutaangalia suluhisho jingine," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Tumewapoteza wachezaji muhimu, lakini wengine wawili wamepona Jordi Alba na Sergi Roberto.

"Tutaangalia namna ya kuukabili mchezo wetu huo ujao. Bado nina matumaini makubwa ya kufanya vizuri."






# United yafikia pazuri kumsajili Grealish

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imeongeza hatua zaidi katika mpango wake wa kutaka kumsajili nyota wa Aston Villa, Jack Grealish.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 kwa kipindi chake chote amecheza hapo Villa Park ikiwa ndio klabu yake ya utotoni na iliyomlea, lakini majaliwa ya Grealish yapo shakani kwani Aston Villa kwa sasa wanapambana kutoshuka daraja pamoja na Watford na West Ham.

United ni moja kati ya klabu za Ligi Kuu ya England zinazomuwania Grealish ambaye wanaweza kumsajili mwishoni mwa msimu huu.

Gazeti la Manchester Evening News limeripoti kwamba, klabu hiyo itatuma ofa yao mapema mwishoni mwa mwezi huu.

Ingawa Grealish hataweza kujiunga na Manchester United hadi dirisha la usajili litakapofunguliwa kipindi cha majira ya joto, kikosi hicho cha Ole Gunnar Solskajer kinaonekana kinataka kumalizana mapema na mchezaji huyo kabla ya Machi.

Taarifa zaidi zinasema kwamba, Man United wamekubali kulipa fedha kiasi cha pauni milioni 45 kilichopo kwenye kipengele cha mkataba wake ili aachiwe kutoka pale West Midlands.

Man United tayari ilianza kuimarisha kikosi chake wakati wa dirisha la usajili wa dirisha dogo la Januari wakati walipomsajili Bruno Fernandes.

Grealish awali alikuwa akihusishwa na kutakiwa pale Tottenham Hotspur, ambapo walishindwa kumsajili mwaka 2018 kwa ada iliyotajwa kuwa ni pauni milioni 25.

## HABARI MICHEZO

# Sancho haondoki Dortmund msimu huu

**DORTMUND,** Ujerumani

KUNA uwezekano mkubwa Jadon Sancho atabakia katika klabu ya Borussia Dortmund baada ya msimu huu kumalizika.

Sancho mwenye umri wa miaka 19, amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia kwenye Ligi Kuu ya England baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia kwa miamba hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Lakini winga huyo wa kimataifa wa England sasa anaonekana wazi kwamba ataendelea kubaki hapo Dortmund.

Sancho ameripotiwa kwamba ana furaha kuendelea kucheza pale Dortmund na uwezekano wa kuondoka mwishoni mwa msimu huu ni mgumu kwa mujibu wa gazeti la kila siku la Ruhr Nachrichten la nchini Ujerumani.

Kinda huyo mkataba wake wa sasa na klabu hiyo unamalizika mwaka 2022 na hivyo msimu ujao wa 2020-21 ataendelea kucheza Dortmund.

Klabu za Liverpool, Manchester City, Manchester United na Chelsea zimetajwa kwamba zipo kwenye mbio moja za kumwania Sancho.





# LAMPARD: KIPIGO CHA BAYERN KIMETUPA SOMO

**LONDON,** England

FRANK Lampard ameitaka Chelsea kujifunza na kuelewa namna wanavyotakiwa kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano baada ya kipigo walichokipata kutoka kwa Bayern Munich.

Chelsea walipoteza kwa kufungwa mabao 3-0 kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya mtoano wa 16-bora dhidi ya mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Jumanne, huku Serge Gnabry akifunga mawili na Robert Lewandowski moja pale katika dimba la Stamford Bridge.

'Blues' hao walimpa presha nyingi golikipa wa Bayern, Manuel Neuer, huku wakimpoteza mchezaji wao Marcos Alonso aliyelimwa kadi nyekundu baada ya VAR kumwonyesha akifanya faulo ya makusudi.

Na sasa Lampard anajua kuhusu timu yake inavyotakiwa kujifunza kutoka kwenye mchezo huo na alisema kuna somo amepata.

"Hii ndilo soka la daraja hili," alisema Lampard akiwaambia waandishi wa habari. "Kiwango cha Bayern Munich kilikuwa cha kuvutia, kwa hakika ni timu imara, nilikuwa najua hilo.

"Mchezo uliokuwa mgumu kwetu, na tumejifunza na naamini wachezaji wangu wamejifunza jinsi ya kucheza kwenye hatua hii.

Ingawa alikataa kukata tamaa ya kufuzu kwenye mchezo wa marudiano machi 18, lakini Lampard alisema kipaumbele cha Chelsea kwa sasa ni kuhakikisha wanamaliza kwenye nne bora ya Ligi Kuu ya England.

# *Gattuso aipania Barca Camp Nou*

**NAPLES,** Italia

KOCHA wa Napoli, Gennaro Gattuso amesema watanunua "helmets" ya kujilinda ili kuhakikisha wanashinda mchezo wao wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano wa timu 16-Bora dhidi ya Barcelona.

Licha ya kuanza kuongoza kwa bao la Dries Mertens, ambaye alifikia rekodi ya kuwa mfungaji bora wa wakati wote wa Napoli, miamba hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, walilazimishwa sare ya 1-1 nyumbani, juzi Jumanne.

Antoine Griezmann aliisawazishia Barca kipindi cha pili, huku miamba hao wa LaLiga wakimpoteza Arturo Vidal aliyetolewa nje kwa kadi nyekundu dakika za mwisho. Na Gattuso amesema timu yake ipo tayari kwa ajili ya mpambano wa marudiano pale Camp Nou Machi 18.

"Mambo hayajaisha kwa upande wetu hasa tukiwa tunacheza hatua hii ya 16 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya," alisema Gattuso akiwaambia waandishi wa habari.

"Tunajua kwamba tutakuwa na wakati mgumu kule. Tutanunua helmets (kofia ngumu) kwa ajili ya kujilinda.

"Tutakwenda na vifaa vyetu vyote muhimu na tutacheza mchezo huo kwa nguvu zote kwa sababu bado nafasi ipo na mambo hayajaisha bado."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# LEWANDOWSKI AMFIKIA RONALDO REKODI UEFA

Ni ya mabao wakati Bayern ikiisambaratisha Chelsea na kuendelea kutesa timu za...

**LONDON** England

ROBERT Lewandowski ameifikia rekodi bora ya mabao ya ugenini kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyowekwa na Cristiano Ronaldo wakati akiiongoza Bayern Munich kuichapa Chelsea katika michuano hiyo.

**Lewandowski alifunga bao moja na kutoa pasi za mwisho mbili wakati vinara hao wa Bundesliga wakiibuka na ushindi wa mabao 3-0 katika Uwanja wa Stamford Bridge kwenye mechi ya mkondo wa kwanza ya hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi.**

Straika huyo wa Bayern, Lewandowski alishirikiana vema na Serge Gnabry kwa ufanisi kwa kumtengenezea mabao mawili yaliyopishana kwa dakika tatu, kabla ya kuunganisha nyavuni krosi ya Alphonso Davies kukamilisha ushindi huo.

Lewandowski sasa amefikisha mabao 11 katika mechi saba za Ligi ya Mabingwa, rekodi bora zaidi kwake kwenye msimu mmoja, wakati pia ameifikia rekodi ya Ronaldo ya kufunga mabao tisa mechi za ugenini katika michuano hiyo ya Ullaya ambayo Mreno huyo aliiweka msimu wa 2013-14.

Kwa kushangaza, nyota huyo wa Poland alicheza kwa dakika 672 bila kuziona nyavu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano kabla ya kufunga bao hilo juzi.

Ushindi huo wa Bayern unamaanа wamefunga mabao matatu ama zaidi kwenye mechi za ugenini dhidi ya timu nne tofauti za England katika michuano hiyo tangu mwaka 2013 - ilipoichapa Arsenal mara mbili, Tottenham na sasa Chelsea.

Wigo huo wa kipigo hicho, ndicho kikubwa zaidi kwa Chelsea kuwahi kukipata nyumbani kwenye michuano yoyote ya Ulaya katika historia ya klabu hiyo.

Wakati Lewandowski na Gnabry wakihusika kwa mabao hayo, kilikuwa ni kiwango bora zaidi cha beki kinda wa pembeni, Davies kilichokodolewa macho.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, alikuwa na kasi ya kutisha na pia alimsumbua sana beki wa kushoto wa Chelsea, Reece James na kumpa kazi kubwa ya kukaba.

## ZISIKUPITE

### YAJIONGEZA KWA GREALISH

MANCHESTER United imepiga hatua katika mkakati wao wa kumsajili kiungo wa Aston Villa, Jack Grealish, 24. ***(Manchester Evening News)***

### AUBAMEYANG ANUKIA KUUZWA

ARSENAL inaweza kusikiliza ofa kwa Pierre-Emerick Aubameyang majira haya ya joto ili kuepuka kumpoteza bure mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, mwaka ujao. ***(Mail)***

### GUARDIOLA AWANIWA JUVE

RAIS wa Juventus, Andrea Agnelli amesema mabingwa hao wa Italia wanazingatia kutoa ofa kwa kocha wa Manchester City, Pep Guardiola. ***(Manchester Evening News)***

### RAMOS HANA HARAKA MADRID

BEKI wa Real Madrid, Mhispania Sergio Ramos, 33, hana haraka ya kujadili mkataba mpya na miamba hiyo ya Bernabeu lakini amesema uhusiano wake na klabu hiyo ni "mkubwa". ***(Goal)***

### MANE KUIGHARIMU BARCELONA

KIPENGELE cha mkataba wa Philippe Coutinho, inamaana Barcelona itapaswa kulipa pauni milioni 225 ili kumsajili kiungo wa Senegal, Sadio Mane, 27. ***(Mirror)***

### STERLING MGUU NJE NDANI CITY

MANCHESTER City inaweza kuwapoteza wachezaji wake wengi muhimu, ikiwa ni pamoja na mshambuliaji Raheem Sterling, kama itatwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu. ***(ESPN)***

### LINGARD, PEREIRA KUUZWA

MANCHESTER United inaweza kumuuza mshambuliaji wa England, Jesse Lingard, 27, na kiungo Mbrazil Andreas Pereira, 24, mwishoni mwa msimu. ***(Express)***

### YAVUTIWA NA CUCURELLA

ARSENAL inavutiwa na beki wa kushoto wa Hispania U-21, Marc Cucurella na ipo tayari kulipa pauni milioni 20 kama dau linalohitajika ili kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, ambaye anacheza kwa mkopo Getafe akitokea Barcelona. ***(Cadena Cope via Sport Witness)***

### AMFIKIRIA ARRIZABALAGA

KIPA wa Hispania, Luis Enrique anazingatia kuhusu kipa wa Chelsea, Kepa Arrizabalaga, 25, kukosa nafasi ya kuanza mara kwa mara wakati huu akiandaa mipango yake ya michuano ya Ulaya majira ya joto. ***(AS - in Spanish)***

### KROOS AZIDI KUIOTA UNITED

KIUNGO wa Real Madrid, Mjerumani Toni Kroos, 30, amesema mkataba wake na Manchester United "kimsingi ulikamilika" kabla ya kocha David Moyes kutimuliwa. ***(The Athletic)***

### WENGER AMFUNGUKIA GNABRY

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger amesema alijua winga wa Bayern Munich, Mjerumani Serge Gnabry, 24, angebaki na 'Gunners' hao. ***(beIN Sports, via Metro)***

## Mdhamini Bima Marathon 2020 hadharani

**Ma Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB, imetangazwa kuwa Mdhamini Mkuu wa Mbio za Bima Marathon 2020, zinazotarajiwa kufanyika Machi 28, mwaka huu jijini Dar es Salaam, chini ya uratibu wa Kampuni ya African Digital Banking Summit.

Kwa udhamini huo, mbio hizo zinazoenda kufanyika kwa mara ya pili mfululizo, zitatambulika kwa jina la NMB Bima Marathon 2020, ambazo zitahusisha mbio za kilomita 21, kilomita 10 na kilomita tano.

NMB imedhamini mbio hizo kwa kitita cha Sh. milioni 35, ambako hafla ya NMB kutangaza udhamini wake huo katika mashindano hayo imefanyika jana jijini Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa kukabidhi mfano wa hundi ya udhamini, Meneja Mwandamizi wa Bima wa NMB, Martin Massawe, alisema wamevutiwa kudhamini Bima Marathon kutokana na mlengo wake.

"Mashindano haya yanatumika kama jukwaa la kutoa elimu ya Bima kwa Watanzania, lakini kuimarisha afya. Nasi tumeona ni fursa tunayoweza kuitumia kutangaza huduma mpya ya Bancassuarance.

"Lakini hii si mara ya kwanza kwetu NMB kudhamini michezo, tumefanya hivyo katika soka ambako tumeidhamini Taifa Stars na timu za Azam FC na Singida United. Tumefanya hivyo pia katika mpira wa magongo, gofu na kriketi na kadhalika," alisema Massawe.

## Simba Queens, Yanga Princess

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha Simba Queens kinatarajia kuwakaribisha Alliance Girls katika mechi ya raundi ya 10 ya Ligi Kuu Wanawake Tanzania (SWPL), itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Mo Simba Arena jijini Dar es Salaam wakati Yanga Princess itawaalika Marsh Queens katika Uwanja wa Karume Ilala.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Mashindano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Baraka Kizuguto, alisema maandalizi ya mechi zote yanakwenda vizuri na tayari wachezaji waliokuwa katika timu za Taifa wameshaof ripoti katika klabu zao.

Kizuguto alisema anaamini mechi za ligi hiyo zitaendelea kuwa na ushindani na hiyo itachangia kuwaimarisha wachezaji ambao matunda yake yanaonekana katika kupeperusha bendera ya nchi kwenye michuano ya kimataifa.

Alizitaja mechi nyingine zitakazochezwa leo ni kati ya Mlandizi Queens dhidi ya TSC Queens kwenye Uwanja wa Mabatini, Pwani wakati Panama Girls wataivaa Baobab Queens, Ruvuma Queens wakiwakaribisha Tanzanite huku JKT Queens wakichuana na Kigoma Sisterz kwenye Uwanja wa Isamuhyo.

Alliance Gilrs yenye pointi 25 ndio vinara wa ligi hiyo wakifuatiwa na Simba Queens wenye pointi 23 na Ruvuma

# KILI CANVAS HABARI YA MJINI MOSHI

**Na Mwandishi Wetu**

KILI Canvas iliyozinduliwa na Kampuni ya Bia Tanzania (TBL), kupitia Bia yake ya Kilimanjaro Premium Lager hivi karibuni jijini Dar es Salaam, kwa sasa ndio habari ya Mjini Moshi mkoani Kilimanjaro kwa wakazi na wageni wanaotarajia kushiriki kilele hicho.

Canvas ina lengo la kuhamasisha wakimbiaji wa vitongoji mbalimbali wa Mkoa wa Kilimanjaro na wageni kutoka mataifa mbalimbali kuelekea kilele cha mbio za Kili Marathon zinazotarajiwa kufanyika Machi Mosi, 2020 mkoani Kilimanjaro

Kili Canvas ni picha maalumu iliyochorwa kwa ukubwa na msanii wa Sanaa ya Uchoraji, Athumani Hamis (Ochu) ambapo mkimbiaji yeyote akipita karibu yake anapigwa picha na picha hiyo yenye muunganisho wa teknolojia ya kisasa baadaye kumtumia picha hiyo kupitia simu yake ya mkononi.

**Hata hivyo, mkimbiaji anatakiwa kujisajili na kupewa 'chip maalumu' ambayo anatakiwa kuwanayo kwa maelekezo ya wataalamu hao.**

Meneja wa Bia ya Kilimanjaro Premium Lager, Irene Mutiganzi, alisema baada ya wakazi wa jiji la Dar es Salam kushuhudia Kili Canvas inavyofanya kazi, sasa ni zamu ya wakazi wa Manispaa ya Moshi na vitongoji vyake pamoja na wageni wote kutoka mataifa mbalimbali kupiga picha kwenye Canvas hiyo kama kumbukumbu maalumu ya ushiriki wako wa Kili Marathon 2020.

"Kwa sasa Kili Canvas tumeiweka pale Keys Hoteli usikose kufika kujiandikisha kupiga picha na kuwa na kumbukumbu maalumu ya Kili Marathon 2020.

Mwisho Irene aliwahimiza Watanzania tujitokeze kwa wingi mwaka huu kushiriki kilele cha mbio za Kili Marathon kama waandaaji kwani nchi zaidi ya 52 kutoka Mataifa mbalimbali wameshadhibitisha kushiriki kwa kujiandikisha.



Meneja mpya wa Kilimanjaro Premium Lager, Irene Mutiganzi, akipiga picha kwenye Kili Canvas iliyochorwa na Msanii wa Sanaa ya Uchoraji, Athuman Hamis (Ochu), katika Mtaa wa Kilimanjaro Avenue Manispaa ya Moshi mjini jana, ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha jamii kufanya mazoezi kwa ajili ya afya na kujiandaa na kilele cha mbio za Kili Marathon zinazotarajiwa kufanyika mwishoni mwa wiki hii, Machi Mosi 2020 mkoani Kilimanjaro. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Chama afunguka Simba inavyosaka mataji Bara*

**Na Saada Akida**

KIUNGO wa kimataifa wa Simba, Clatous Chama, amesema wachezaji wa timu hiyo wameahidi kuendelea kupambana kwa sababu bado hawajaridhika na nafasi waliyopo katika Ligi Kuu Bara.

Hata hivyo, Simba yenye pointi 62 iko kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 62 ikifuatiwa na Azam FC yenye alama 45 huku Namungo iliyoko nafasi ya tatu ina 43 na Yanga wanashika nafasi ya nne pointi zao 41, lakini wakiwa na mechi mbili mkononi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Chama alisema wao kama wachezaji ni kuona wanafikia malengo waliyoyaweka katika msimu huu kwa asilimia 100, hivyo kila mechi watakayoshuka uwanjani ni sawa na fainali.

Chama alisema kwa sasa wana kazi ya kuhakikisha wanashinda kila mechi wanayocheza ya Ligi Kuu Bara pamoja na mashindano ya Kombe la FA ili wajihakikishie nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa.

Mzambia huyo alisema anajua ushindani wanaokutana nao kwa sababu timu zote wanazokutana nazo zimejipanga vema kusaka ushindi ili kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi na kusonga mbele katika mashindano ya Kombe la FA.

"Tuna kazi kubwa ya kufanya katika mashindano tunayoshiriki, kufanya vizuri kwenye Kombe la FA, na ni imani yetu kuona tufanya vizuri na kupata matokeo chanya ili kujiweka katika nafasi nzuri iwe ligi au FA," alisema kiungo huyo.

Chama alikuwa mmoja wa wachezaji wa Simba walioiondoa Stand United kwa ushindi wa penalti 3-2 baada ya kumaliza dakika 90 za kawaida kwa sare ya bao 1-1. Timu nyingine zilizotinga hatua ya robo fainali kabla ya mechi za jana jioni ni pamoja na Namungo FC, Sahare All Stars na Ndanda FC.

# Michezo

Alhamisi Februari 27, 2020

Nipashe




Lewandowski amfikia Ronaldo rekodi Uefa UKURASA 30

NIFUTE KIATU...



Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, akimpongeza kiungo wa timu hiyo Haruna Niyonzima, kwa kumfuta kiatu baada ya kuifungia timu hiyo bao pekee wakati ikishinda 1-0 dhidi ya Gwambina FC kwenye mechi ya hatua ya 16-Bora, iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Penalti ya Kagere yaua shabiki Dar

**Na Mwandishi Wetu**

PENALTI aliyokosa mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere wakati Simba ikiitoa Stand United kwa changamoto ya mikwaju ya penalti 3-2 kwenye mechi ya hatua ya 16-Bora, ya Kombe la FA, imesababisha kifo cha shabiki wa timu hiyo, mkazi wa Jeti- Lumo jijini Dar es Salaam, Pacience Mhagama.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga juzi, timu hizo zilizoka sare ya bao 1-1 baada ya dakika 90, ndipo changamoto ya mikwaju ya penalti ilipochukua nafasi yake na Kagere akiwa mpigaji wa tuta la kwanza, alikosa.

Hata hivyo, Claotus Chama, Deo Kanda na Hassan Dilunga walifunga penalti zao huku Ibrahim Ajibu naye akikosa, lakini Stand United nayo ikajikuta ikikosa tatu na hivyo Simba kutinga hatua ya robo fainali.

Akizungumza na mwandishi wetu, mtoto wa marehemu Mhagama, Edwin alisema baba yake alikuwa akiangalia mechi na rafiki zake nyumbani na baada ya Kagere kukosa penalti alianguka ghafla na kupoteza fahamu.

"Mimi sikuwa nyumbani, ila marafiki zake waliokuwa wakiangalia naye mechi hiyo walinipigia simu na kunieleza kuwa baba ameanguka ghafla baada ya Kagere kukosa penalti na amepoteza fahamu.

"Wakati wanamkimbiza hospitali alifariki dunia wakiwa njiani, hivyo kwa sasa maiti ipo Hospitali ya Temeke na tunafanya taratibu ya kusafirisha kwenda kuzika Songea

# Niyonzima aibeba Yanga FA

### ●●● Apiga bao la mwaka, huko Azam FC na Kagera Sugar nazo zavuka kwa matuta...

**Na Somoe Ng'itu**

YANGA imefanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA baada ya kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Gwambina FC katika mechi ya hatua ya 16-Bora iliyochezwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana, huku mabingwa watetezi Azam wakisonga mbele kwa kuwafunga Ihefu kwa changamoto ya penalti 5-4.

**Bao pekee lililowapa ushindi Yanga lilifungwa na kiungo Mnyarwanda wa Yanga, Haruna Niyonzima sekunde chache kuelekea mapumziko, baada ya kupiga shuti la mbali ambalo lilikwenda moja kwa moja wavuni na kumwacha golikipa wa Gwambina, Ibrahim Isihaka akijaribu kuruka bila mafanikio.**

Katika kuonyesha heshima, Kocha Mkuu wa Yanga Mbelgiji Luc Eymael, alifuta vumbi kiatu cha Niyonzima akimaanisha kutoa heshima kwa bao aliloifungia timu yake kuwa na kiwango cha juu.

Hata hivyo, Yanga ndiyo ilikuwa ya kwanza kufanya mashambulizi katika mechi hiyo ambapo dakika ya tano Isihaka aliwahi kudaka krosi iliyopigwa vizuri na Bernard Morrison na kuwanyima Yanga bao la mapema huku Gwambina wakijibu shambulio hilo dakika sita baadaye.

Alikuwa ni mshambuliaji wa zamani wa Stand United, Jacob Massawe akimalizia krosi ya Pastory Athanas, lakini shuti lake lilizidi kipimo kidogo na kupaa juu ya lango na kuinyima timu yake hiyo inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza bao la kuongoza.

Dakika ya 39, Yanga ilipoteza nafasi nyingine ya kufunga kupitia kwa Morrison ambaye alipiga mpira nje akiwa jirani na lango la Gwambina na kuharibu kazi nzuri iliyofanywa na Mapinduzi Balama.

Kipa wa Azam FC, Razak Abalora jana alikuwa nyota wa mchezo baada ya kupangua penalti mbili za Ihefu na kufunga penalti ya ushindi kwa timu yake ambayo inashikilia ubingwa wa michuano hiyo inayotoa tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Azam ililazimika kusubiri matuta baada ya dakika 90 za kawaida kumalizika wakiwa suluhu na wenyeji wao Ihefu ambayo inashiriki Ligi Daraja la Kwanza.

Wachezaji wengine wa Azam waliofunga penalti katika mechi hiyo iliyochezeshwa na refa Athumani Lazi kutoka Morogoro ni pamoja na Obery Chirwa, Yakubu Mohammed, Neva Tekete na Bruce Kangwa, wakati Shabani Chilunda akipaisha penalti iliyofanya waanze kupigiana moja moja kufuatia tano kumalizika.

Katika mechi nyingine Kagera Sugar imesonga mbele baada ya kuwafunga kwa penalti 3-0 KMC FC ya Dar es Salaam, kufuatia sare ya bao 1-1 dakika 90 za kawaida huku Alliance nayo ikisonga mbele kwa mikwaju ya penalti 5-3 baada ya sare kama hiyo dhidi ya JKT Tanzania ndani ya dakika 90.

Timu nane zilizotinga hatua hiyo ni pamoja na Yanga, Azam FC, Simba, Namungo FC, Sahare All Star, Ndanda, Kagera Sugar na Alliance.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >